

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 30 June, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZO WASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi) kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHE. PAUL J. LWANJI (K.n.y. MHE. GEORGE M. LUBELEJE-MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2008/2009.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMAJI WA UPINZANI OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mwenzetu ambaye atauliza swali la kwanza napenda kuwafahamisha tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko ziara mikoani na ameniletea barua hapa kwamba anayekaimu kuongoza shughuli za Serikali humu Bungeni ni Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Waziri wanchi, Masuala ya Muungano. La pili natumaini mmekuwa na mapumziko mazuri ya mwisho wa wiki tunaianza tena wiki nyingine ya kazi ya kuendelea kuwawakilisha wananchi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Na. 122

**Kupeleka Waganga na Wauguzi – Zahanati ya
Kata ya Matanga**

MHE. ANNA R. LUPEMBE aliuliza:-

Kwa kuwa Zahanati ya Kata ya Matanga katika Manispaa ya Sumbawanga imefunguliwa tarehe 28/062006 pamoja na nyumba ya Mganga wakati wa mbio za Mwenge, lakini hadi sasa haijapata mganga wala muuguzi?

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupeleka Mganga na Muuguzi ili wananchi wa Kata hiyo waweze kupatiwa matibabu badala ya kwenda sehemu nyingine kutaka huduma ya matibabu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali halisi ya huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi wa Manispaa ya Sumbawanga hususan katika Kata ya Matanga kuwa si ya kuridhisha. Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ina zahanati 18 zinazomilikiwa na Serikali ikiwemo zahanati ya Matanga. Kwa sasa Halmashauri ina watumishi wa kada mbalimbali za afya wapatao 167 idadi hii ni sawa na asilimia 40 tu ya watumishi wanaohitajika.

Kwa mujibu wa mwongozo wa kitaifa uliotolewa na Wizara ya Afya na ustawi wa jamii, zahanati inapaswa kuwa na maafisa tabibu wawili (2) wauguzi wawili na mhudumu wa afya mmoja (1).

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuona umuhimu wa kusogeza huduma karibu na wananchi, ilijenga zahanati ya Matanga ambayo ilizinduliwa rasmi tarehe 28/06/2006. Pamoja na jitihada hizi za kusogeza huduma karibu na wananchi, bado Halmashauri hii inakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa watumishi wa kada za afya.

Kwa sasa zahanati ya Matanga ina wahudumu wa afya wawili tu, hivyo kuna upungufu wa maafisa tabibu wawili na wauguzi wawili. Hili ni tatizo ambalo linazikumba Halmashauri karibu zote nchini na wala siyo tu kwa Manispaa ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema mkakati wa Serikali ni kuendelea kuboresha huduma za afya hususan kupeleka watalaam wa afya hususan kupeleka watalaam wa afya katika vituo vya afya na zahanati.

Changamoto kubwa tunayoipata ni watumishi wengi hasa wanaotoka vyuoni kutopenda kufanyakazi huko Wilayani. Serikali itaendelea kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwataka vijana hao kuainisha Wilaya tatu ambazo wangependa kufanya kazi baada ya kukamilisha mafunzo yao ya vyuo.

Aidha, tunaendelea kuzihamasisha Halmashauri kuandaa mazingira mazuri ya kazi ikiwa ni pamoja na kuelekeza nguvu katika ujenzi wa nyumba za watumishi wao. Namshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na uongozi wa Halmashauri katika kubuni mazingira mazuri ambayo yatasaidia kuwafanya watumishi wavutiwe kufanyakazi kwenye Halmashauri hiyo na pia ashirikiane na watalaam wa Halmashauri hususan Mganga Mkuu wa Wilaya.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imeshakuwa mazoea kabisa wafanyakazi tunawasomesha hawataki kwenda kufanyakazi katika vituo vya kazi. Je, Serikali inaangalia tu hawa wafanyakazi/wanafunzi tunaowasomesha katika vyuo kwa gharama kubwa hawataki kwenda wanawatazama tu.

(a) Je, Serikali sasa itachukua hatua gani kali kwa kuwa kule vijijini kuna binadamu wanaishi ili waweze kwenda kufanyakazi?

(b) Kwa kuwa Serikali imeona kabisa sasa hivi na mikakati ya kuongeza vituo vya afya katika vijiji vyetu, haioni kuwa ifuate mfano wa Wizara ya Elimu kuchukua wanafunzi wa *form four* kwenda katika vyuo mbalimbali iwe kama vile nguvu kazi ili iweze kuokoa vijiji mbalimbali na hii hatua ambayo inakuja sasa hivi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Anna Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ilipokuwa ndiyo inayoajiri tu utaratibu tuliokuwa tunautumia ni kwamba kama mtumishi amepangwa kwenda mahali tunamchukulia hatua. Lakini katika mazingira ya soko huria kwamba wako watu wengi ambao wanaelekeza katika eneo hili. Utaratibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira ya kazi kule ambapo hawa watumishi wanatakiwa kwenda kufanyakazi. Ukisema kwamba unachukua hatua kama tulivyokuwa tunafanya kule nyuma matokeo utakayoyapata ni kwamba hawa wote watakimbia watakwenda kule kwenye *private sector* kwa maana ya sekta binafsi na Serikali itakuwa imebaki hivi hivi.

Rai ya Serikali ni kuomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote hapa tuhakikishe kwamba katika Halmashauri zetu tunaboresha mazingira ya kazi. Manispaa ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga inafanya vizuri sana kwa kweli Mkoa wa Rukwa una utaratibu mzuri sana wa kuhakikisha kwamba unawawekea mazingira mazuri watumishi wanaokwenda kule ili waone kwamba kunafaa kufanyakazi. Hizo ndiyo hatua ambazo tunafanya na sisi tumeshirikiana na Wizara ya Utumishi kuona kwamba mazingira ya kazi yanakuwa ni mazuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, amezungumzia swali la pili kwamba je, hatuoni kwamba kuna umuhimu wa kuchukua mfano unaofanana na ule wa Wizara ya Elimu. Nataka niseme kwamba hapa tunapozungumza habari ya afya tunazungumza habari ambayo ni nyeti kidogo ukilinganisha na suala la elimu kwamba tuchukue watu wanamaliza *form four* ni kweli nakumbuka kule nyuma tulikuwa tuna watu wanaitwa *rural medical elders* lakini wakati tunapotakiwa kuchukua mfano huo, lazima tuwe waangalifu tukijua kwamba tunachukua eneo ambalo linahusu maisha ya moja kwa moja na kwa hiyo wazo hili tunalichukua lakini tunalifanyia kazi katika utaratibu wa kuona kwamba tunakuwa waangalifu ili tusije tukaleta madhara zaidi. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema ni kwamba afya, waratibu watalaam inabidi kuwa na watalaam ambao wamebobe. Lakini Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa sasa hivi imefanya mpango wa kufupisha urefu wa kozi badala ya kufundisha miaka mitatu au minne, sasa hivi zile kozi tumezifanya vile *comprehensive* kwa hiyo minimum ni miaka miwili ambapo tunapata watalaam ka *RMS* au *Trained Nusses*. Kwa hiyo, hii itatusaidia kuweza kupata wafanyakazi wengi kuweza kwenda kupelekwa katika huduma za afya. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Naibu Waziri kwa majibu ya ziada.

Na. 123

Mji wa Lamadi Kupewa Hadhi ya Mji Mdogo

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Lamadi unakuwa kwa kasi sana; na kwa kuwa, tayari Serikali imekwisha anza kupima viwanja ili kuupanga uweze kuendelea na mahitaji halisi ya mipango miji ikiwa ni pamoja na huduma za jamii:-

(a) Je, ni lini Mji huo utakubaliwa rasmi kuwa ni Mji Mdogo wa Lamadi?

- (b) Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Mji huo mwezi Mei, 2007, alitoa ahadi ya kuharakisha kuwapatia maji wananchi hao. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu za Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Serikali haijawahi kuanzisha na kutangaza unaotajwa na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni Mji wa Lamadi; bali Ofisi yangu inatambua kukisajili Kijiji cha Lamadi chenye jumla ya vitongoji kumi na moja (11). Kijiji hiki cha Lamadi ni miongoni mwa Vijiji vitano (5) vya Kata ya Kalemela ambavyo ni Kijiji cha Lukungu, Chamugasa, Bushingwamhala na Mayega.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Magu kwa kubuni na kutekeleza Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi unaotenga maeneo ya makazi, huduma za kijamii na kiuchumi katika eneo la Kijiji hicho cha Lamadi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu inatambua jitihada zinazoendelea kufanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Magu ya kuandaa mazingira yanayowezesha kuanzishwa kisheria Mji Mdogo wa Lamadi na Mamlaka yake. Napenda kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Magu kuendeleza jitihada zake za kutekeleza vipaumbele vya mchakato unaoendelea sasa wa kuboresha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii na miundombinu iliyopo katika eneo hilo la Lamadi.

Pale ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Magu itakapokamilisha na kuwasilisha TAMISEMI pendekezo rasmi la kupandisha eneo hilo kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo, Ofisi yangu italichukulia hatua ipasavyo.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Dr. Chegeni kuwa katika mwaka wa Fedha wa 2008/2009, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilifuatilia juhudi zilizoanza kufanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Magu na Mkoa wa Mwanza kuhusu ufumbuzi wa tatizo la huduma ya maji ya bomba katika eneo la Vijiji vya Lamadi na Lukungu.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada ambazo imeshazianzisha juu ya hiki kijiji cha Lamadi ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri amekiita Kijiji cha Lamadi. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Lamadi ni kiungo muhimu sana na hasa kwa wakazi wa Mikoa ya Shinyanga, Mara na Mwanza na kwa kuwa Lamadi anachokiita ni kijiji kwa kweli hakifanani na Kijiji bali kinafanana na Mji. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuweka msukumo wa makusudi kabisa ili kuweza kupandisha Kijiji hiki cha Lamadi kuwa Mji Mdogo? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa jitihada za Serikali ni kusogeza utawala kwa wananchi na kwa kuwa Lamadi pamoja na Wilaya ya Magu na Mkoa wa Mwanza tumeshapeleka ombi rasmi la kuugawa Mkoa wa Mwanza na kuigawa Wilaya ya Magu ili kupata Wilaya ya Magu na Wilaya Busega. Je, ni lini Serikali itajitahidi kuharakisha mchakato huu ili wananchi wa Magu wafanane na wananchi wa Siha ambao wenyewe wana kata chache zaidi lakini wana Wilaya kuliko wananchi wa Wilaya ya Magu? (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu mawili ya Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kama anavyosema Dr. Chegeni eneo hili linaloitwa Lamadi ambalo ni kama Kijiji kwa maana ya ripoti tulizonazo na kumbukumbu tulizonazo ni eneo ambalo linaonekana kwamba linakwenda haraka sana katika mazingira ya kibiashara na kwa maana ya ukuaji wa mji.

Napenda kuchukua nafasi hii kwa kweli kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwamba anaonyesha jitihada za waziwazi za kuhakikisha kwamba Mji huu unabadilishwa sasa badala ya kuwa unamilikiwa kama kijiji unakuwa unamilikiwa sasa kama Mji Mdogo ambao una maana yake kubwa kwa maana ya kupeleka maendeleo zaidi kwa wananchi.

Kwa hiyo, kama nilivyosema katika jibu la Msingi hatuna tatizo kabisa na ku-*develop* eneo hili liwe Mji Mdogo kwa sababu utaratibu unasema tu kwamba jambo hili linaanza na Halmashauri na Halmashauri yenyewe inafikiri kwamba kuna haja ya kufanya hivyo sisi hatuna tatizo kama Serikali pindi watakapokuwa wamekamilisha mpango huo tutahakikisha kwamba wanafanya hivyo na tutahakikisha kwamba wanakuwa mdogo. Kwa hiyo, ni suala la kuwasiliana na sisi tu tuweze kufanya jambo hilo.

Swali la pili, linazungumzia habari ya kusogeza huduma zaidi kwa wananchi sasa hivi tunazungumza habari ya *D by D (decentralization by Devolution)* kwa maana ya kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi lakini wakati huo huo kwa maana ya kupeleka huduma zaidi kwa wananchi na *resources* na vitu vingine. Kwa hiyo, anachozungumza Mheshimiwa Dr. Chegeni hapa ni jambo la msingi pia kwa maana ya kwamba sisi hatuna *objection* yoyote.

Sasa kama mnavyokumbuka juzi tulijibu hapa tukasema kwamba tumeshindwa sasa kuendelea kutoa Wilaya nyingine kwa ajili ya wale wanaoomba kwa sababu ziko

Wilaya 11 ambazo zimeanzishwa na ambazo zinahitaji huduma mbalimbali na ambazo sasa hivi tunaanza kujenga Makao Makuu kwa ajili ya kujenga Halmashauri, Zahanati na huduma nyingine muhimu ambazo zinazungumzwa hapa. Amezungumzia pia kama vile ilivyo katika Wilaya ya Siha, Wilaya ya Siha ilikuwa na mazingira maalum ambayo yaliombewa ndiyo ikakubalika kwamba iwe Wilaya. Lakini nataka niseme hapa kwamba hatuna *objection* yoyote pale utakapofika na hali itakaporuhusu tutahakikisha kwamba Wilaya hiyo inapatikana pia. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa taarifa tu ya wote ni kwamba Wilaya ya Siha ilianzishwa kabla ya Mheshimiwa Mwanri kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sifa ambazo Kijiji hicho cha Lamadi kinazo zinafanana kabisa na sifa ambazo kijiji changu cha Mlowo kule Mbozi kinazo na kwa kweli kinakua kwa kasi kubwa sana. Kwa kuwa tayari Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi tulishaleta Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ombi la kuufanya Mji wa Mlowo uwe Mji Mdogo. Je, Waziri anatuambia nini sisi wananchi wa Wilaya ya Mbozi kuhusu Mji Mdogo wa Wilaya ya Mlowo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, habari hii ya Mji Mdogo wala haikuhitaji mimi kukaa katika nafasi hii niliyonayo sasa hivi kujibu kwa niaba ya Waziri Mkuu. Tulipokuwa tumekaa hapa mimi nimeketi hapa nakumbuka Mheshimiwa Pinda wakati akiwa Naibu Waziri na akiwa Waziri ambaye ni Waziri wetu Mkuu alisema kabisa hapa kwamba utaratibu wa kuanzisha Halmashauri ya Mji Mdogo unaanza na Halmashauri yenyewe inayohusika. Yaani hiyo ndiyo *the bottom line*. Pale wanakaa wanapanga wanasema sisi tunataka kuwa na Mji Mdogo wa Mlowo kama anavyozungumzwa na Mheshimiwa Zambi. Kwa hiyo, kama Mji huu utakuwa umeombewa na umekidhi vigezo vyote ambavyo tumevitamka hapa sisi hatutakuwa na tatizo lolote la kukubali kwamba uwe Mji Mdogo mradi tufuate utaratibu unaotakiwa. (*Makofi*)

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa makao ya Wilaya karibu yote au ni miji midogo au ni vijiji. Je, Serikali haioni kutoa ruksa kwa Makao Makuu ya Wilaya kuwa ni Halmashauri za Miji kuliko kuwa Halmashauri za Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selelii Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachosema mwenzetu Mheshimiwa Mbunge Selelii, ni kwamba ufike mahali useme kwamba maNdhari hapa ni Halmashauri na ni Makao

Makuu *automatically* sema kwamba hapo pote panakuwa Mji Mdogo kama namWelewa vizuri ndivyo anavyosema hapa.

Lakini ziko hoja sisi tumepokea katika Wizara za Halmashauri ambazo zimetakiwa zigeuke ziwe Mji Mdogo Halmashauri zenyewe zinakataa zinasema hapa pale usipafanye pawe Mji Mdogo. Lakini ukiangalia *logical* yenyewe ya suala la kuunda Halmashauri ya Mji Mdogo ni suala la kufuata utaratibu tu. Huwezi tu ukaubatiza Mji pale ukasema huu sasa kuanzia sasa ni Mji Mdogo kwa sababu unakidhi hivyo.

Sisi tunachosema ni kwamba kweli ukiangalia mazingira ya makao makuu yote ya Halmashauri yanafanana na Mamlaka ya Mji Mdogo.

Lakini ina *politics* na *economics* zake ambazo lazima ziwe *resolved* kule kule kwenye Halmashauri inayohusika ili sisi tunapofanya hapa wasitushangae waseme nyie mmetAka Mji Mdogo hili lilikuwa siyo hitaji letu sisi.

Kwa hiyo, kama kuna haja hiyo tutaomba tufuate utaratibu huo lakini hatuoni *problem* yoyote katika hilo, isipokuwa tunaona *problem* kutamka kwamba Halmashauri zote, Makao yake Makuu sasa yanaitwa Mji Mdogo ndiyo *problem* yenyewe. Lakini hakuna tatizo kama Halmashauri zenyewe zitakuwa zimetaka kufanya hivyo na zinakidhi haja hiyo. (*Makofi*)

Na. 124

Maafisa Kwenye Balizi za Tanzania

MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-

Kwa kuwa, jamii za Watanzania wanaoishi nje ya nchi zimeongezeka sana:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Maafisa Maalum wa kushughulikia jamii kwenye Balizi za Tanzania nje?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa nLaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba jamii ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi imeongezeka kutokana na kukua kwa mahusiano

yetu na nchi za nje kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kuna aina mbili za Watanzania waishio nje ya nchi kihalali: Kwanza, wale wanaokwenda kwa shughuli maalum kama vile mafunzo na kazi za mkataba. Pili, kuna wahamiaji ambao kwa sababu mbalimbali wameamua kuishi nje kihalali. Balozi zetu zina utaratibu maalum wa kuwaandikisha hao wote.

Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania anahamasishwa kwenda Ubalozini au kuuandikia Ubalozini ulio karibu naye na kutoa taarifa zake. Lengo la utaratibu huu ni kutuwezesha kujua wako wapi na kwa shughuli zipi. Na wanapoondoka kurejea nyumbani wanatakiwa kutoa taarifa ili Ubalozini uweze kuweka kumbukumbu zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waliohamia na kufanya makazi yao nje hushauriwa kuunda Jumuiya ya Watanzania na kushirikiana na Ubalozini katika masuala mbalimbali ya kijamii. Aidha, katika kila Ubalozini kuna Afisa Maalum ambaye mbali na kazi za kidiplomasia, hushughulikia masuala ya kijamii na kuna Afisa anayeshughulikia masuala ya wanafunzi Watanzania wanaosoma katika eneo husika. Wawakilishi wetu wa heshima pia hutoa huduma za kijamii kwa Watanzania wote wanaoishi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kufuatia ongezeko kubwa la idadi ya Watanzania katika baadhi ya nchi, Wizara yangu imechukua hatua ya kupeleka Maafisa Uhamiaji katika Balozi kama vile *London, Washington, Nairobi, Pretoria, Bujumbura* na Abu Dhabi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lipo kwa wale Watanzania ambao wameingia katika nchi hizo isivyo halali, kwa kuwa wahamiaji wa aina hii huwa hawapeleki taarifa zao Ubalozini hivyo inakuwa vigumu kupatiwa huduma za kijamii kupitia Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, natoa wito kwa Watanzania wote waishio nchi za nje ambao bado hawajajiandikisha Ubalozini wafanye hivyo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa.

Swali langu la msingi lilikuwa linahusu kuanzishwa kwa *Tanzanian Community Officers* kwa ajili ya kushughulikia hizo Jumuiya za Watanzania walioko nje.

Kwa maeneo ambayo Watanzania ni wengi sana kwa mfano Marekani kumekuwa na matatizo makubwa ya mahusiano kati ya Balozi na Watanzania na wameanzisha hizo Jumuiya na matatizo makubwa yanatokea pale ambapo wanapokuwa wamefariki. Kwa

mfano tatizo lililotokea Michigan mwaka jana ambapo vijana wawili wa Kitanzania waliuwawa na mpaka leo hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa dhidi ya watu ambao waliwaua Watanzania hao.

Kwa hiyo, nilikuwa napenda Waziri alifahamishe Bunge hili kwa yale ambayo maeneo Watanzania ni wengi sana, haoni kwamba kuna umuhimu huo wa kuanzisha maafisa maalum kwa ajili ya kuhusisha kusaidia hizo Jumuiya za Watanzania walioko nje? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zitto, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi katika nchi zote ambazo Watanzania wapo kwa Marekani, Uingereza, Nairobi Watanzania hao huhamasishwa na ubalozi kuanzisha Jumuiya zao. Jumuiya nyingi zimekwishaanzishwa. Leo ukienda London kuna Jumuiya, Ukienda Dubai kuna Jumuiya ya Watanzania na sehEmu nyingine mbalimbali.

Kwa hiyo nakubaliana naye kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha Jumuiya hizo na Balozi zinajitahidi kuhamasisha Watanzania waanzishe Jumuiya hizo ili waweze kusaidiana. Mfano Marekani Jumuiya ya Watanzania iko na inafanyakazi vizuri.

Hivi karibuni Mbunge mmoja alifiwa na ndugu yake ni Watanzania hawa walisaidiana kwa kutumia Jumuiya hii kuchangishana na kusafirisha maiti kuileta Tanzania. Kwa hiyo, ni kazi ya Balozi na Wizara yangu kuhamasisha Watanzania wanaoishi nchi za nje wafanye Jumuiya hizo kwa madhumuni ya kusaidiana. *(Makofi)*

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko kwa baadhi ya Watanzania wanaoishi nchi za nje kwamba baadhi ya Balozi haziwajali wanapokuwa na matatizo wanapofika kwenye ofisi za ubalozi. Hivyo wanaona hakuna sababu hata ya kwenda kujiandikisha kwenye balozi zetu na kwa kuwa kuna mfano kamili tulitembelea ubalozi wa Canada na maafisa walikiri kwamba hawajui idadi ya Watanzania wanaoishi Canada.

Je, sasa hivi Serikali inachukua jukumu gani la kuhakikisha kwamba balozi zetu zinawajali kikalifu Watanzania na hasa wakiwa na shida na waweze kuona kwamba hawa ni ndugu zetu japokuwa wapo nje? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: Kazi za Balozi ni kushughulikia Watanzania wanaoishi katika maeneo

yao kwa sababu Ubalozi kwa kidiplomasia inaitwa *extra territory* ya Tanzania katika nchi ile.

Kwa hiyo, ile pale ni nchi na kila Mtanzania aliyoko katika eneo lile ana haki ya kwenda pale kwenda kuelezea tatizo lako au shida yake yoyote, kama kuna ubalozi wowote hauwajali Watanzania, kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza Ubalozi huo unakwenda nje ya utaratibu wa kazi zake. (*Makofi*)

Tukielezewa Ubalozi, Wizara yangu itachukua hatua dhidi ya Afisa yoyote yule ambaye amekwenda nje ya utaratibu wake. Pale ni nyumbani kwa Watanzania na Mtanzania yoyote ana haki ya kwenda pale kusaidiwa, kama hakusaidiwa pale akasaidiwe wapi? Kwa hivyo kama kuna ushahidi tuko tayari, Wizara yangu iko tayari kuchukua hatua dhidi ya Ofisa yoyote yule aliyekwenda, aliweza kumdharau Mtanzania aliyekwenda pale kuelezea shida zake. (*Makofi*)

Na. 125

**Malipo ya Waliokuwa Wafanyakazi wa Mashamba ya
Chai na Mkonge – Korogwe**

MHE. ENG. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa, wakazi wengi wa Jimbo la Korogwe Vijijini walikuwa ni watumishi kwenye mashamba ya Chai na Mkonge yaliyokuwa yanamilikiwa na raia wa kigeni; na kwa kuwa, wengi wa watumishi hao walisimamishwa kazi mara tu baada ya mashamba hayo kumilikishwa kwa waendeshaji wengine na wengi hawajalipwa madai au mafao yao ya haki mpaka sasa:-

(a) Je, ni lini watu hao watalipwa malipo hayo?

(b) Kwa kuwa, thamani ya fedha kwa miaka ishirini iliyopita si sawa na thamani ya shilingi ya leo. Je, Serikali haioni umuhimu wa uhalali wa kulipa riba katika madai ya wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA
KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, napenda nitoe maelezo mafupi tu yafuatayo:-

Kwanza kuhusu mashamba ya Mkonge: Mashamba ya Mkonge yaliyoko katika Wilaya ya Korogwe ambayo yameuzwa bila kulipa mafao ya wafanyakazi ni yafuatayo:-

-Shamba la Kwashensi ambalo lilimilikiwa na CHAVDA liliuzwa kwa utaratibu wa ufilisi kwa Bwana Mathayo Mnkande mwaka 1998.

-Shamba la Hale-Mwakinyimbi ambalo lilimilikiwa na CHAVDA lilikabdihiwa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya upanuzi wa Mji wa Hale.

-Mashamba ya Gombezi, Magunga, Magoma, Hale na Mwelya yaliuzwa na PSRC kwa M/s *Katani Limited*. Wafanyakazi 92 waliokuwa watumishi katika mashamba hayo walitumia mafao yao kununua hisa katika kampuni hiyo. Aidha, mwekezaji amenyang'anywa mashamba na Serikali baada ya kuonekana kwamba ameshindwa kuyaendeleza ili yabinafishwe upya kwa utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, Mashamba ya Chai: Madai ya wafanyakazi yaliyopo ni yale ya kampuni binafsi ya iliyokuwa *George Williamson (T) Limited* katika shamba la *Ambangulu Tea Estates* kama malimbikizo ya mishahara ambayo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2005 yalifikia shilingi 233,389,005.25. Mwaka 2006, shamba hilo liliuzwa kwa kampuni ya *Mohamed Enterprises (T) Limited* likiwa tena chini ya mufilisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tunashauri wadai kutoka katika mashamba ya mkonge wawasilishe mchanganuo wa madai yao kwenye Taasisi ya *Consolidated Holding Corporation (CHC)* iliyochukua nafasi ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) ili Taasisi hiyo ione uhalali wa madai hayo na namna yanavyoweza kushughulikiwa.

Kuhusu mashamba ya Chai ya Ambangulu ambayo hivi sasa yamenunuliwa na *Mohamed Enterprises (T) Limited*; madai yako Mahakamani na uamuzi wa Mahakama unasubiriwa. Kwa taarifa tulizonazo Kampuni ya *Mohamed Enterprises (T) Limited* iliuziwa mali bila madeni yaliyokuwa yanajumuisha madai ya wafanyakazi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli thamani ya fedha ya miaka ishirini iliyopita si sawa na thamani ya shilingi ya leo. Pamoja na kutambua hivyo, Serikali kwa bahati haina utaratibu wa kulipa madai pamoja na riba.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri ya Naibu Waziri, ningepomba niulize swali moja la ziada. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba wako wanaodai na taarifa tulizonazo ni kwamba madai haya yalikuwa *PSRC* na sasa anatuambia madai hayo yapelekwe *CHC*. Je, haoni kama hii ni njia ya kuwakatisha wananchi, wadai wale tamaa kwa kuzungusha kwamba waanze tena upya kupeleka madai yao *CHC*? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA): Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia yoyote ya kuwazungusha wananchi.

Lengo la kuwaambia wapeleke katika Mamlaka hiyo nyingine niliyoitaja, ni kwa sababu hivi sasa *PSRC* haifanyi kazi hizo. Sasa Mamlaka hiyo niliyoitaja ndiyo imechukua nafasi hiyo badala ya *PSRC*. Kwa hiyo, kupitia kule ni kama kusaidia wananchi wale waweze kufufua madai yao upya na hatimaye waweze kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge na wakulima kwamba yako matatizo na liko tatizo la msingi ambayo mimi nimeliona katika mashamba haya Katani na hata yale ya chai ambayo mengine yako Rungwe na mengine yako katika Mkoa wa Tanga.

Tatizo kubwa la msingi katika mashamba haya ni kwamba kumekuwa na utaratibu wa kumilikishana mashamba. Mimi naita kama kiholela kwa sababu miliki ya shamba inaweza ikahamishwa moja kwa moja kutoka kwa mmiliki mmoja huyu pasipo kushirikisha watu wengine na wakulima wale ambao walikuwa wakishiriki katika mashamba hayo wao wanapelekwa tu kama upepo.

Kwa mfano, katika mashamba yale ya Ambangulu na Rungwe ya chai, Sir George Williamson ambaye ndiye alikuwa na mashamba haya, aliyamilikisha kwa Shamji ambaye alikuwa Uingereza na baadaye huyu Shamji akahamisha tena akayahamishia kwa *Mohamed Enterprises (T) Limited* na *Mohamed Enterprises (T) Limited* hakuchukua madeni yaliyokuwa yameachwa na makampuni yaliyopita.

Sasa mimi nafikiri pamoja na yote haya ipo haja ya kuhakikisha kwamba tunaangalia Sheria ya kilimo cha mkataba ili wakulima wetu hawa nao wawe katika mwanga na ikiwezekana wanasheria wa Serikali wasaidie wakulima kujua haki zao badala ya kuhamahama, umiliki unahamishwa, halafu wao wanabaki hewani.

Na. 126

Mradi wa Maji-Salama Mtwango na Kibao

MHE. BENITO W. MALANGALILA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kupeleka maji kwenye vijiji vya Samala, Mtwango na Kibao katika mwaka wa fedha 2007/2008 lakini mpaka sasa tunakaribia mwisho wa mwaka wa fedha maji hayajapelekwa katika vijiji hivyo:-

- (a) Je, ni kwa nini Serikali haijatekeleza mradi huo?
- (b) Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi huo ili isionekane inawadanganya wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vijiji vya Samala, Mtwango na Kibao ni miongoni mwa vijiji 10 vilivyochaguliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Programu hii inatekelezwa katika nchi nzima ikiwa na lengo la kuwapatia wananchi maji safi na salama.

Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi katika vijiji tajwa kumetokana na gharama kubwa inayohitajika kwa utekelezaji wa programu kwa ujumla, ambapo Serikali ilikuwa inatafuta fedha za utekelezaji kutoka kwa wafadhili mbalimbali. Jumla ya dola za Kimarekani 951 milioni zinahitajika kwa ajili ya kutekeleza programu ya maendeleo ya sekta ya maji kati ya sasa na mwaka 2010. Washirika wa Maendeleo wamekubali kuchangia dola za Kimarekani 700 na Serikali itatoa fedha sawa na dola za Kimarekani 251.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia ili kuharakisha utekelezaji wa mradi mzima ambao ni kweli umechukua muda mrefu. Hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kwamba kati ya Septemba 2008 na Machi 2009, wataalam washauri watakamilisha usanifu na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya makandarasi wa ujenzi. Kwa sababu hiyo, ni dhahiri kwamba utekelezaji halisi wa miradi hiyo utaanza si kabla ya mwaka 2009/2010.

Hata hivyo, Serikali katika bajeti ya 2009/2009 imetenga shilingi bilioni 62 ambazo tayari zimewekewa mihadi (*commitment*) na *World Bank* na Benki ya Dunia na kwamba ziko tayari kutumika. Fedha hizi zitasaidia kupunguza makali ya shida ya maji katika maeneo mengi pamoja na Mufindi wakati tunasubiri kuanza utekelezaji halisi wa mradi mkubwa wa vijiji 10 kwa kila Wilaya.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Asili ya swali hili ni kwamba kulikuwepo na vijiji vitano, vitatu na vingine Kisulu na Mpanga. Serikali ilisema kwamba vijiji hivi vitatu, Sawala, Mtwango na Kibao vitashughulikiwa na Wizara ya Maji. Sasa hivi inaonekana kwamba itashughulikia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Sasa mbona hii Serikali inawachanganya wananchi pamoja na mimi Mbunge wao?

Swali la pili, kama nilivyosema Kijiji cha Kitiru na Mpanga kilikuwa kishughulikiwe na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na tayari sisi Halmashauri tulishajipanga kushughulikia hivi viwili. Sasa kwa jibu hili ina maana kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inatakiwa ishughulikie vijiji vitano kiasi ambacho uwezo wetu haupo?

SPIKA: Linaonekana ni swali hilo hilo ila sehemu ya pili umeliremba zaidi lile la kwanza.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, vijiji vya Mtwango na Kibao wakati wa maandalizi havikuwekwa hata kwenye utaratibu wa *Qwick Wings* kwa sababu tayari vilikuwa vimekwishachaguliwa kuwekwa moja kwa moja katika vijiji 10 na bado utaratibu wetu ni huo huo hatujasema kwamba sasa baadhi ya miradi tumesema Halmashauri tumeikabidhi sasa kila kitu.

Sisi tumejitoa, la hashu. Tunachosema ni kwamba tunatafuta fedha ili hatimaye vijiji vyote hivyo vitekelezwe na fedha kupitia na programu ya kuendeleza sekta ya maji. Na ndiyo maana hata hivi sasa tunavyozungumza tayari tumekwishanza. Najua Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiniuliza lakini baada ya muda mfupi mkisoma na kwenye magazeti mtaona, tumetoa na matangazo kwamba Halmashauri nyingi tumezipatia fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi yenu hii pamoja na hiyo anayoitaka katika eneo lake Mheshimiwa Malangalila. Tumetumia fedha nyingi kwa kipindi hiki, tumezipa Halmashauri za Miji, Halmashauri za Wilaya 132, jumla ya bilioni 12 takriban.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri naomba Mheshimiwa Malangalila asiwe na wasi wasi kwa sababu Halmashauri zote tumeziwekea huu utaratibu. Pale ambapo miradi inasubiri programu ya kuendeleza sekta ya maji, basi watakuwa na subira lakini ndiyo maana tumeweka fedha kidogo kwa ajili ya kuendelea na kazi hii wakati tunasubiri fedha zile nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia niseme Halmashauri 8 za Njombe, Makete, Kibaha, Kibaha Town, Arusha, Ngorongoro, Ilala, Kinondoni, tumeshindwa kuzitumia fedha wiki iliyopita, kwa sababu wao mpaka leo hii wameshindwa kufungua akaunti za *Water Sector Development Programme*. (Makofi)

SPIKA: Maswali mafupi sana sana ya nyongeza kwa sababu sekta ya maji ni muhimu. Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Job Ndugai.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Kwa kuwa Serikal imefanya kazi nzuri sana kupeleka maji Mkoani Singida kupitia miradi ya Benki ya Dunia na kwa kuwa miradi hiyo karibu yote iliyofungwa Singida zimefungwa pampu ndogo zenye *piston* moja ambazo zinashindwa kusukuma maji kwenda kwenye tenki.

Je, Serikali inafahamu tatizo hilo na kama inafahamu ina taratibu gani, kwa sababu wananchi sasa hivi wanalalamika kwamba miradi hiyo haitoi maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, yanapotokea matatizo ya utendaji katika Halmashauri husika au Halmashauri ya Mji, basi ni vema Halmashauri husika yenyewe ituarifu na si lazima kuja kupitia Bungeni,

mtuarifu kwamba hapa maji hayatoki, pale ambapo tumeona, tumepata taarifa na nimetembea mimi mwenyewe kwa mfano, tumechukua hatua na mahali pengine tumegundua kwamba kweli kulikuwa na matatizo ya kiufundi na tumechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani watu ambao hawakuweza kufuata taratibu.

SPIKA: Swali la mwisho fupi la nyongeza. Mheshimiwa Ndugai.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika kunipa fursa hii niulize swali moja fupi la nyongeza pamoja na shukrani kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri anayotoa.

Nilipenda tu kuuliza kuhusiana na eneo la Kibaigwa ambao ni mji mdogo na soko kuu la kimataifa pale pana matatizo makubwa sana ya maji, ulikuwepo mpango kwa ajili ya kusaidia miji midogo Gairo, Kibaigwa na Mpwapwa kupitia usaidizi wa Serikali ya Ufaransa. Jambo hili limekuwa haliongelewi kabisa hapa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu huo wa miji midogo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, napenda nikiri kwamba kulikuwa na utaratibu huo na utaratibu huo huo haujafa.

Labda tu nimshauri au nimwahidi Mheshimiwa Ndugai kwamba tutajitahidi kuangalia tufufue kwa sababu tayari fedha zilikwishatengwa na Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya mradi huo sasa kama kuna kulegea legea katika utekelezaji basi mimi naomba nimwahidi kwamba nitafuatilia hata katika kipindi hiki nikiwa hapa tuhakikishe kwamba tunafufua juhudi hizo zilizokwishaanzwa.

Na. 127

Usalama wa Maji yanayotumika Geita

MHE. ERNEST G. MABINA aliuliza:-

Je, maji yanayotumika kwa matumizi ya wananchi wa Geita yana usalama kiasi gani kwa afya ya wakaaji wa sehemu hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, nitoe tena maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mji wa Geita wenye wakazi wapatao takriban 50,000 unapata huduma ya maji safi na salama kutoka kwenye visima vilivyochimbwa maeneo wa mji. Hata hivyo visima vilivyopo havikidhi mahitaji halisi ya mji. Aidha, kuna chanzo cha

maji ya chemchem kutoka mlima wa Kagera ambayo yanahudumia wakazi wa mji wa Geita wapatao 4,000.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha huduma ya maji kwa mji wa Geita, Serikali ina mpango wa kupata chanzo cha maji ya kutosha mahitaji ya mji mzima, ya sasa na baadaye. Mchakato wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria umbali wa kilometa 50 kutoka Senga Mchangani hadi Geita Mjini umeanza na mpaka sasa upembuzi yakinifu, upimaji na usanifu wa awali umekamilika. Usanifu wa kina unatarajiwa kufanyika mwaka wa fedha 2008/2009 chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji yaani *Water Sector Development Program (WSDP)* na taratibu za kumpata mhandisi mshauri zinaendelea.

Aidha, Wizara yangu kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imetenga shilingi 368,000,000/= ambazo zitatumika kukarabati miradi ya maji katika Halmashauri ya Geita kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji wakati mchakato wa ufadhili wa Benki ya Dunia unaendelea.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vyote vya maji hupimwa kwa kuzingatia viwango vya kitaifa vya ubora wa maji ya kunywa nchini kabla ya wananchi kuanza kutumia chanzo husika.

Upimaji wa ubora wa maji umedhihirisha kwamba chanzo cha maji cha Bwawa la Nyamalembo kilichopo Geita kimechafuliwa na madini za zebaki *mercury* yanayotumika kwa ajili ya kuoshea dhahabu katika eneo la Nyankumbo hivyo chanzo hiki hakifai kwa matumizi ya binadamu hata kwa wanyama.

Mheshimiwa Spika, madini aina tofauti tofauti yana madhara tofauti kwa binadamu yanapozidi viwango vinavyokubalika kwa mfano, madini ya zebaki au *mercury* yakizidi kiwango cha 0.001 miligramu kwa lita yanaweza kusababisha saratani, yanaharibu chembechembe za mwili, yanasababisha kutokuona na kupunguza uwezo wa kufikiri na hatimaye hata kifo. Natoa rai kwa wananchi katika maeneo yanayoyachimbwa madini ya dhahabu waache kabisa mtindo wa kusafisha dhahabu katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, maji yanayotumiwa na wananchi wa Geita kutoka kwenye visima na chemchem yana usalama kwa sababu yamepimwa na yapo katika viwango vilivyowekwa kitaifa. Aidha, Serikali ina utaratibu wa kukagua na kupima maji mara kwa mara na kuhakiki ubora wake ili kuchukua hatua zinazofaa uchafuzi unapogundulika ikiwa ni pamoja na kuacha vyanzo hivyo au kuyatibu maji hayo.

MHE. ERNEST G. MABINA: Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa huu mpango wa kuleta maji Geita ulianza muda mrefu ambao ulikuwa chini ya *MCC* na *MCC* wakasema kwamba hataweza kuleta maji kutokana na miradi ambayo walikuwa wanafadhili. Sasa hivi wamesema kwamba kuna huu mpango wa *WSDP* ambao wataleta maji kutoka Asenga mpaka Geita. Upembuzi yakinifu ilikuwa imekadiriwa bilioni 18.5 na sasa hivi wamekinzana na majibu ya swali langu lililopita katika kipindi cha Bunge lilipita walisema kwamba maji Geita watalewa kutoka

SPIKA: Mheshimiwa nenda kwenye swali sasa.

MHE. ERNEST G. MABINA: Kutokana na watu wa GGM, je Serikali inasemaje mradi wa Asenga wataufadhili kweli wakati pesa walizotenga hapa ni kidogo? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Naona swali limepanuka zaidi kutoka kwenye usalama wa maji ya Geita mpaka mradi huo mwingine.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, mradi ule nao umo katika programu yetu mzima hii. Tukisema programu ya kuendeleza sekta ya maji kwa jumla, tunazungumzia Tanzania nzima. Kwa hiyo, hatuna miradi ambayo tutaibagua tuseme huu hatutautekeleza na ule hatutautekeleza. Ndiyo maana tumeweka utaratibu kwamba wakati tunangoja ile programu iive basi tumeweka huu utaratibu wa kuweka fedha kwa ajili ya kuandaa miradi hii iwe inatoa huduma kwa wananchi.

Ni jukumu la Halmashauri husika kuweka kipaumbele kwenye mradi ule, sisi tukipeleka pesa mara nyingi tunapeleka katika Halmashauri, ili wao ndiyo waweke kipaumbele. Nimesema kwamba katika mwaka ujao tumetenga bilioni 62 zianze kutumika wakati tunangoja programu hiyo iive. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba awe na subira kidogo.

Na. 128

Ajali za Usafiri majini

MHE. MGENI JADI KADIKA aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi hasa wa Visiwani mfano, Tanga, Pemba, Unguja, Mafia, Ukerewe na kadhalika, hudumia usafiri wa majini kwa kutumia boti, mashua, jahazi na kadhalika na kwa kuwa wengi wao hupata ajali kwa chombo kuzama au kupasuka kutokana na dhoruba kali:-

Je, kwa mwaka 2006-2008 ni ajali ngapi zilitokea na wananchi wangapi walipoteza maisha na wangapi waliokolewa?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme kuwa si kweli kwamba wengi wa wananchi wanaosafiri majini kwa kutumia boti, mashua, majahazi na kadhalika hupata ajali. Takwimu za ajali zilizotokea majini kati ya mwaka 2006 na 2008 kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge, ni kama ifuatavyo:-

Katika mwaka 2006, ajali 5 zilizotokea majini katika Visiwa vya Magege, Kerebe, Ihela, Bogorola Ukerewe na Muleba. Katika ajali hizo jumla ya watu 57 walipoteza maisha na watu 54 waliweza kuokolewa. Katika mwaka 2007, ajali 11 zilitokea majini katika maeneo ya Kilwa Masoko, Dar es Salaam, Ukerewe, Mabibi-Ukerewe, Tanga, Nkungu-Chunya katika Ziwa la Rukwa. Mwanza, Kisiju, Kisiju-Kilindoni na Kinesi. Katika ajali hizo jumla ya watu 30 walipoteza maisha na 149 waliokolewa.

Katika mwaka huu wa 2008, ajali 5 zimetokea majini katika maeneo ya Dar es Salaam, Nyamukazi Bukoba, Ziwa Tanganyika, Pemba na Pangani. Katika ajali hizo jumla ya watu 62 walipoteza maisha na 17 waliokolewa. Takwimu hizo ni za ajali ambazo taarifa zake rasmi zilipokelewa kwenye mamlaka husika. (*Makofi*)

MHE. MGENI JADI KADIKA: Ahsante, nashukuru Mheshimiwa Spika kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tarehe 10 Juni, 2008 boti iliyotoka Tanga kuelekea Pemba ilizama na Watanzania wasiopungua 20 walipoteza maisha na hakuna maiti iliyookolewa. Je, Serikali ilichukua hatua gani?

Swali langu la pili. Je, Serikali inaonaje sasa kuwakopesha makoti ya kuokolea maisha wamiliki wa vyombo hivyo ili kukabiliana na maafa yanapotokea?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, katika hiyo ajali ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja ya kupoteza maisha idadi ya watu 20 hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua kusema kweli kwanza itakuwa ni lazima kuhangaikia kuwaokoa na bahati mbaya inapotokea kwamba haijafanikiwa, wamepoteza maisha inayofuata sasa ni kuweka tahadhari kwa siku za baadaye ambazo kwa sasa hivi tunachozingatia ni kutoa elimu kwa wenye vyombo wote kuhakikisha kwamba vinakuwa katika hali ya usalama na hasa wawe wanazingatia utabiri wa hali ya hewa wanaopewa na Mamlaka husika ili ajali hizi zisiendeele kutokea. Ikitokea iwe ni bahati mbaya tu.

Lakini Mheshimiwa Spika, katika swali la pili la kuomba hawa wenye vyombo kukopeshwa makoti na vitu vingine vya kuokolea. Hii ni hatua moja tu. Lakini niseme tu kwamba katika vyombo hivi hawa wenye vyombo vya majini wanatakiwa waweke tahadhari zote si lazima wakopeshwe na Serikali lakini kwa upande wa Serikali hatua zinazochukuliwa ni kama nilivyosema hii ya kuweka tahadhari ya kutoa utabiri wa hali ya hewa.

Lakini vile vile kwa sasa hivi vyombo vyetu hivi vya usafiri vimeongezewa minara ya kutoa ushauri. Kwa hiyo, kwa hatua hii nadhani kwamba wananchi wanaweza kuwa wana tahadhari za usalama unaotakiwa kusafiri majini. (*Makofi*)

Kuharakisha Utoaji wa Vitambulisho vya Uraia Tanzania

MHE. SALIM HEMED KHAMIS aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Tanzania inapokea wageni kwa njia mbalimbali:-

Je, kwa nini Serikali haiharakishi mchakato wa kuanzisha vitambulisho vya uraia ili iwe rahisi kutambua nani ni Mtanzania na nani si Mtanzania?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, adhema ya Serikali ni kuwa imeanza kutoa vitambulisho vya Taifa kwa Raia na wageni ifikapo mwishoni mwa mwaka 2009, baada ya matayarisho muhimu kukamilika. Tayari jengo kwa ajili ya Ofisi anzilishi ya vitambulisho limenunuliwa na kufanyiwa marekebisho muhimu na tayari limewekwa samani na vitendea kazi muhimu.

Aidha, Mratibu wa Mradi wa vitambulisho amekwishateuliwa ili kusimamia uanzishwaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Mei, 2008 Serikali ilitangaza awamu ya kwanza ya zabuni ya Vitambulisho vya Taifa yaani *Prequalification stage* na zabuni zimefunguliwa tarehe 25 Juni, 2008. Hivi sasa mchakato wa kuchuja zabuni unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu na unyeti wa suala hili Serikali inalifanya zoezi hili kwa umakini mkubwa.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Zanzibar ina uzoefu na teknolojia bora kabisa miongoni mwa teknolojia za utengenezaji wa vitambulisho vya uraiya duniani. Na kwa kuwa, Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara ni nchi moja. Je, kwanini Serikali ya Muungano wa Tanzania haikuzungumza na Ndugu zao wa Zanzibar kuhamisha teknolojia hii kuja hapa bara ili kupunguza gharama na ili kukwepa aina yoyote ya ufisadi ambayo inaweza kutokea katika utaratibu huu uliopangwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, utaalamu wa kutengeneza vitambulisho unahitaji umeme. Na kwa kuwa, umeme vijijini ni chini ya asilimia moja

ya vijiji vyetu vya Tanzania ndiyo vyenye umeme. Je, Serikali itatumia mkakati gani kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanaoishi vijijini wanapata vitambulisho?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa, anasema kwamba Zanzibar inao uzoefu na hilo kweli Serikali inalifahamu. Lakini ningependa kusema kwamba mazungumzo yalikuwepo na katika Bodi ambayo inahusisha utaratibu huu, wawakilishi wa Zanzibar wamo na hili suala hawakulizungumzia kusema kwamba kama alivyolieza Mheshimiwa Mbunge hapa.

Kwa hiyo, ninaweza nikalijibu kwa misingi hiyo kwamba Zanzibar imo katika bodi hiyo ambayo inashughulikia masuala ya vitambulisho na wao wa upande wa Zanzibar hawakulizungumza hilo suala. Kwa hiyo, mimi ninachukulia kwamba wao wanaamini kabisa kwamba ilikuwepo haja ya kuchukua njia tofauti kwa sababu halikuzungumzwa kama alivyolizungumzia. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, pili naomba niseme tu kwamba ni kweli kumekuwa na masuala ya ufisadi, lakini ninadhani itakuwa ni dhana ya hatari kwamba kila kitu ambacho Serikali inajaribu kukifanya kinatizamwa katika misingi ya kusema kwamba ndani yake kuna ufisadi. Nafikiri tutafika pahala itakuwa ni vigumu Serikali kufanya majukumu yake kwa kuogopa kivuli cha kusema kwamba kila tutakalolifanya dhana ya ufisadi inakuwepo. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kujibu Swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, Salim Hemed Khamis. Kwa kusema kwamba hili suala la kupata vitambulisho vya utaifa sio uraiya, vya utaifa wa Tanzania halina uhusiano na umeme vijijini kwasababu vitambulisho hivi havitatengenezwa vijijini.

Vitambulisho hivi vitatoka pahala ambapo vitatengenezwa ambapo umeme upo kama vitu vingine vinavyotengenezwa lakini watu watakuwa na haki za kupata. Kama vile *passport* za Tanzania sio kwamba zinatengenezwa kila mahali katika Mkoa au katika Wilaya za Tanzania. Lakini watu wa vijijini wanapata hizo *passport*. Kwa hiyo nadhani hata vitambulisho vitakuwa katika misingi hiyo. (*Makofi*)

Na. 130

Gesi Asilia Kutumika Tanzania

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania imekwisha gundua hazina kubwa ya gesi asilia na kwamba utafiti zaidi bado unaendelea:-

Je, ni lini gesi hiyo asilia itaanza kutumika kama nishati mbadala kwaajili ya kuendeshea magari badala ya dizeli na petroli ili kupunguza matumizi makubwa ya fedha za kigeni?

Je, ni lini gesi hiyo itaanza kusambazwa kwa matumizi ya majumbani ili kupunguza uharibifu wa mazingira kwa ajili ya kukata kuni na kuchoma mkaa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli gesi asilia imegunduliwa Songo Songo, *Mnazi Bay* na Mkuranga na utafiti zaidi wa mafuta na gesi unaendelea katika maeneo yenye miamba inayofahamika kijiolojia kuambatana na mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (*TPDC*), lipo katika jitihada za kuanzisha na kuendeleza mradi wa matumizi ya gesi asilia katika Jiji la Dar-es-Salaam, kama nishati mbadala kwa magari na matumizi ya majumbani pamoja na taasisi. *TPDC* kwa kushirikiana na kampuni ya *Ultimate Petroleum Technology Limited* ya China mwezi Julai, 2007 walikamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa matumizi ya gesi asilia Jijini Dar-es-Salaam, kama nishati mbadala. Mpango wa biashara wa matumizi ya gesi hiyo asilia ulikamilika mwezi Oktoba, 2007. Kutokana na utafiti huo, mradi utatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itakuwa ya mradi hamasishi, *pilot project*, ukihusisha matumizi ya gesi kwenye magari kama 200 hivi, taasisi na nyumba kama 70 eneo la Mikocheni. Watekelezaji wa mradi ni *TPDC* na *Pan African Energy* na utagharimu dola za Marekani milioni tatu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya mradi itafuatia baada ya tathmini ya mafanikio ya mradi hamasishi na gharama za mradi awamu ya pili zinakisiwa kuwa ni Dola milioni 32. awamu hiyo itajumuisha kutandika mabomba ya kusafirishia gesi, kuweka mitandao ya kupeleka gesi majumbani na kubadilisha magari kama 8,000 hivi ili yatumie gesi. Juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo zinafanyika. Tayari *TPDC* imewasiliana na wawakilishi wa Serikali ya China na Korea hapa nchini, ambao wameonyesha nia ya kushirikiana katika mradi huo.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze mdogo wangu, Naibu Waziri wa Nishati, Mchumi Mheshimiwa Adam Malima, kwa

majibu mazuri. Ningependa sasa niombe anipatie majibu kwa maswali mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya mradi hamasishi ina ashiria kana kwamba matumizi ya gesi katika kuendeshea magari pamoja na nyumbani ni jambo jipya. Ukweli ni kwamba matumizi ya gesi kwa kuendeshea magari na majumbani katika ulimwengu ni jambo la kawaida sana. Kwa hiyo, nashangaa kwanini jibu lake linaonyesha kana kwamba sisi Tanzania tunataka kugundua gurudumu katika eneo hili. Swali, ameeleza kwamba Wizara inatayarisha mpango kamambe na baadaye utaletwa katika Bunge hili ili tuupitishie. Ningependa kufahamu kwa uhakika kabisa na kwa maana hiyo ninahitaji Serikali itoe *commitment* ni lini mpango huu kamambe tukizingatia dharura ya upandaji wa bei za mafuta katika soko la dunia. Utaletwa katika Bunge hili ili tuupitishie? (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, katika jibu lake anasema *TPDC* itashirikiana na *Pan African Enterprises* kuifanya kazi hii. Hii *Pan African Energy* ni kampuni ya nje, suala linalotakiwa kufanywa hapa...

SPIKA: Malizia swali, sio ushauri.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, suala linalotakiwa kufanywa hapa ni kusambaza gesi. Hivi tunahitaji kampuni ya nje kuja kuisaidia *TPDC* kuja kusambaza gesi hapa nchini? Kwanini isifanyiwe na *TPDC* yenyewe?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Kaka yangu Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya mradi hamasishi siyo kwa sababu Tanzania tumegundua jambo jipya, hapana, isipokuwa katika miradi hii ya kutumia gesi asilia kwa matumizi haya ya majumbani tumegundua kwamba kote ambako tumejaribu kufanya utafiti ile *transformation* imekuwa ngumu kidogo kwa sababu ya mazowea ya matumizi ya nishati yaliyokuwepo hapo awali.

Tunachofanya ni kwamba tumetenga magari kama 200, nyumba kama 70, kwa awamu ya kwanza kwa Jiji la Dar-es-Salaam, ambalo ndilo linatumia nishati kwa wingi zaidi kuliko mkoa mwingine wowote Tanzania. Na baada ya mafanikio ya ile *transformation* itatuongoza kujua sasa uwekezaji ule tunauweka katika mfumo gani. Na tumesema kwamba awamu ya pili ambayo kusema kweli ni awamu kubwa na kaka yangu Mheshimiwa Siraju, anajua gharama ya milioni 32 kwa hali ya sasahivi ya uchumi wetu ni gharama kubwa.

Lakini bado tunakisia kwamba awamu hiyo ya pili italenga magari 8,000 italenga mataasisi makubwa. Lakini pia itajumuisha kupeleka mtandao wa matumizi ya gesi maeneo ya Dar-es-Salaam ili wale watumiaji wa nyumbani waweze kuyafikia kwasababu *issue* siyo kuwapelekea tu gesi, *issue* ni kuwapelekea gesi hiyo iwe na unafuu zaidi

kuliko mkaa na matumizi mengine waliyokuwanayo sasa hivi. Kwa hiyo kusema kweli si jambo jipya lakini tunataka tulifanye ili pia liwe na mafanikio ya moja kwa moja na lisiwe kama jambo ambalo tunajaribu jaribu. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama hizi za *US \$ 32,000,000* kwa awamu ya pili. Awamu ya kwanza ni dola milioni 3, kwahiyo jumla jambo lote kwa Dar-es-Salaam, tu litagharimu kama dola milioni 35 na zaidi kidogo kwasababu Dar-es-Salaam tuna nyumba zaidi ya hizo elfu 30 tulizotaja. Lakini nadhani tukubaliane kwamba tukipata mwekezaji wa sekta binafsi na kwasababu hili jambo linataka liendeshwe kibiashara *TPDC* kutia mkono mule ndani ni jambo zuri kwasababu tunatarajia kwamba na wao watakuwa wamelitumia hilo kama namna ya kuboresha uwekezaji na kuboresha mapato yao.

Lakini kwa kiwango hiki nadhani *TPDC* peke yao hawana uwezo wa kuhimili uwekezaji wa milioni 35 mpaka 40 dola. Kwa hiyo nadhani ni vizuri na yeye atanikubalia kwamba hili jambo *TPDC* watafute ushirikiano na makampuni makubwa isipokuwa tu kwamba serikali tutaingilia kati kujua kwamba mikataba ile na makubaliano yale yana maslahi kwa wananchi wa Tanzania. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, mwisho ameniomba nizungumzie sera. (*Makofi*).

SPIKA: Aah, ameelewa kabisa kama tulivyoelewa sisi.

Na. 131

Sheria Za Elimu Nchini

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE K.n.y. LUHAGA J. MPINA aliuliza:-

Kwa kuwa, utoaji wa elimu bora unategemea mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia pamoja na sheria zinazoendana na wakati:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipitia upya sheria za elimu na kuzifanyia marekebisho?

(b)Je, taarifa za Wakaguzi wa Elimu ya Msingi huripotiwa wapi na hushughulikiwaje?

(c)Je, serikali itakubaliana nami kuwa, sheria inayomzuia kijana aliyehitimu darasa la saba kukariri imepitwa na wakati?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imeanza mchakato wa kupitia upya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995.

Mchakato huo umeanza kwa kupata maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Taasisi za Dini, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, *NGO's*, Mashirika ya Kimataifa, Walimu, Bodi za Shule, Kamati na wananchi. Baada ya kukamilisha hatua hiyo Wizara itaendelea na hatua zinazofuata katika kurekebisha sera ya elimu na mafunzo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebisha na Sheria Namba 10 ya mwaka 1995 inamtaka Mkaguzi wa shule kila anapokagua shule kuandika taarifa na kuituma kwa Kamishna wa Elimu, mwenye shule na wadau wengine wa elimu.

Kwa shule za msingi za Serikali, wenye shule ni Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji, Manispaa, Jiji na Wilaya. Nakala za taarifa hizo hupelekwa kwa Mwalimu Mkuu, Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, Mratibu Elimu Kata na Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Kanda.

Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi za mazoezi zilizo kwenye Vyuo vya Ualimu na Shule ya msingi ya Arusha ziko chini ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, hivyo taarifa ya Ukaguzi inapelekwa kwa Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Ukaguzi wa shule hushughulikiwa kwa kuendeleza mazuri yaliyojitokeza na kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imeanza kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, tunakaribisha maoni ya ziada ya kila Mheshimiwa Mbunge.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nilitaka kujua tu kwamba kwa kuwa, katika mfumo na sera ya Tanzania ya Elimu haitambui Elimu ya Watoto Wadogo wenye umri wa miaka kuanzia mitatu hadi mitano. Je, kwa kuwa sasa viko vyuo vya binafsi kama kile cha Mtumba, Mkoani Dodoma hapa hapa Dodoma, ambacho ni cha Ustawi wa Jamii, lakini kinafundisha Walimu wa Chekechea, Serikali haitambui. Je, Serikali inasema nini katika eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa ibara ya 11 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inazungumzia juu ya haki ya kila mtu kupata elimu kwa kadri ya upeo wa akili yake. Na wapo watoto ambao wanamaliza darasa la saba na wanakuwa wanapenda kuendelea lakini wamefeli. Sera yetu inakataza kukariri. Je, Serikali haioni kwamba jambo hilo limepitwa na wakati? Ni vizuri wakaruhusu ili kila mtu apate haki hii ya msingi kwa mujibu wa Katiba?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Simbachawene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la watoto kuanzia miaka mitatu hadi mitano haliko katika mfumo rasmi wa elimu chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Watoto wa umri huu hulelewa katika vituo vya kulelea watoto na hivi viko chini ya Wizara tofauti, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inaanzia miaka mitano, sita, kwa shule za awali ambazo ndio ziko katika mfumo rasmi wa elimu yetu ya Tanzania na hizi ziko chini ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kama nilivyosema hatukuwa na *system* ya kukariri darasa la saba kutokana na sheria ya elimu Namba 25 ya mwaka 1978 ambayo pia ilirekebisha mwaka 1995 na mwaka 1998. Na nimesema ni kutokana na kwamba darasa la saba lilikuwa ndiyo *terminal* katika *system* yetu. Huwezi ukakaririsha mtoto ambaye amefikia kikomo cha elimu inayotakiwa ambayo ni *Compulsory Education*, lakini tunarekebisha sheria hii.

Kwahiyo, nimesema katika mchakato huo ambao umeanza tunaomba maoni ya wadau wengi akiwemo Mheshimiwa Simbachawene, kama kuna haja ya kukaririsha watoto wa darasa la saba basi tunaomba hayo maoni ili tuweze kuyaingiza na sheria nafikiri ita *accommodate* maoni yote ya wadau. (*Makofi*).

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha sasa ni matangazo. Nitaanza na wageni na wageni wafahamu kwamba ninapowatamka basi wasimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua.

Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa William Ngeleja, anao wageni wake wafuatao. Kwanza ni Mheshimiwa Ken Konga, Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Maji, Zambia. *From the Republic of Zambia, the Minister for Energy, welcome Sir. We are very happy to welcome our neighbours brothers and sisters from Zambia. Zambia and Tanzania of course have had a fantastic relationship. We are joined by so many things including the neighbourhood at Tunduma. So we are happy to see you here.* Amefuatana na Katibu Mkuu, Ndugu Peter Mumba, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. *Permanent Secretary, welcome welcome.* (*Makofi*)

Wapo pia Mhandisi Muzelenga, Mkurugenzi Muendesaji wa *TAZAMA pipe lines*, yule pale, karibu. Mhandisi M. Kikula, Mkurugenzi wa Uendesaji Uhandisi *TAZAMA*, yule pale. Bi. Mjengwa, Katibu wa kampuni, *Company Secretary* kutoka Ndola – Zambia, yule pale, naona wenzetu wanazingatia jinsia kiasi fulani.

Vile vile ni Ndugu A. Saunyama, Meneja wa *TAZAMA pipe line* upande wa Tanzania na wajumbe wawili wa Bodi ya Wakurugenzi wa *TAZAMA* kutoka Tanzania, Ndugu Khalfan na Ndugu Zuberi, wote wale pale, karibuni sana (*Makofi*)

Naomba tutambue kuwepo kwa Ndugu Edward Hosea, Mkurugenzi Mkuu wa *TAKUKURU* akiwa ameambatana na Kamanda wa Mkoa wa *TAKUKURU* na Maofisa wengine wanne, wako wapi sijui? Waheshimiwa Wabunge, pale katika jukwaa la Spika pale, kuna wageni muhimu sana kwangu. Ni walimu na Bodi ya Shule ya Msingi ya Urambo Kati, shule hii ndio Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta, alikosoma kuanzia mwaka 1950 hadi 1953. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ujumbe unaongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule, Bwana Peter Sitta. mnacheka. Lazima kujijenga unadhani mambo haya ovyo ovyo haya na Mjumbe mwingine rafiki yangu Nssoro. Bwana Nassoro naomba usimame, Mwalimu Mkuu, naomba asimame, yule mama pale. Pia naomba na wengine wote muweze kusimama. Karibuni sana, karibuni sana, tutaonana baadaye hapo kwenye saa sita mchana hivi. (*Makofi/Kicheko*).

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Galinoma na Mheshimiwa Mng'ong'o na Mheshimiwa Pindi Chana. Ni waheshimiwa Madiwani 27 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, naomba wasimame, wale pale. Karibuni sana kutoka Iringa, ni mmoja wa mikoa ninayoipenda sana, mlinifundisha kazi mwaka 1987, nilipokuwa Mkuu wenu wa Mkoa, ahsante sana. Wapo wageni wa Mheshimiwa John Paulo Lwanji, ambao ni Sechele Lwanji na Diana Lwanji, nadhani ni wanae anasema wanasoma. Sechele na Diana? Kwa heshima pia naomba tutambue uwepo wa washiriki 80 wa maonyesho ya asasi za kiraiya, *AZAKI*. Wale viongozi wa *AZAKI* naomba msimame, asasi za kiraiya. Na nichukue nafasi wakati huo huo kwanza kuwashukuru kwa kuja tena mara hii na pia kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge, kwamba asasi za kiraiya kutoka Mikoa yote ya nchi yetu, Bara na Visiwani, wameweka maonyesho pale kwenye eneo letu la maonyesho.

Mnaombwa sana sana kuwepo pale, ufunguzi rasmi utafanyika leo asubuhi. Lakini maonyesho yataendelea leo, kesho na keshokutwa na kadhalika. Pia pale mutayakuta matrekta madogo ya kilimo ambayo ni vizuri kuyaangalia kwasababu yanaweza kuwa ni ukombozi katika baadhi ya mikoa kwa shughuli za kilimo. Ahsante sana *AZAKI*, karibuni tena. Halafu wapo washiriki 27 kutoka shirika la *DONBOSCO*, wale wa *DONBOSCO* naona hawakufika leo. Ahsante sana. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wabunge, vikao. Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ameniomba niwatangazie wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwamba kutakuwa na kikao muhimu sana leo, tarehe 30 Juni, 2008 saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi 432. Kamati ya Fedha na Uchumi, saa 5.00 asubuhi ukumbi namba 432 kwa kikao muhimu sana. Mheshimiwa Alhaji Mohamed Misanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameomba niwatangazie kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ya Miundombinu, ukumbi namba 231. Kwa hiyo saa 7.00 mchana Kamati ya Miundombinu ukumbi 231.

Hili tangazo muhimu sana kwa Wabunge, wote wa Mkoa ya Kusini. Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, ameniomba nitangaze kwamba leo mchana saa 8.30 hapa Dodoma katika viwanja vya *VETA*, kutakuwa na sherehe maalum ya kutiliana sahihi mkataba wa ujenzi wa Barabara ya Ndundu – Somanga kwa kiwango cha lami, kati ya Wizara ya Miundombinu na Mkandarasi anaitwa *M. A. Karafi & Sons* wa Kuwait. Hivyo Mheshimiwa Waziri, anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Miundombinu na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Pwani, Lindi na Mtwara, kuhudhuria katika ghafla hiyo hapo *VETA*, Dodoma. Saa 8.30 hafla ya utiaji sahihi mkataba wa ujenzi wa barabara ya lami, Ndundu – Somanga, Waheshimiwa Wabunge wa Pwani, Lindi na Mtwara pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Miundombinu pale *VETA*, Dodoma, mchana huu. (*Makofi*).

Kwa tangazo hili ningewaomba na Wabunge wa Mkoa wa Tabora, wahudhurie sherehe hiyo ikiwa ni mazoezi. Maanake nadhani tangazo kama hili nitaweza kurudiwa kwenye mkutano wa Bajeti mwaka ujao kuhusu barabara ya Manyoni, Itigi, Tabora, Urambo, Kaliua, Malagarasi hadi Kigoma. Kwa hiyo Mheshimiwa Seleli, Mheshimiwa Nkumba, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Kaboyonga, tafadhalini. Eeh, na Mheshimiwa Lwanji, jirani yetu, muende mukaone wenzenu wa Pwani, Lindi na Mtwara, mambo haya hutokeaje ili na sisi tujiandae kwa mwaka ujao. Ahsante sana na wa Kigoma, Mheshimiwa Zitto. Nashukuru sana. (*Makofi/Kicheko*).

Leo saa 9.00 mchana nitapokea wageni mashuhuri, ni Tume ya Huduma za Bunge za Kenya. Sasa walivyopanga Itifaki mimi nimeona mtu mzito pale ni Makamu wa Rais, lakini wao wamesema ni Spika. Wao wamesema Spika, ataambatana na Spika Marende, atakuwa na Makamu wa Rais Kalonzo Musyoka na wajumbe wengine saba (7) wa Tume ya Huduma za Bunge saa 9.00. Kwa hiyo niliona mufahamu hilo. Kesho asubuhi tutakuwa nao hapa watakuja kuangalia, kushuhudia kipindi cha Maswali na Majibu.

Kwa hiyo, pia wajumbe wote wa tume naomba tusaidiane ili tuweze kuwa *Airport* kuwapokea. Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kama kawaida yake amepanga mapokezi mazuri kwa wageni wetu hawa jirani zetu Kenya. Naomba sana wajumbe wa Tume na baadaye wenyeviti pia tutawakutanisha nao lakini yeyote ambaye atajisikia kuja kule ni vizuri akawepo pia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaendelea sasa, Katibu endelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 -Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba, kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais – Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Tume ya Mipango (Fungu 66) na Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Fedha ya Ofisi ya Rais – Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Mipango na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii, kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Makamu wake Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2008/2009, hatua ambayo imetuwzesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu tangu alipochaguliwa kushika wadhifa huo mwaka 2005. Mheshimiwa Rais katika uongozi wake ametekeleza vema si tu, yale aliyoahidi kwa wananchi wakati wa uchaguzi bali pia mengi yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005; kwa kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa kwa mafanikio makubwa sana. Mafanikio ambayo yamepatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuvutia wawekezaji, Serikali za nchi zilizoendelea na wafadhili mbalimbali kujenga imani na Serikali yetu, hivyo kuwafanya waendeleo kutoa misaada katika sekta mbalimbali. Umahiri na uadilifu wake katika uongozi umekubalika katika Jumuiya za Kimataifa hata kuwezesha achaguliwe kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendeleo kumjalilia afya njema, maarifa na hekima katika uongozi wake ili aendeleo kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais kwa kumsaidia na kumshauri Rais kwa hekima katika utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo. Nampongeza pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa

kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi hiyo na uteuzi wake kuthibitishwa kwa kishindo na Bunge lako Tukufu. Huu ni ushahidi wa kutosha na wa wazi kuwa wananchi wana imani naye katika nafasi hii aliyopewa.

Aidha, hotuba aliyoitoa mbele ya Bunge lako Tukufu wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2008/2009, ni kielelezo cha upevu wake katika uongozi kama Mshauri Mkuu wa Rais na imesaidia kuonyesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Kilosa, Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba yake ambayo imebainisha misingi na mwelekeo wa bajeti na uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2008/2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikupongeze wewe mwenyewe kwa umahiri wako katika kuliongoza Bunge hili Tukufu ambalo limetoa maamuzi mazito yaliyothibitisha upevu wake katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini. Aidha, nikupongeze pia, kwa kuteuliwa kwako kuwa Makamu wa Rais wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola. Uteuzi huu unazidi kudhihirisha jinsi Watanzania walivyopevuka katika uongozi ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais mwaka huu. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kupitia Viti Maalum akiwemo Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude P. Rwakatare na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Mbunge wa CCM, kwa ushindi alioupata katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kiteto. Ni matumaini yetu kuwa mchango wao utaongeza nguvu ya Bunge lako katika kuwatumikia wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii, pia kumshukuru Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora kwa ushirikiano wake mkubwa katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Bwana Phillemon Lutangilo Luhanjo, Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Michael Peter Mwanda, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu, Bwana George Daniel Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Balazi Charles Kashasha Mutalemwa, Katibu Mkuu (Kazi Maalum), Tume ya Mipango, Bwana Eric Francis Shitindi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Makamishna na Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais ambao wamefanya kazi kubwa katika kuwezesha hotuba hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, pia, nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wenzetu wa Wizara, Miko na Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma kwa ushirikiano wao wakati wa kuandaa hotuba hii. Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo la Mtwara Vijijini ambao walinichagua kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu na hatimaye kwa imani hiyo hiyo Mheshimiwa Rais akaniteua kushika wadhifa nilionao. Nawaahidi kwamba nitatekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa ujasiri na uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwa jamaa na familia za Wabunge wenzetu waliofariki dunia katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, marehemu Salome Joseph Mbatia ambaye hadi anafariki alikuwa Naibu Waziri, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Pia, tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie ndugu wa marehemu moyo wa subira.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kuhusu kuongezeka kwa Mafungu yanayotolewa taarifa katika hotuba hii, kutoka Mafungu matano yaliyojumuishwa katika hotuba yangu ya mwaka jana hadi sita ambayo yanatolewa taarifa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyokumbuka, mwezi Februari mwaka huu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda upya Baraza la Mawaziri. Kufuatia hatua hiyo, Serikali ilitoa tamko la mgawanyo wa majukumu ya Wizara kupitia Tangazo lake Na. 20 la Februari, 2008. Katika mabadiliko hayo, mbali ya kuunganishwa iliyokuwa Wizara ya Fedha na iliyokuwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na kuwa Wizara ya Fedha na Uchumi, iliundwa pia Tume ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais. Tume ya Mipango imerithi Fungu 66 ambalo linafanya Mafungu yanayotolewa taarifa katika hotuba hii kuwa sita, yaani Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Fungu 30 – Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 66 – Tume ya Mipango na Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma. Baadaye kidogo nitatoa maelezo zaidi kuhusu maudhui na mwelekeo wa Tume ya Mipango iliyoundwa pamoja na matazamio yetu kuhusu kazi zake.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo matatu ambayo ni; Mapitio ya Utekelezaji wa shughuli za mpango wa mwaka 2007/2008, Maelezo ya Mpango wa Kazi wa mwaka 2008/2009 na Maombi ya fedha za kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Kazi kwa Mwaka 2007/2008 wa Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais - Ikulu ina mafungu mawili, yaani Fungu 20 kwa ajili ya Ofisi ya Rais na

Fungu 30 kwa ajili ya Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Ofisi hii ina majukumu ya kusimamia masuala ya Baraza la Mawaziri, Utawala Bora, kuratibu vyombo vya Serikali ambavyo ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Aidha, Ofisi ya Rais inasimamia Usalama wa Taifa, utekelezaji wa sera ya mawasiliano kwa umma, dhifa za Serikali, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa kazi za Ikulu, usimamizi rasilimali watu na kuratibu utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ikulu ambayo ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania *Social Action Fund - TASAF*) na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Ofisi ya Rais – Ikulu iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuongoza, kufuatilia, kuratibu uendeshaji bora wa Serikali na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Rais na Baraza la Mawaziri. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika masuala ya siasa, jamii, uchumi, sheria, diplomasia na ushauri mwingine wenye lengo la kumsaidia Rais na Baraza la Mawaziri kufanya maamuzi;
- (b) Baraza la Mawaziri lilijadili na kutolea maamuzi Nyaraka 54, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu ilitoa ushauri katika Nyaraka 80. Aidha, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilijadili Nyaraka 110;
- (c) Watumishi 92 walihudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwaongezea uwezo na kuboresha utendaji wao wa kazi;
- (d) Maafisa 114 kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na TAMISEMI walipatiwa mafunzo juu ya kuandaa sera, kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maamuzi ya Serikali na utayarishaji na usambazaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri;
- (e) Wajumbe 70 wa Kamati za Uadilifu za Wizara na Taasisi za Serikali walipatiwa mafunzo kuhusu Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa Awamu ya Pili, Utawala Bora na Maadili;
- (f) Rufaa 108 za Watumishi wa Umma zilipokelewa na kuchambuliwa na uamuzi wa Rais au Katibu Mkuu Kiongozi kutolewa. Aidha, Malalamiko 413 yalipokelewa na kuchambuliwa na kutolewa uamuzi kwa maelekezo ya Rais au Katibu Mkuu Kiongozi;

(g) Wakurugenzi wa Utawala na Utumishi 26 wa Wizara, Mwakili Wafawidhi 20 wa Kanda na Makatibu Tawala Wasaidizi 20 walipatiwa mafunzo ya namna ya kushughulikia malalamiko na rufaa za watumishi wa umma na wananchi wengine; na

(h) Jengo la wageni katika Ikulu Ndogo ya Chamwino, limefanyiwa ukarabati. Aidha, uwekaji wa umeme na mfumo wa zimamoto umekamilika katika Ikulu Ndogo ya Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Jukumu kubwa la TAKUKURU ni kuzuia, kuelimisha umma juu ya rushwa na athari zake katika jamii na mbinu za kupambana na rushwa nchini; kuchunguza tuhuma mbalimbali na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa. Aidha, TAKUKURU inalo jukumu la kuishauri Serikali namna ya kuziba mianya ya rushwa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008, TAKUKURU ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Upelelezi wa tuhuma za malalamiko ya vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali nchini umeendelea na majalada 2,887 yalichunguzwa;

(b) Uchunguzi wa tuhuma 1,009 ulikamilika na hivyo hatua mbalimbali kuchukuliwa. Aidha Jumla ya kesi 378 ziliendeshwa Mahakamani. (*tazama Jedwali Na. 1*);

(c) Wachunguzi wapya 50 walijiririwa na kupatiwa mafunzo ya awali ya uchunguzi, Wachunguzi Wasaidizi 204 walihudhuria mafunzo elekezi ya wiki mbili na wachunguzi 130 walipatiwa mafunzo ya kati ya uchunguzi. Aidha, watumishi 374 walipata mafunzo ya utaalum kuhusiana na rushwa, na watumishi 135 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi;

(d) Ofisi mbili mpya katika vituo maalum na vya kibiashara vya Chalinze na Ikwiriri zimefunguliwa kati ya ofisi tisa zilizokuwa zimepangwa kufunguliwa katika kipindi cha 2007/2008 na hivyo kufanya nchi nzima kuwa na ofisi 140. Aidha, ujenzi wa jengo la ofisi ya Makao Makuu umeanza na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari 2009;

(e) TAKUKURU ilishiriki katika maonesho na maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Saba Saba na Nane Nane, kama njia mojawapo ya kuelimisha jamii juu ya madhara ya rushwa. Aidha, kalenda 150,000 za ukutani, 5,000 za mezani, majarida 44,870 na vipeperushi 140,000 vilichapishwa na kusambazwa kwa wadau.

(f) Tafiti 28 zilifanyika ili kubaini mianya ya rushwa na hatimaye kutoa mapendekezo Serikalini ya namna ya kuziba mianya hiyo; na

(g) Machapisho 7,506 yanayotokana na tafiti mbalimbali kuhusu njia bora za kuzuia na kudhibiti rushwa katika idara na Taasisi za Serikali yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania *Social Action Fund* – *TASAF*). *TASAF* ina jukumu la kusaidia jamii katika kuainisha, kuchambua mahitaji, kuweka vipaumbele, kuratibu na kukusanya rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Utekelezaji wa miradi hii una lengo la kupambana na umaskini kupitia dhana shirikishi ya jamii. Katika mwaka 2007/2008 *TASAF* ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Wajumbe 22,640 wa Kamati za usimamizi wa miradi walipata mafunzo ya utunzaji sahihi wa kumbukumbu za utekelezaji wa miradi, taratibu za ununuzi, kuandaa taarifa na kuziwasilisha kwa wadau;

(b) Jumla ya miradi 2,264 yenye thamani ya Sh.54,874,879,000/= iliibuliwa na kutekelezwa katika Halmashauri zote za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba, na hivyo kufanya miradi iliyofadhiliwa na *TASAF* Awamu ya Pili kuwa 4,402 yenye thamani ya Sh.102,217,707,479/=. (*Tazama Jedwali Na. 2*);

(c) Tathmini tatu zenye lengo la kujua utekelezaji wa miradi zilifanyika. Tathmini hizo ni ‘*Technical Audit*’ iliyokuwa na lengo la kuangalia ubora wa kazi zinazofanyika kwa kulinganisha na viwango vilivyowekwa; ‘*Beneficiary Assessment*’ ambayo ililenga kupata maoni ya walengwa wa mradi kuhusu ubora au matatizo wanayopata katika utekelezaji wa miradi na ‘*Community Score Card*’ iliyolenga kupima kiwango cha ubora wa huduma za ushauri na ufundi zinazotolewa na wataalam wakati wa utekelezaji;

(d) Tathmini yenye lengo la kupima ni kwa kiasi gani hali za maisha zimeimarika kutokana na utekelezaji wa miradi imeanza mwezi Aprili 2008 na itakamilika mwezi Desemba 2008;

(e) Utaratibu unaotumika na baadhi ya Taasisi kupitishia fedha zao *TASAF* kwa ajili ya miradi mbalimbali umeendelea kudumishwa. Miradi inayonufaika na utaratibu huu ni “*Marine and Coast Environmental Conservation Project - MACEMP*”, *Participatory Forest Management -PFM* na miradi ya UKIMWI katika Visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, kutokana na mafanikio yaliyopatikana, *TACAIDS* imeamua kuingia makubaliano na *TASAF* ili kutumia utaratibu wake katika kufadhili miradi ya makundi ya jamii inayoishi na Virusi vya UKIMWI na UKIMWI;

(f) Mafunzo yalitolewa kwa wataalam, wanajamii na viongozi 71,632 katika maeneo ya usimamizi wa fedha; usimamizi na ufuatiliaji wa miradi, utunzaji wa mazingira; usimamizi wa ununuzi na mbinu za utoaji elimu na habari;

(g) Vikundi 1,653 vyenye wanachama 21,153 vilianzishwa katika Halmashauri 44 za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba;

(h) Mafunzo ya awali ya utaratibu wa Kuweka Akiba na Kuwekeza chini ya Mpango wa Uhawilishaji Fedha kwa jamii maskini (*Community Based – Conditional Cash Transfer – CB-CCT*) ili jamii hizo ziweze kunufaika na huduma muhimu za kijamii hasa

elimu na afya umeanzishwa. Mpango huu umeanza kwa kuandaa miongozo na kutoa elimu kwa wataalam katika Halmashauri za Chamwino, Bagamoyo na Kibaha;

(i) Taasisi nne (4) za Maendeleo ya Jamii (*Community Foundations*) zimeanzishwa katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Manispaa za Arusha, Morogoro na Kinondoni; na

(j) Mwongozo ulio katika lugha rahisi wa Taratibu za Ununuzi, uliandaliwa. Mwongozo huu, una tafsiri rahisi kwa baadhi ya vipengele vya sheria kuhusu ununuzi unaoendana na shughuli za kila siku za jamii katika utekelezaji wa miradi. Hatua hii imelenga kuzisaidia jamii kufanya ununuzi katika ngazi ya jamii, kwa kufuata taratibu za ununuzi zilizowekwa na kuongeza uwajibikaji na ufanisi katika matumizi ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), madhumuni ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania – MKURABITA ni kuandaa mfumo mpya wa umiliki rasilimali na uendeshaji biashara utakaowawezesha wamiliki rasilimali (ardhi na majengo) na wafanyabiashara walio katika sekta isiyo rasmi kutambulika kisheria na kutumia mali zao kujipatia fursa zilizopo katika soko rasmi ikiwa ni pamoja na mikopo kutoka kwenye vyombo vya fedha. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 MKURABITA ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Maandalizi ya mapendekezo ya mabadiliko ya sheria mbalimbali yenye lengo la kurahisisha na kuharakisha urasimishaji wa rasilimali na biashara yamekamilika;

(b) Utaratibu rahisi wenye gharama nafuu, shirikishi na endelevu unaotokana na mabadiliko ya sheria za biashara na ardhi umeandaliwa;

(c) Upembuzi yakinifu wa awali wa mfumo wa mawasiliano kati ya masijala mbalimbali hasa zinazohusu ardhi, watu na biashara ili kuweza kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa kamilifu kuhusu umiliki mali na uendeshaji biashara kuanzia ngazi ya Kijiji/Shina hadi Taifa umekamilika. Aidha, Mkakati wa Mawasiliano kwa ajili ya kuwafikia walengwa umekamilika na utanza kutumika rasmi katika mwaka wa Fedha 2008/2009;

(d) Kanuni za uanzishaji na uendeshaji biashara ikiwa ni pamoja na mifumo mipya ya kumiliki na kuendesha biashara zimekamilika na ni sehemu ya mfumo mpya uliokusudiwa. Aidha, mafunzo ya biashara na masoko yanaendelea na walengwa 695 wamefaidika na mafunzo haya;

(e) Maandalizi ya Mwongozo wa Urasimishaji Ardhi na Biashara yameanza na yanakusudiwa kukamilika Septemba 2008;

(f) Utekelezaji wa miradi ya mafunzo/majaribio uliendelea katika Wilaya za Handeni, Bagamoyo, Kasulu na Kinondoni ambapo katika Wilaya ya Handeni jumla ya

mashamba 1,190 yamepimwa na hati miliki za kimila zimeandaliwa kwa kutumia Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999;

(g) Ujenzi wa Masijala za Vijiji saba vilivyomo katika eneo la mradi umekamilika. Viwanja 1,423 katika eneo la Hananasif katika Manispaa ya Kinondoni vimeshapimwa na ahadi za Toleo 400 zimeshatolewa. Katika Wilaya ya Bagamoyo upimaji wa ardhi katika vijiji 6 ambavyo ni Msoga, Kihangaiko, Fukayosi, Kiwangwa, Msinune na Masuguru unaendelea. Upimaji wa ardhi unakwenda sambamba na ujenzi wa masijala za vijiji hivi 6. Aidha, mpango wa ujenzi wa masijala ya wilaya ya Bagamoyo umeanza. Mashamba makubwa 25 yamepimwa Wilayani Kasulu na maandalizi ya Hati za Hakimiliki yanaendelea kukamilishwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Baada ya kutoa taarifa ya mapitio kuhusu Ofisi ya Rais – IKULU, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 32.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa kubuni na kuhuisha sera, sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za umma, kujenga uwezo wa watumishi wa umma ili watoe huduma bora kwa wananchi na kuweka mifumo ya uendeshaji na muundo wa Serikali unaoleta tija na ufanisi katika utendaji kazi. Katika kufanikisha majukumu haya, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma inatekeleza Programu ya Mabadiliko ya Utendaji katika Utumishi wa Umma inayolenga kuinua kiwango cha utoaji huduma katika Utumishi wa Umma. Chini ya mpango huu maeneo yanayopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuhakikisha watumishi wa umma wanafanya kazi kwa uaminifu na uadilifu na kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na taratibu zilizopo;

(b) Kuhakikisha kwamba katika kuajiri watumishi wa umma masuala ya ujuzi na anuai za jamii yanazingatia sera, sheria, kanuni na taratibu na kwamba watumishi wanaendelezwa ili kuwajengea uwezo zaidi;

(c) Kuhakikisha utendaji kazi wa watumishi unapimwa na kutuzwa kulingana na viwango vya utendaji kazi vilivyopo na kwamba kuna mazingira mazuri ya kazi ambapo sheria na kanuni zinatumiwa kwa haki na usawa;

(d) Kuhakikisha kwamba mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano inaimarishwa Serikalini na inatumiwa kutoa taarifa katika kufanya maamuzi sahihi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa umma;

(e) Kuhakikisha kwamba Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Ofisi za Mikoa zinajishughulisha na majukumu mahsusi tu ya Serikali ambayo yanaendeshwa kwa gharama nafuu na kuachia shughuli zingine kutekelezwa na sekta binafsi; na

(f) Kuhakikisha wananchi wanaarifiwa vilivyo kuhusu huduma wanazotarajia kuzipata Serikalini na kuwa na Utumishi wa umma unaojali wateja.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, mojawapo ya shughuli muhimu za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ni kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko ya Utendaji katika Utumishi wa Umma. Programu hii imepangwa kutekelezwa kwa awamu kuanzia mwaka 2000 hadi 2012. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu hii, iliyopangwa kufanyika kati ya mwaka 2000 hadi 2007 sasa imekamilika. Awamu ya pili ya programu ilipangwa kuanza mwaka 2008 hadi 2012. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Awamu hii ilianza rasmi baada ya kuzinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 28 Januari, 2008.

Mheshimiwa Spika, Awamu hii ya Pili ya Programu ya Mabadiliko ya Utendaji katika Utumishi wa Umma imelenga kuimarisha utendaji unaojali matokeo na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Katika kutekeleza awamu hii, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itakuwa na jukumu la kuziwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Sekretarieti za Mikoa kujenga uwezo wa kusimamia, kupanga na kutekeleza shughuli za mabadiliko kulingana na vipaumbele vyao. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara ishirini na tano (25) zimewezeshwa kupanga mipango ya mabadiliko na kuijumuisha katika mpango wao wa kazi wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upandishwaji vyeo, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2007/2008 tuli ahidi kushughulikia suala la upandishwaji vyeo kwa watumishi wa umma Serikalini 85,267. Napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wa umma Serikalini lilifanyika.

Aidha, wachache waliobakia kutokana na sababu mbalimbali wanaendelea kushughulikiwa na kutumiwa barua zao. Katika kuhakikisha kwamba watumishi wa umma Serikalini wanapandishwa vyeo kwa wakati, imetolewa miongozo inayowaelekeza waajiri kuendesha mazoezi ya upandishwaji vyeo kwa wakati ili kuepuka watumishi kukaa katika ngazi moja kwa muda mrefu bila sababu za msingi kama ilivyotokea katika siku zilizopita.

Mheshimiwa Spika, ajira mpya na mbadala. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kugharamia ajira mpya na mbadala 41,435. Hadi Juni, 2008 idadi ya nafasi zilizoidhinishwa kujazwa kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mikoa na Serikali za Mitaa zilikuwa 36,331. Kati ya hizo, ajira mpya 33,402 na ajira mbadala 2,929. Bado tunaendelea kupokea taarifa zinazohusu utekelezaji wa vibali vilivyotolewa kutoka kwa waajiri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mishahara. Katika mwaka 2007/2008, Serikali iliendelea kufanya marekebisho ya maslahi ya watumishi kwa kuanza kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kuboresha Maslahi ya Watumishi wa Umma na kwa kuzingatia Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma. Mapendekezo ya

Tume yamegawanyika katika makundi mawili; kundi la kwanza ni mapendekezo yanayohusu umuhimu wa kuboresha maslahi ya watumishi wa umma; na kundi la pili linahusu njia mbalimbali za kuongeza mapato ili Serikali iweze kumudu kugharimia uboreshaji wa maslahi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mapendekezo ya Tume, Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma lilifikia uamuzi wa kupandisha kima cha chini cha mishahara wa watumishi Serikalini kutoka Sh.80,760/= hadi Sh.100,000/= kwa mwezi kuanzia Januari 2008. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa bajeti, utekelezaji wa mabadiliko haya kwa maana ya kuanza kulipa mishahara hiyo mipya na malimbikizo utafanywa kuanzia Julai 2008. Aidha, mapendekezo mengine ya Tume yanaendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha lengo lililokusudiwa katika Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma linafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliendesha zoezi la kuhakiki rasilimali watu na kugundua kuwepo kwa watumishi hewa 1,413 katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika eneo la Shule za Sekondari, waliosababisha hasara za ya Sh.3,043,609,699/= kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, maeneo mengine yaliyofanyiwa uhakiki huo na matokeo ya uhakiki ni kama ifuatavyo. Manispaa ya Ilala ambako tulikuta watumishi hewa 40, Manispaa ya Kinondoni ambako tulikuta watumishi hewa 12, Wizara ya Maliasili na Utalii ambako tulipata watumishi hewa 36 na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Morogoro ambako hakukuwa na mtumishi hewa, jumla ya watumishi hewa waliogundulika katika zoezi hili ni 1,501 waliosababisha hasara ya Sh.3,174,133,809/=, taratibu za kuwachukulia hatua za kisheria au za kinidhamu kwa wale wote waliohusika na kusababisha kuwepo kwa watumishi hewa zinashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo niliyoyatoa hapa juu kuhusu shughuli zilizofanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2007/2008, yapo mafanikio mengine yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango wa mwaka 2007/2008. Mafanikio hayo ni kama yafuatavyo:-

(a) Katika jitihada za kuboresha na kuinua kiwango cha utoaji huduma katika utumishi wa umma mafanikio yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Miundo ya Wizara ishirini na tatu (23), Idara Zinazojitegemea kumi na moja (11) na Wakala wa Serikali nne (4) ilihuishwa na kuidhinishwa;

(ii) Orodha za kazi za Wizara saba (7), Idara Zinazojitegemea kumi na moja (11) na Wakala za Serikali sita (6) ziliandaliwa na kuidhinishwa;

(iii) Wakala 4 za Serikali zilianzishwa na hivyo kufanya idadi ya wakala zilizoanzishwa hadi sasa kufikia ishirini na tisa (29). (*Tazama Jedwali Na. 3*);

(iv) Mafunzo ya mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utendaji kazi katika Wizara 29 na Sekretarieti za Mikoa 21 yalitolewa;

(v) Wizara na taasisi ishirini na tatu (23) ziliwezesha kutumia Sekta Binafsi katika kutoa huduma za mapokezi, ulinzi na usafi;

(vi) Watumishi katika Wizara tatu (3) walipata mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kompyuta wa taarifa za kiutumishi;

(vii) Ofisi 6 za Wakuu wa Mikoa zilizokuwa zimesalia ziliwekewa mfumo bora wa utumiaji na utunzaji wa kumbukumbu. Aidha, kazi kama hiyo ilianza katika ofisi 9 za Wakuu wa Wilaya;

(viii) Viongozi na watumishi 360 walipatiwa mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi yaliyolenga katika kuongeza ujuzi na ufanisi katika utendaji wao wa kazi; na

(xi) Kuwapatia watumishi wanawake 40 mafunzo ya uzamili kama njia mojawapo ya kuwajengea uwezo wa kushika nafasi za maamuzi katika utumishi wa umma. (*Tazama Jedwali Na. 5, 6 na 7*).

(b) Katika kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimaliwatu mafanikio yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma (1998), ilifanyiwa marekebisho na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 1994 zipo katika hatua ya mwisho ya marekebisho. Aidha, Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 ilihuishwa;

(ii) Miongozo kuhusu namna ya kutayarisha Mikataba ya Huduma kwa Mteja, Mipango ya Rasilimaliwatu Katika Utumishi wa Umma, Mpango Mkakati na Bajeti, Kudhibiti Kuenea kwa maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi na kuhudumia watumishi waathirika iliandaliwa na kukamilishwa;

(iii) Mkutano wa mwaka wa Wakurugenzi wa Utawala na Utumishi, Maafisa Utawala Wakuu Wafawidhi na Makatibu Tawala Wasaidizi toka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretarieti za Mikoa ulifanyika. Mkutano huo una lengo la kuwajengea maofisa hao uwezo wa kuandaa mikakati ya kuboresha huduma katika taasisi zao. Aidha, mkutano wa mwaka wa Makatibu Tawala wa Wilaya ulifanyika mwezi Mei 2008 hapa Dodoma;

(iv) Mfumo wa kushughulikia malalamiko uliandaliwa na kufanyiwa majaribio katika Wizara 7, na ulionyesha mafanikio kwani kwa kiasi kikubwa ulirahisisha ushughulikiaji wa kero za wananchi;

(v) Zoezi la uhakiki wa watumishi lilifanyika katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambapo liliendeshwa katika shule zote za Sekondari, Halmashauri za Manispaa za Kinondoni na Ilala na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kazi hii kwa hivi sasa inaendelea kufanywa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii;

(vi) Mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara umeunganishwa na kutumika katika Wizara 19 (*Tazama Jedwali Na. 4*). Lengo la mfumo huu ni kurahisisha ushughulikiaji wa malipo na maslahi mbalimbali ya watumishi tangu wanapojiunga na Utumishi wa Umma na kuendelea hadi wakati wa kustaafu au kuacha kazi;

(vii) Utafiti kuhusu namna ya kuzingatia masuala ya anuai za jamii katika utumishi wa umma umefanyika.

(c) Katika kuelimisha umma juu ya mambo mbalimbali yanayohusu utendaji na mwelekeo wa utumishi wa umma mafanikio yafuatayo yalipatikana:-

(i) Elimu kwa umma kuhusu mabadiliko katika utumishi wa umma ilifanyika kupitia vipindi vya televisheni, radio na makala za magazeti. Aidha vitabu na machapisho mbalimbali yalitayarishwa na kusambazwa sehemu mbalimbali kwa madhumuni hayo;

(ii) Mikutano ya wadau wa utumishi wa umma na watendaji ya kujadili utendaji kazi wa watumishi wa umma na mifumo ya utendaji kazi kama vile Mfumo wa Wazi wa Kupitia na Kupima Utendaji (*Open Performance Review and Appraisal System - OPRAS*) na mikataba ya Huduma kwa Mteja ilifanyika katika Wilaya 6 za Mkoa wa Lindi;

(iii) Wiki ya Utumishi wa Umma ilifanyika kwa mafanikio makubwa kati ya tarehe 16 - 23/06/2008. Taasisi za umma 115 zilishiriki katika kufanya maonyesho ya shughuli zao katika wiki hii; na

(iv) Kongamano kuhusu uimarishaji wa utendaji katika utumishi wa umma lilifanyika kwa kushirikisha Washirika wa Maendeleo, Watendaji Wakuu kutoka Wizara, Idara Zinazojietegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, Viongozi wa Madhehebu ya Dini, Vyama vya Kijamii na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi.

(d) Ujenzi wa jengo la Serikali Mtandao ulikamilika na jengo kuanza kutumika; na

(e) Viongozi wastaafu wa kitaifa 12 waliendelea kuhudumiwa kwa mujibu wa Sheria Na. 3 ya mwaka 1999 pamoja na Marekebisho yake ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Chuo cha Utumishi wa Umma, kilijielekeza katika kujenga uwezo wake ili kiweze kutoa mafunzo ya kuongeza ujuzi na ufanisi katika utendaji kama njia mojawapo ya kusaidia utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko ya Utendaji katika Utumishi wa Umma. Mafanikio yafuatayo yalipatikana kutokana na utekelezaji wa mpango wa kazi wa mwaka 2007/2008:-

- (a) Muongozo wa kuendeleza stadi za kazi uliandaliwa na kuanza kutumika;
- (b) Mitaala minne (4) iliandaliwa kwa ajili ya mafunzo ya uongozi katika Utumishi wa Umma;
- (c) Maandalizi ya kufungua tawi la Chuo Mtwara yameanza kwa kupata jengo litakalotumiwa na Chuo; na
- (d) Watumishi wanane (8) wamepelekwa kwenye mafunzo ya shahada ya uzamili; na
- (e) Majengo ya chuo yaliyopo Dar-es-Salaam, yamefanyiwa ukarabati ambapo vyumba vinne (4) vya madarasa, ofisi nane (8) na chumba kimoja cha ukumbi wa mikutano viliongezwa.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo kwa Mtandao (TGDLIC). Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo kwa Mtandao (TGDLIC), kimekuwa kitovu cha mafunzo na midahalo ya maendeleo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000. Kituo hiki ni kimojawapo kati ya mtandao wa vituo zaidi ya 130 duniani vinavyotumia teknolojia ya habari na mawasiliano. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, viongozi mbalimbali, wadau kutoka serikali za mitaa, vikundi vya vijana, wanafunzi, wataalamu mbalimbali, vikundi vya wanawake wajasiriamali, wanaharakati dhidi ya UKIMWI na wengine wengi walifaidika na teknolojia inayowawezesha kupata taarifa mbalimbali za maendeleo wakiwa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, kituo kimeweza kutoa mafunzo kwa jumla ya washiriki 2,226 katika fani ya Uongozi, midahalo ya kitaaluma ya Serikali za Mitaa, midahalo ya kupambana na UKIMWI, midahalo na mafunzo mengine katika nyanja mbalimbali za ufanisi kazini na matumizi ya kompyuta kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, ulifanywa upembuzi yakinifu kwa ajili ya mpango wa vituo vishiriki Mikoani. Matokeo ya upembuzi huo yameonesha kuwa kutakuwa na manufaa makubwa ikiwa kituo kitafanikiwa kuwa na vituo Mikoani, ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya washiriki watakaonufaika na hivyo kutoa nafasi kubwa zaidi kwa Watanzania kupata taaluma muhimu zitakazoboresha utendaji wa kazi na kuongeza ufanisi. .

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ni chombo kinachohusika na kujenga imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa viongozi wa umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliweka mkazo katika kukuza dhana ya utawala bora, hususan, maadili ya viongozi na ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kupokea na kuhakiki tamko la mali na madeni ya viongozi wa umma kwa mujibu wa Sheria Na. 13 ya mwaka 1995. Viongozi wa umma 4,864 walirejesha Fomu za Tamko la Mali na Madeni kati ya viongozi 7,447 waliotumiwa Fomu za Tamko. Mchanganuo wa viongozi hawa ni kama ifuatavyo: Viongozi wa Siasa ni 2,130 kati ya 3,983, Viongozi wa Utumishi wa Umma ni 2,734 kati ya 3,464. Orodha ya Viongozi wa Umma 3,186 ambao hawajarejesha Fomu ya Tamko kwa majina na mahali walipo imeandaliwa na hatua zaidi zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria;
- (b) Kuchunguza malalamiko ya wananchi dhidi ya viongozi wanaotuhumiwa kukiuka maadili ya viongozi. Jumla ya malalamiko 88 yalipokelewa. Malalamiko hayo yako katika hatua mbalimbali za uchunguzi baada ya kufanyiwa uchambuzi wa awali ili kubaini yale yanayohusiana na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (c) Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma 260 wa ngazi mbalimbali nchini kote yalihakikiwa ili kubaini usahihi wa taarifa walizotoa kuhusu mali na madeni yao. Kutokana na uhakiki huo, viongozi wanne (4) walibainika kuwa na mali zaidi ya zile walizotaja katika Tamko lao, na Sekretarieti imeanzisha uchunguzi wa kina dhidi yao;
- (d) Elimu ya maadili kwa viongozi wa umma na kwa wananchi kwa njia mbalimbali ikiwemo radio, semina na machapisho mbalimbali ilitolewa. Jumla ya kalenda 6,000 za ukutani na 1,000 za mezani zenye ujumbe kuhusu maadili zilichapishwa, na vipindi 572 vya radio viliandaliwa na kurushwa na vituo vya radio mbalimbali nchini. Aidha, vipindi 9 vya Televisheni vilirushwa na *TBCI* na *ITV*. Vipindi hivi vyote vinasisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili bora kwa Viongozi wa Umma na wananchi kwa ujumla;
- (e) Watumishi 19 wa kada mbalimbali wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma walipatiwa mafunzo ya muda mfupi hapa nchini na nje ya nchi ili kuboresha utendaji wao wa kazi;
- (f) Ofisi sita za Kanda zilizopo Arusha, Dodoma, Mbeya, Mtwara, Mwanza na Tabora ziliimarishwa kwa kuajiri watumishi wapya na kununua vitendea kazi;
- (g) Uandaaji wa mfumo wa kanzi data (*data bank*), umekamilika kwa ajili ya Viongozi wa Umma na rasilimali zao. Aidha, uwekaji wa mtandao wa ndani wa Kompyuta (*Local Area Network - LAN*), *Server*” na uwekaji wa mifumo ya kompyuta, umekamilika;
- (h) Maandalizi ya kupitia upya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Na. 13, ya mwaka 1995, kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali ya kutenganisha Uongozi Serikalini na Biashara yamekamilika. Lengo la mabadiliko haya ni kukidhi mahitaji ya muda wa kati na mrefu katika kuimarisha na kuinua viwango vya maadili bora miongoni mwa viongozi wa umma, hususan katika mgongano wa maslahi;

(i) Rasimu ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lugha nyepesi imekamilika; na

(j) Shughuli za Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi, kupitia Kamati ya Uendeshaji wa Mfuko ziliendelea kusimamiwa. Kamati ya Uendeshaji wa mfuko imekamilisha uchambuzi wa maombi ya awali 177 yaliyowasilishwa kwa ajili ya kupatiwa ruzuku na inakamilisha taratibu za kuidhinisha fedha za ruzuku kwa waombaji waliopitishwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma. Tume ya Utumishi wa Umma inao wajibu wa kuhakikisha kwamba masuala yote ya utumishi yanaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa ajira katika utumishi wa umma inazingatia sifa, uwezo na ushindani kwa madhumuni ya kufanikisha utendaji wenye malengo na matokeo yanayopimika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kazi zilizopangwa mwaka 2007/2008, Tume ya Utumishi wa Umma imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Ukaguzi wa uzingatiaji sheria, kanuni na taratibu zinazohusu rasilimali watu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 51 na ukaguzi maalum katika Wizara nne, umekamilika;

(b) Rufaa 178 kati ya rufaa 215 zilizowasilishwa Tume zimefanyiwa kazi na kutolewa maamuzi;

(c) Mashauri ya nidhamu 157 kwenye Idara ya Utumishi wa Walimu yameshughulikiwa;

(d) Jumla ya malalamiko 168 yamepokelewa na kushughulikiwa na maamuzi kutolewa;

(e) Walimu 11,304 kati yao wanaume 5,659 na wanawake 5,645, wamesajiliwa. Aidha, walimu 9,638 kati yao wanaume 4,077 na wanawake 5,561 wamethibitishwa kazini;

(f) Jumla ya Walimu 3,335 waliojiendeleza na kujiongezea sifa za kielimu wanaume wakiwa 1,988 na wanawake 1,347, wamebadilishiwa vyeo kulingana na miundo yao;

(g) Maafisa Wateule (*Focal Persons*) 123, wamepewa mafunzo ili waweze kuzisaidia mamlaka zao za ajira na nidhamu kutekeleza majukumu yao kikamilifu;

(h) Maafisa wa Tume wameshiriki katika vikao 101 vya Bodi za Ajira za Halmashauri, vikao 126 vya Kamati Maalum za Ajira za Wizara na Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali na vikao 3 vya Kamati za Sekretarieti za Mikoa;

(i) Jumla ya walimu 43,575 waliokuwa wamelundikana katika cheo kimoja kwa muda mrefu wamepandishwa vyeo;

(j) Elimu kuhusu namna ya kuboresha Utumishi wa Umma ilitolewa kwa wadau mbalimbali kupitia vipindi vya radio na magazeti. Jumla ya vipindi vya radio 52 vilirushwa hewani kupitia TBC Taifa na machapisho 52 kupitia magazeti;

(k) Watumishi 103 wamedhaminiwa na Tume kuendelea na mafunzo mbalimbali;

(l) Taratibu za Uendeshaji za Utumishi wa Afya zimekamilika, za Utumishi wa Serikali za Mitaa zipo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na za Utumishi wa Walimu zipo kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi; na

(m) Tume iliwasilisha mapendekezo ya ushirikiano wa Tume za Utumishi za Afrika Mashariki kwenye Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, Tume imetembelea Tume ya Utumishi Serikalini Zanzibar kubadilishana uzoefu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kazi wa Mwaka 2008/2009, wa Ofisi ya Rais – Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Mipango na Tume ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Ikulu. Ofisi ya Rais, Ikulu itaendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Ofisi ya Rais Ikulu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na kumpatia ushauri katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya uchumi, siasa, jamii, sheria na uhusiano wa Kimataifa;

(b) Kushughulikia rufaa za watumishi wa umma zinazopelekwa kwa Rais na kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

(c) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti na Kupambana na Rushwa Awamu ya Pili na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;

(d) Kuendelea na uchambuzi wa nyaraka na kutoa ushauri kwa Wizara juu ya uandishi wa nyaraka za Baraza la Mawaziri, kuhudumia Baraza la Mawaziri na Kamati zake; Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu. Aidha, Sekretarieti itafuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri;

(e) Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa kushirikiana na “*Better Regulation Unit*” itafanya uchambuzi wa nyaraka kwa kutumia mfumo wa “*Regulatory Impact Assessment – RIA*” kwa lengo la kuhakikisha kuwa utekelezaji wa masuala ya kisheria na kiseria yaliyoamuliwa na Baraza la Mawaziri yanaleta matokeo tarajiwa;

(f) Kukamilisha Mfumo wa Upashanaji Habari na Mawasiliano na kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi juu ya utumiaji wa mfumo huo;

(g) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kupambana na UKIMWI mahali pa kazi;

(h) Kutoa mafunzo kwa watumishi kulingana na mpango wa mafunzo ili kuwaongezea ujuzi na ubora wa utendaji; na

(i) Kupitia upya Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kufuatilia utekelezaji wake. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mwaka 2008/2009. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kuendelea na uchunguzi wa tuhuma 1,888 zilizopo na nyingine zitakazowasilishwa. Kipaumbele kitawekwa katika tuhuma za rushwa kubwa kwenye maeneo ya mikataba mikubwa, Ununuzi Serikalini, matumizi ya fedha za Serikali katika miradi mikubwa pamoja na tuhuma nyingine zitakazoonekana kuisababishia Serikali hasara;

(b) Kuendesha kesi 314 zilizopo Mahakamani na nyingine zitakazoendelea kufikishwa Mahakamani;

(c) Kufanya tafiti 7 kubwa Makao Makuu na 42 ndogondogo Mikoani katika sekta za umma na binafsi kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa;

(d) Kuendelea kuelimisha watumishi wa TAKUKURU na wananchi juu ya sheria mpya ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ikienda sambamba na utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa dhidi ya Rushwa Awamu ya Pili. Aidha, mkakati wa kuelimisha umma juu ya rushwa nchini utapewa kipaumbele;

(e) Kuelimisha wananchi kuhusu vita dhidi ya rushwa kwa kutumia vyombo vya habari, machapisho mbalimbali pamoja na jarida la TAKUKURU ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa wananchi na wadau wote;

(f) Kuajiri watumishi 192 na kufungua ofisi ndogo 7 katika vituo maalum na vya kibiashara ambapo kuna kero nyingi za rushwa. Maeneo hayo ni Makambako, Ilula, Isaka, Holili, Mtukula, Kyaka na Tunduma;

(g) Kutoa mafunzo ya uchunguzi kwa watumishi 202, mafunzo elekezi kwa watumishi 140, mafunzo ya uongozi kwa watumishi 40 na mafunzo maalum kwa watumishi 195; na

(h) Kujenga ofisi moja (1) ya Mkoa wa Manyara na ofisi mbili (2) za Wilaya za Mpanda na Iramba, na kukamilisha jengo la Makao Makuu ya TAKUKURU lililopo Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). *TASAF* Awamu ya Pili, itaendelea kushirikiana na jamii katika kuibua miradi na kuiwezesha miradi hiyo kutekelezwa ili kuboresha hali yao ya maisha. Katika mwaka 2008/2009, *TASAF* imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuziwezesha jamii zote Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba kutekeleza jumla ya miradi 1,950;

(b) Kutoa elimu ya uwezeshaji kwa wataalam wa Halmashauri zote za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba kuhusu elimu ya ujasiriamali kwa miradi ya makundi maalum ili kuziinua jamii hizi kiuchumi;

(c) Kuhamasisha jamii ili kujiunga katika mpango wa Kuweka na Kuwekeza. Jumla ya wanajamii 42,000 wanatarajiwa kunufaika na mpango huu;

(d) Kuandaa hadidu za rejea kwa wataalam 246 watakaotoa huduma kwa jamii katika utekelezaji wa miradi;

(e) Kuiwezesha jamii kutekeleza jumla ya miradi 500 inayofadhiliwa na wahisani wengine wanaopitishia fedha zao *TASAF*;

(f) Kuwafikia maskini zaidi ya 2,000 katika mpango wa uhawilishaji wa fedha kwa jamii maskini ili kuwawezesha kunufaika na huduma za kijamii;

(g) Kutoa elimu kwa wajumbe wote wa Halmashauri za vijiji, Kamati za Mitaa na Mabaraza ya Ushauri ya Sheha ambapo miradi inayofadhiliwa na *TASAF* inatekelezwa ili kuwawezesha kusimamia miradi kwa ufanisi;

(h) Kufanya tathmini ya mipango ya majaribio iliyobuniwa na *TASAF* na kutekelezwa na Halmashauri chache, ili kuona kama inaweza kutekelezwa na Halmashauri zote za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba. Mipango hiyo ni: Uhawilishaji Fedha kwa jamii maskini (*Community Based – Conditional Cash Transfer – CB-CCT*) na uanzishwaji wa Taasisi za Maendeleo ya Jamii (*Community Foundations*);

- (i) Kusimamia mpango wa motisha unaojulikana kama “*Carbon Finance*” kwa wahifadhi misitu kama hatua ya kupunguza hewa chafu katika anga. Mpango huu unasisitiza matumizi ya njia mbadala kama vile “*bio – gas*” badala ya mkaa au kuni;
- (j) Kuelimisha na kutoa mafunzo juu ya uanzishaji wa Taasisi za Maendeleo ya Jamii kwa Halmashauri 10 za Miji;
- (k) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya shughuli za *TASAF* kwa kushiriki katika maonyesho Wiki ya Utumishi wa Umma, Saba Saba na Nane Nane;
- (l) Kufanya tathmini kwa jamii inayotekeleza miradi inayofadhiliwa na *TASAF* ili kuhakikisha kama jamii hizo zinafaidika na miradi waliyoiibua;
- (m) Kufanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa fedha za miradi zinatumiwa kama ilivyokusudiwa na viwango vya ubora kuzingatiwa kwa mujibu wa vigezo vya sekta husika;
- (n) Kuwajengea uwezo Waratibu na Wahasibu wa *TASAF* katika Halmashauri za Tanzania Bara na Visiwa vya Unguja na Pemba ili waweze kusimamia utekelezaji wa miradi; na
- (o) Kutoa taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na *TASAF* kwa wadau ili kutathmini hali ya utendaji wa Mfuko.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Katika mwaka 2008/2009 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania utaendelea kuratibu utekelezaji wa Awamu ya Tatu kama ifuatavyo:-

- (a) Kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria na ya kitaasisi yatakayoweza kuanzisha mfumo tarajiwa wa urasimishaji ardhi na biashara kwa kasi na ufanisi zaidi;
- (b) Kusimamia na kuratibu urasimishaji wa ardhi katika vijiji 60 kwenye Wilaya 10 kwa kutumia mfumo mpya ulioboreshwa. Wilaya hizo ni Serengeti, Makete, Rufiji, Nachingwea, Musoma, Mbozi, Njombe, Mpwapwa, Mvomero na Pemba Mkoani;
- (c) Kusimamia na kuratibu urasimishaji wa ardhi mijini kwa kuanzia na Mikoa miwili (2) ya Tanzania Bara ambayo ni Dar es Salaam na Mbeya. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazotekelezwa, ni kama zilivyoonyeshwa katika Kitabu cha hotuba ukurasa wa 44 na 45 ambayo ni:-

- (d) Kuanzisha na kutekeleza kampeni za uhamasishaji nchi nzima juu ya mapendekeo ya mabadiliko yaliyoandaliwa kuhusu umiliki wa rasilimali na biashara;
- (e) Kusimamia uanzishwaji wa vituo viwili vya mawasiliano kwenye maeneo ya uendeshaji biashara na umiliki wa ardhi ili kuwawezesha walengwa kupata taarifa zote zonazohusu urasimishaji wa rasilimali na biashara pamoja kutambua fursa zilizopo kwa walengwa waliorasimisha rasilimali zao na biashara;
- (f) Kukamilisha upembuzi yakinifu juu ya uanzishwaji wa Masijala ya Kitaifa itakayoimarisha mawasiliano kuhusu umiliki wa ardhi na biashara na mwenendo wake katika soko;
- (g) Kufanya majaribio ya matumizi ya rasilimali katika kupata mikopo kwa kuanzia miji ya Arusha, Mbeya ya Zanzibar; na (*Makofi*)
- (h) Kuandaa mfumo rahisi wa kutunza kumbukumbu za mahesabu ya biashara na ulipaji kodi ili uwe kivutio cha kutumia miundo mipya ya biashara iliyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, itaendelea kusimamia utekelezaji wa *program* ya mabadiliko ya utendaji katika Utumishi wa Umma. Utekelezaji wa program hii katika kipindi hiki utajielekeza katika kuziwezesha Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekretarieti za Mikoa kujijengea uwezo wa kusimamia, kupanga na kutekeleza mabadiliko haya kulingana na vipaumbele watakovyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, taratibu za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa program katika Wizara zitafanyika, ili kubaini upungufu na kuangalia uwezekano wa kurekebisha kadri utakavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Upandishaji wa vyeo. Katika mwaka fedha 2008/2009 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kugharamia ajira mpya 34,894 kati ya nafasi hizo 14568 ni kwa ajili ya Wizara, Idara zinazojitegemea, nafsi 994 ni kwa ajili ya Sekretarieti za Mikoa na nafasi 19332 ni kwa ajili ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sekta zilizopewa kipaumbele katika mgao wa nafasi hizo, ni Elimu nafasi 17,037 sawa na 49%, Afya nafasi 4132 sawa na 11.8%, Kilimo nafasi 871 sawa na 2.5%, Mifugo nafasi 691 sawa na 2% na nafasi zilizobaki 12,163 ni kwa ajili ya sekta nyingine. Aidha, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi 54,665 idadi hii inajumuisha watumishi 25,672 kutoka Wizara na Idara zinazojitegemea, watumishi 1783 kutoka Sekretarieti za Mikoa na watumishi 27,210 kutoka Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Mishahara. Mwaka 2008/2009, Serikali imepanga kutumia Shilingi trillion 1.458 kwa ajili ya kugharamia malipo ya mishahara kwa watumishi. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 277.51 ambazo ni sawa na 24%

ikilinganishwa na kiasi cha shilingi trillion 1.180 zilizopangwa kutumika katika mwaka wa fedha 2007/2008, kiasi hiki kitatumika kugharamia nyongeza ya mishahara zilizoanza mwezi Januari, 2008 ajira mwaka, upandishwaji wa vyeo na nyongeza za kawaida za mishahara za mwaka. Mishahara imeongezeka kati ya 17% hadi 30%. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Rais kwa kuhakikisha njia za kuongeza mapato zinaimarishwa na kusimaiwa ili kuongeza uwezo wa Serikali wa kuboresha maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizopagwa kutekelezwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kama zilivyoorodheshwa katika Kitabu cha hotuba ukurasa wa 47 – 51 ambazo ni kama ifuatavyo:-

(a) Katika eneo la kuziwezesha Wizara na Taasisi za Serikali kuinua kiwango cha utoaji huduma, kazi zifuatazo zinakusudiwa kutekelezwa:-

(i) Kuendelea na kazi iliyoanza ya kuziwezesha Wizara na Taasisi nyingine za Serikali kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini; (*Makofi*)

(ii) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa miundo ya Wizara, Idara zinazojitegemea ili kuona kama lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi limefikiwa. Aidha, tathmini inalenga pia kuainisha majukumu yanayoweza kutekelezwa vizuri na Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa au sekta binafsi;

(iii) Kukamilisha Sera ya Taifa ya Utunzaji kumbukumbu na nyaraka. Aidha, kazi ya kuweka mfumo mpya wa Utunzaji wa kumbukumbu na uhifadhi wa nyaraka katika Halmashauri za Wilaya na Ofisi za Wakuu wa Wilaya 20, itaendelea;

(iv) Kubadilisha Idara 2 za Serikali kuwa Wakala;

(v) Kukamilisha mfumo wa uwajibikaji na kuandaa mifumo mipya ya utendaji kazi kwa matumizi ya Wizara, idara zinazojitegemea na wakala za Serikali. Kazi hii itajumuisha pia kuandaa mwongozo wa viwango vya menejimenti vitakavyotumika katika taasisi hizo; na

(vi) Kuendelea kuhusiana miundo ya Wizara, Idara zinazojitegemea kulingana na mahitaji kwa lengo la kuongeza ufanisi wa taasisi husika. Kazi hii, itajumuisha pia kuziwezesha taasisi hizo kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma ambazo si lazima zitolewe na Serikali. Aidha, mwongozo wa ushirikishaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma utahuishwa. (*Makofi*)

(b) Katika eneo la kuimarisha utawala, uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimali watu, kazi zifuatazo zitafanyika:-

(i) Kuendelea kuhuisha Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazosimamia utendaji katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kuendelea na zoezi la uhakiki wa rasilimali watu pamoja na orodha ya malipo ya mishahara (*payroll inspection*) katika Wizara, idara zinazojitegemea, wakala, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya. Lengo likiwa ni kubaini na kushughulikia kasoro zilizopo katika matumizi ya rasilimali watu na fedha za mishahara; (*Makofi*)

(iii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kushughulikia malalamiko na kero mbalimbali za wadau wa Serikali na pia kutoa elimu juu ya matumizi ya mfumo huo;

(iv) Kuendelea kuziwezesha Wizara na Taasisi za Serikali kuandaa program za kudhibiti kuenea kwa UKIMWI katika sehemu za kazi na kusimamia utekelezaji wake;

(v) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wake na wale wenye ulemavu ili waweze kuhimili mazingira ya ushindani katika ajira na katika kushika nafasi za juu za maamuzi;

(vi) Kuendelea kuboresha mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara. Hii itajumuisha pia kutengeneza sera ya usalama wa mfumo huo, kutoa mafunzo ya kuunganisha katika Wizara na taasisi mbalimbali zilizobaki;

(vii) Kuanzisha taasisi ya uongozi katika Utumishi wa Umma; na

(viii) Kuendelea kuratibu shughuli za mafunzo kwa watumishi wa umma, yanayotolewa na wahisani mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi.

(c) Katika eneo la kuelimisha umma kuhusu hali na mwelekeo wa Utumishi wa Umma, kazi zifuatazo zitafanyika:-

(i) Kuendelea kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu *program* ya kuboresha Utumishi wa Umma kupitia vipindi vya radio, machapisho na makala mbalimbali, vijitabu, kushiriki katika maonyesho kama vile Wiki ya Utumishi wa Umma, Sabababa na Nanenane; na

(ii) Kuandaa mikutano na Waandishi wa Habari pamoja na Wadau mbalimbali yenye lengo la kutangaza taarifa mbalimbali zinazohusu mwenendo wa Utumishi wa Umma na Program ya Mabadiliko kwa kadri inavyoendelea kutekelezwa.

(d) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha kuhifadhia kumbukumbu tuli, cha Dodoma na kituo cha Kanda ya Mwanza, utaanza;

(e) Kuanzisha Kituo cha kuwaenzi waasisi wa Taifa letu;

(f) Kuweka miundombinu ya Serikali mtandao utakaoziunganisha Wizara na Taasisi za Serikali. Hii itajumuisha pia kuunda Tovuti Kuu ya Serikali na kuboresha mfumo wa kiusalama wa mtandao wa Serikali; na (*Makofi*)

(g) Kuendelea kutoa huduma kwa viongozi wastaafu wa Kitaifa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma. Katika mwaka 2008/2009, Chuo cha Utumishi wa Umma, kimepanga kuendelea na mikakati ya kujiimarisha katika kutoa mafunzo yanayochangia kuleta ufanisi katika Utumishi wa Umma. Hivyo, jitihada zitafanywa kuwapeleka watumishi katika Mafunzo ya Uzamili pamoja na kuajiri Watumishi Waelekezi ili kuongeza idadi ya wataalamu waliopo. Pia chuo kitafanya ukarabati wa majengo yaliyopatikana katika Mji wa Mtwara, ili kuwezesha ufunguzi wa tawi la Chuo mjini hapo. Aidha, chuo kitaendelea na mpango wake wa ushirikiano na asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kupanua uzoefu na kutoa mafunzo ya kisasa na yenye gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo kwa Mtandao (*TGDLC*). Katika mwaka wa fedha 2008/2009, pamoja na kuendelea kuwawezesha Watanzania kushiriki katika midahalo mbalimbali na mafunzo, kituo kitafanya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ukarabati wa Ofisi za kituo;

(b) Kukuza na kuboresha uwezo wa wafanyakazi wa kituo ili kukidhi ongezeko la wateja na mabadiliko ya haraka ya teknolojia;

(c) Kukuza mtandao wa kituo ili kuwafikia wahitaji walioko Mikoani kwa kuanza utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa ya upembuzi yakinifu juu ya kuanzisha vituo shirikishi vya elimu mtandao Mkoani kwa kuanzia na Mkoa ya Arusha, Dodoma, Morogoro na Mwanza;

(d) Kuongeza ushirikiano na asasi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ili kuendelea kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia ya kisasa na wa gharama nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ambacho ni chombo chenye majukumu ya kukuza na kuimarisha maadili mema miongoni mwa Viongozi wa Umma, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kuchunguza malalamiko dhidi ya Viongozi mbalimbali watakaotuhumiwa kukiuka maadili ya Viongozi wa umma na kuchukua hatua;
- (b) Kupokea na kuhakiki Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma 7,447 waliopo na watakaoteuliwa na hatimaye kuingiza rasilimali na madeni yao kwenye Daftari la Mali na Madeni;
- (c) Kuhakiki Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma 400, kwa kutumia njia ya uwiano kwa kila kada ili kubaini ukweli na usahihi wake;
- (d) Kutoa elimu ya Maadili ya Viongozi kwa Viongozi na wananchi kwa njia ya radio, magazeti, televisheni, semina na machapisho mbalimbali pamoja na kushiriki kwenye maonyesho ya Kitaifa kama vile Wiki ya Utumishi wa Umma, Sabasaba na Nanenane; (*Makofi*)
- (e) Kuajiri watumishi wapya kujaza nafasi za wazi 30 zilizopo Makao Makuu na Ofisi za Kanda, ili kufikia idadi ya Watumishi 145 walioidhinishwa katika Ikama ya Sekretarieti;
- (f) Kuwapatia watumishi wa Sekretarieti, mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili kuboresha utendaji wao wa kazi. Jumla ya watumishi 50 wa kada mbalimbali walipatiwa mafunzo.
- (g) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za mfumo wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi;
- (h) Kukamilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati na mrefu katika kuimarisha na kuinua viwango vya maadili bora miongoni mwa Viongozi wa Umma; na
- (i) Kukamilisha na kuchapisha Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma kwa lugha nyepesi ili Viongozi na wananchi, waweze kuzielewa na kuzitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango. Kama wote tunavyokumbuka, wakati akitangaza mabadiliko ya Muundo wa Serikali, mwezi Februari mwaka huu, Mheshimiwa Rais alitangaza kuundwa kwa Tume ya Mipango kama chombo mahususi (*Think-Tank*) cha kuchambua Sera na Mikakati ya kiuchumi kwa upeo wa muda wa kati na muda mrefu na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii kwa lengo la kuimarisha mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Mheshimiwa Rais aliamishia katika Wizara mpya ya Fedha na Uchumi pamoja na vyombo vingine shughuli zote za upeo wa muda mfupi na za kiutendaji zilizokuwa zikifanywa na iliyokuwa Wizara ya Mipango,

Uchumi na Uwezesaji. Mgawanyo huo wa majukumu ulifafanuliwa kikamilifu katika tangazo la Serikali (*Government Notice*), Na. 20 ya tarehe 13/2/2008.

Mheshimiwa Spika, dhamira hiyo ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na chombo cha kuangalia mbali, ilifuatiwa na hatua za kubuni muundo wa chombo hicho. Muundo uliobuniwa utaunganisha nguvu za wataalamu wachache watakaokuwa katika ajira ya Tume hiyo, pamoja na za wataalamu katika taasisi za kitafiti za hapa nchini na hata nje ya nchi ili kufanya uchambuzi wa kina juu ya masuala na changamoto mbalimbali za kiuchumi na za kijamii zinazoikabili nchi yetu.

Aidha, muundo na mfumo wa kazi za Tume mpya ya Mipango inayoundwa, utakuwa tofauti sana na ule wa Tume ya zamani yaani ya 1989 hadi 1995, ukiwa hasa na lengo la kuimarisha uchambuzi na mawasiliano ya kitaalamu kabla ya masuala husika hayajafikishwa katika ngazi za maamuzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Tume itafanya kazi kwa kushirikiana na watu na makundi mbalimbali ya kijamii ambao watakuwa na ujuzi na uzoefu maalum katika mambo yatakayokuwa yanafanyiwa uchambuzi. Tume inatazamiwa kuwa Kituo Rejea cha Sera na Ushauri wa Kiuchumi na kijamii kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili ifanye kazi katika mtazamo nilioueleza, Muundo wa Tume ya Mipango umegawanyika katika maeneo matano ya kitaalamu nayo ni:-

Eneo la kwanza, litajikita katika masuala ya uchumi jumla (*macro-economy*);

Eneo la pili, litajikita katika masuala ya sekta za uzalishajimali zikiwemo kilimo, viwanda, Madini, mifugo, uvuvi, misitu na kadhalika;

Eneo la tatu, litajikita katika sekta ya za miundombinu na huduma zikiwemo barabara, reli, viwanja vya ndege, mawasiliano, Nishati, maji, utalii, biashara, ardhi na kadhalika;

Eneo la nne, litajikita katika sekta za huduma za jamii na masuala ya idadi ya watu zikiwemo elimu, afya, mazingira, ajira, habari, michezo na kadhalika; na

Eneo la tano, litajikita katika biashara na ushirikiano wa kiuchumi kimataifa.

Aidha, maeneo hayo kitaalamu yatasaidiwa na Idara mbili na vitengo sita vitakavyoshughulikia mambo mbalimbali ya huduma na uendesaji. (*Tazama Chati Na.1*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/2009, utakuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango katika mwelekeo wa *think-tank*.

Msukumo utawekwa katika kuainisha masuala muhimu ya kiuchumi na kijamii ambayo yanahitaji kufanyiwa uchambuzi wa kina kwa lengo la kutoa ushauri kwa Seriklai juu ya hatua muhimu za kuchukuliwa kujibu changamoto mbalimbali zinazokabili Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, tumepanga kuandaa semina maalumu ambapo Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kutafakari kwa kina juu ya maudhui ya Tume ya Mipango na kutoa ushauri utakaoisaidia kutimiza madhumuni ya kuundwa kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

- (a) Kushughulikia rufaa za watumishi dhidi ya maamuzi ya Waajiri na Mamkala za Nidhamu na kuboresha miongozo iliyopo inahusu masuala ya Utumishi wa Umma;
- (b) Kufanya ukaguzi kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozi na taratibu kwenye Mamlaka za Ajira na Nidhamu;
- (c) Kufanya ukaguzi wa utendaji kazi wa watumishi kwenye Mamlaka za Ajira na Nidhamu;
- (d) Kufuatilia ukamilishaji wa Taratibu za Uendeshaji katika utumishi wa Serikali za Mitaa, Utumishi wa Afya na Utumishi wa Walimu;
- (e) Kuendelea kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya radio na kuchapisha makala 52 za magazeti kwa lengo la kuwaelimisha watumishi wa umme, waajiri na wadau wote kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma;
- (f) Kuendelea kugharamia watumishi 101 ambao wako kwenye mafunzo;
- (g) Kushauri na kusaidia Mamlaka za Ajira kuhusu ajira, kuthibitishwa kazini na kupandishwa vyeo;
- (h) Kuendelea kushiriki katika mchakato wa uimarishaji wa ushirikiano baina ya Tume ya Utumishi wa Umma za Afrika Mashariki; na

- (i) Kufanya utafiti kuhusu utendaji wa Tume katika utoaji wa huduma kulingana na matarajio ya wadau.

Mheshimiwa Spika, Majumuisho. Mafaniko niliyoyaeleza katika hotuba hii, yemachangiwa na wengi na kwa namna mbalimbali. Aidha, nachukua fursa hii kuzishukuru nchi na mashirika yafuatayo:-

Australia, China, India, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Malyasia, Misri, New Zealand, Norway, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubeligiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Jumuiya ya Madola, Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Dunia, ACBF, CIDA –Canada, DANIDA, DFID, JICA, NORAD, OPEC, SIDA – Sweeden, UNDP, UNIDO na USAID.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili nchi yetu iwe na uchumi na imani endelevu, tunahitaji Utawala Bora ambapo Sera, Sheria, Taratibu na Kanuni bora, zinatumiwa katika kusimamia uchumi na uendeshaji wa shughuli za umma. Taasisi zilizo katika Ofisi ya Rais – Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tume ya Mipango na Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ndizo zimepewa dhamana ya kuratibu utekelezaji wa majukumu hayo. Hivyo, mipango yetu ya mwaka 2008/2009, imezingatia na inalenga kufanikisha majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza majukumu yetu na shughuli tulizozopanga kuzitekeleza katika mwaka wa fedha 2008/2009, naomba niwasilishe rasmi mapendekeo yetu ya maombiwa fedha kwa mwaka 2008/2009 kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

- (i) Matumizi ya Kawaida Sh. 6,211,007,000/=
- (ii) Jumla Sh. 6,211,007,000/=

(b) Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

- (i) Matumizi ya kawaida Sh.41,090,604,000/=
- (ii) Mpango wa Maendeleo Sh.59,744,657,600/=
- (iii) Jumla Sh. 200,835,261,600/=

(c) Fungu 32: Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

- (i) Matumizi ya Kawaida Sh.12,482,721,000/=
- (ii) Mpango wa Maendeleo Sh.14,257,871,000/=
- (iii) Jumla Sh. 26,740,592,000/=

(d) Fungu 33: Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

- (i) Matumizi ya Kawaida Sh.1,746,831,000/=
- (ii) Mpango wa Maendeleo Sh.210,000,000/=
- (iii) Jumla Sh.1,956,831,000/=

(e) Fungu 66: Tume ya Mipango

- (i) Matumizi ya Kawaida Sh.10,138,884,400/=
- (ii) Mpango wa Maendeleo Sh.1,218,163,000/=
- (iii) Jumla Sh.11,357,074,400/=

(f) Fungu 94: Tume ya Utumishi wa Umma

- (i) Matumizi ya Kawaida Sh. 6,895,749,000/=
- (ii) Mpango wa Maendeleo Sh.104,000,000/=
- (iii) Jumla Sh. 6,999,749,000/=

Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja Ilitolewa Iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nitamuita sasa Mheshimiwa Mwenyekiti au Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Lwanji, karibu!

MHE. JOHN P. LWANJI – (K.n.y. MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, nawasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma), kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu, inahusisha Mafungu 20 na 30. Aidha, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, inahusisha Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma na Fungu 66 – Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam, tarehe 30 Mei, 2008, kushughulikia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi

ya Rais. Kama nilivyoeleza hapo juu, katika kikao chake hicho, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu yaliyofanywa na Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha uliopita na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2008/2009, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Sophia Simba, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) na Mheshimiwa Hawa Ghasia, (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nianze na Ofisi ya Rais (Ikulu).

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008. Katika Mwaka wa Fedha 2007/2008, Ofisi ya Rais, Ikulu, ilitengewa jumla ya Sh.121,250,754,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.69,590,206,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kiasi hicho cha fedha kilitumika kutekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri kwa Mheshimiwa Rais. Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaokwisha, miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais kuhusu masuala mbalimbali ya kitaifa katika sekta za uchumi, siasa, sheria, diplomasia, n.k.

(b) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Ofisi hiyo pia ilitekeleza miradi kadhaa ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, tarehe 17-19 Januari, 2007, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa kushirikiana na MKURABITA, zilifanya ziara ya siku mbili katika Wilaya za Handeni na Bagamoyo na kujionea miradi ya majaribio inayofanywa na MKURABITA. Katika ziara hizo, Kamati zilijionea na kujifunza mikakati mbalimbali inayofanywa na MKURABITA katika kurasimisha rasilimali za wananchi zikiwemo ardhi za wanavijiji ili hatimaye waweze kuzitumia rasilimali hizo kama dhamana za kukopa fedha benki na kujiendeleza kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpango huu ni mzuri na ukifanikiwa utaleta maendeleo kwa wananchi waliopo mijini na vijijini. Hata hivyo, kutokana na mafunzo iliyoyapata katika ziara hiyo, Kamati inashauri kuwa elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi, ikiwahusisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ili wafahamu taratibu mbalimbali za kisheria za umilikaji wa rasilimali zao. Kwa kufanya hivyo, Kamati inaamini kuwa, wale watakaokuwa na ufahamu wa kutosha watawaelimisha na kuwasaidia wenzao kumiliki rasilimali zao ikizingatiwa kuwa baadhi ya wadau katika zoezi hilo ni wazee na wengine hawana elimu ya kutosha.

Aidha, kutokana na kuwepo kwa vikwazo vya kisheria katika zoezi la kurasimisha mali za wananchi, Kamati inashauri kwamba MKURABITA iharakishe mchakato wa

kushughulikia marekebisho ya Sheria za Ardhi, Biashara na Sheria zote zinazoleta vikwazo kwenye mpango huo, ili zifanyiwe kazi na vyombo vinahusika na hatimaye kuwasilishwa Bungeni.

(c) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Katika kipindi kilichopita, pia Ofisi ya Rais (Ikulu), ilitekeleza miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), ambayo kwa bahati nzuri mwaka 2006 na 2007, Kamati yangu kwa kushirikiana na *TASAF*, ilipata fursa ya kukagua miradi hiyo katika Visiwa vya Pemba na Unguja na Mikoja ya Tanga, Iringa, Ruvuma, Mwanza, Shinyanga na Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TASAF*, kwa kuwa wananchi wengi bado hawaelewi mchakato wa *TASAF II*, Kamati inashauri kuwa Serikali ichukue hatua za ziada kuwaelimisha juu ya mchakato huo. Aidha, wananchi waelimishwe kuwa fedha zinazotolewa na *TASAF*, siyo za mikopo ya wajasiriamali bali ni kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Kamati inashauri kuwa Serikali iwahamasishe wananchi kushiriki kikamilifu katika miradi ya *TASAF* kwa kujitolea kuchangia asilimia ishirini kwa wakati unaotakiwa kama masharti ya ufadhili wa *TASAF* yanavyohitaji ili watekeleze miradi hiyo kwa ufanisi.

(d) Mikakati ya kuzuia na kupambana na rushwa. Shughuli nyingine zilizotekelezwa zinahusu mikakati mbalimbali iliyowekwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kuhusu maadili na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Na.11 ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, litakumbuka kuwa mbali ya Sheria Na.11 ya Mwaka 2007, katika Mkutano wa Saba, Bunge lilipitisha Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali (Na.2) ya Mwaka 2007 iliyofanya marekebisho katika Sheria ya Udhhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006 (*The Anti-Money Laundering Act, 2006*), Sheria ya Ushirikiano na Nchi nyingine katika Kudhibiti Vitendo vya Jinai, Sura ya 254 (*The Mutual Assistance in Criminal Matters, Cap.254*), Sheria ya Udhhibiti wa Mali inayotokana na Uhalifu, Sura ya 256 (*The Proceeds of Crime Act, 256*) na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sheria zote hizi zilitungwa katika kuhakikisha kuwa Taifa linadhhibiti vitendo viovu na kuhakikisha kuwa nchi inaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanyika za kupambana na kuzuia rushwa, inaonekana kuwa wananchi bado wanalalamika juu ya kuwepo kwa vitendo vya rushwa katika maeneo kadhaa. Kamati inashauri kuwa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, iendelee kufuatilia maeneo yanayolalamikiwa na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009, maombi ya fedha, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, Kamati yangu imeombwa kuipitishia Ofisi ya Rais, Ikulu, jumla ya Sh. 6,211,007,000/=, kwa Fungu 20 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.200,835,261,600/= kwa ajili ya Fungu 30, kati ya fedha hizo Sh. 141,090,604,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 59,744,657,600 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho, ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuendeleza shughuli zilizofanyika mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuelezea Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 32, liliidhinishiwa jumla ya Sh.37,482,760,300/=, kati ya fedha hizo Sh.9,857,913,000/= zikiwa ni za Matumizi ya Kawaida na Sh.27,624,847,300/= kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Aidha, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 33 liliidhinishiwa Sh.919,240,000/= na Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94, Sh.7,818,121,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizofanyika:-

(a) Miundo, miongozo, mikutano na mafunzo. Katika kipindi hicho, baadhi ya shughuli zilizofanyika zilihusu kuandaa miundo na orodha za kazi za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali. Vilevile kutayarisha miongozo ya mikataba katika sekta ya utumishi wa umma ukiwemo Mkataba wa Huduma kwa Mteja na Mpango Mkakati na Bajeti.

Shughuli nyingine zilikuwa kuandaa mikutano ya watendaji wakuu wa Wizara, Mikoa, Idara Zinazojitegemea ili kuwajengea uwezo, ikiwemo mikutano ya kujadili utendaji kazi wa utumishi wa umma, kuandaa mafunzo kwa viongozi wakuu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha sekta ya utumishi wa umma. Hata hivyo, kuhusu miundo ya utumishi, Kamati inashauri kuwa Serikali iifanyie tathmini miundo ya Utumishi ya Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea kuona kama inakidhi haja zilizokusudiwa.

Kamati inaona kwamba upo uwezekano wa kuwepo kada za watumishi ambazo pengine ziliunganishwa katika muundo mmoja kwa nia njema, lakini katika utendaji kazi watumishi wanaohusika huenda hawaufurahii muundo huo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoshauri kuhusu suala la upungufu wa watumishi wakati nikiwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, Kamati bado inasisitiza kuwa jitihada zaidi ziendelee kufanyika kwa ajili ya kufungua milango ya ajira ili kutosheleza mahitaji ya watumishi Mikoani hususan katika sekta ya afya na elimu.

Pamoja na hayo, Serikali ihakikishe kuwa inatekeleza makubaliano yote yaliyofikiwa kati yake na vyombo vya wafanyakazi hususan kuhusu mishahara na marupurupu mengine.

(b) Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kazi zilizofanyika ni pamoja na kushughulikia Tamko la Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma, kwa kupokea fomu na kuhakiki mali zao, kuchunguza malalamiko yanayowahusu viongozi, uimarishaji wa Ofisi za Kanda, kutoa elimu ya maadili kwa wananchi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza majukumu hayo, Kamati inashauri kuwa kuwe na mawasiliano ya mara kwa mara kati ya Ofisi za Kanda na Makao Makuu wakati wa kupokea na kuhakiki fomu za Tamko la Mali na Madeni kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za watumishi wanaohusika. Kwa kufanya hivyo, Kamati inaamini kuwa kutaondoa usumbufu usio wa lazima kama uliowapata baadhi ya watumishi walioandikiwa barua wakidaiwa kuwa hawajareshesha fomu katika Kanda zao wakati walikwisharejesha Makao Makuu.

Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, Sekretarieti ya Maadili iendelee kuwakumbusha watumishi wote waliotajwa kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kujaza fomu zao na kuzirejesha kwa wakati.

(c) Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa mwaka wa fedha uliopita, Tume ya Utumishi wa Umma, ilishughulikia mambo mbalimbali yaliyowahusu watumishi, ikiwa ni pamoja na kushughulikia mashauri ya nidhamu, kupokea na kushughulikia malalamiko, kushughulikia stahili mbalimbali za Walimu pamoja na kuwabadilisha vyeo, kuwasajili, kuwathibitisha kazini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Tume kwa kazi inazozifanya hususan kushughulikia masuala ya Walimu, kama vile kushughulikia na kuidhinisha kupandishwa vyeo walimu 43,475.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Kamati inashauri kuwa Tume iendelee kukusanya data zaidi na kushughulikia watumishi wa sekta nyingine.

(d) Tume ya Mipango ni chombo kipya kilichoundwa kufuatia kuundwa kwa Baraza la Pili la Mawaziri la Serikali ya Awamu ya Nne, ikiwa chini ya Ofisi ya Rais. Tume ya Mipango inahusisha mtandao wa wataalam wenye ujuzi na uwezo wa kutosha katika nyanja mbalimbali na wenye mamlaka ya kisera katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Tume imejiwekea malengo ya kushughulikia masuala ya uchumi, kuimarisha uchambuzi, kufanya tathmini na mapitio ya sera, kuandaa mipango na mikakati ya kisekta, kuboresha huduma za kupambana na VVU/UKIMWI na kadhalika. Kwa kuzingatia nafasi muhimu ya Tume hiyo katika sekta mbalimbali za jamii na kulingana na uchanga wake, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Tume ya Mipango ijengewe uwezo na kuchota ujuzi na uzoefu wa utendaji kazi wa Tume nyingine inazofanana nazo ili iweze kushughulikia vema masuala mtambuka;

(ii) Tume ya Mipango kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika iangalie namna itakavyoishauri Serikali kupunguza gharama za matumizi ya mafuta ya magari ya Serikali ili kiasi kingine cha fedha kiweze kutumika kwenye miradi ya maendeleo; na

(iii) Tume ishirikiane na Wizara ya Fedha kuja na mkakati wa Mgawanyo wa Rasilimali kwenye mikoa ambayo ipo nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Mbali ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na Mafungu yake, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, pia Kamati ilifahamishwa juu ya kazi mbalimbali zilizopangwa kufanywa na Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Hatimaye, Kamati iliombwa ipitishe jumla ya fedha zinazoombwa na Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) na Mafungu yake yote kwa mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi hayo, Kamati ilipitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha taarifa hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Pili, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Hawa Abdurahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa wakati wote Kamati iliposhughulikia makadirio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma). Ujuzi na uzoefu wao katika nyanja mbalimbali za sekta ya utumishi wa umma, umefanikisha sana kutoa ushauri ulioboresha makadirio ya Ofisi hii. Naomba sasa niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti na Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe ni Mheshimiwa Yusuf R. Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Abdubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangaro. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuwashukuru, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka, Ramadhani Abdallah, Elihaika Mtui, kwa kuhudumia na kuratibu shughuli zote za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, jumla ya Sh. 254,100,488,000/= kati ya fedha hizo Sh.178,565,796,400/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.75,543,691,600/= kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo kama alivyowasilisha mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lwanji, umewasilisha taarifa ya Kamati vizuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mwakilishi wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala haya ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, nimeshangazwa kwamba walioomba kuongea ni watano tu, sijui mmeanza kuchoka? Wizara hii ni siku mbili, hadi kesho, basi huo ni wito tu kwamba wale ambao wanapenda kuchangia katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, bado nafasi ipo.

Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naona anakuja Mheshimiwa Grace Kiwelu, karibu sana. (*Makofi*)

MHE. GRACE S. KIWELU – MSEMaji WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zangu za dhati, kwa kunipa fursa hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti

ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi pamoja na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7) toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo kujadili mambo muhimu kwa maslahi ya umma kwa Watanzania na kwa mema yote ambayo amekuwa akitujaalia. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba majadiliano yetu yataweka mbele maslahi ya umma. Mwenyezi Mungu atusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kwa nafasi ya kipekee kabisa, kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Ofisi ya Rais, Utawala Bora kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha uandaaji wa hotuba hii, kwani ni Msemaji Mkuu katika Wizara zinazojumuishwa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa pongezi za dhati kwa viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwa kutoa miongozo sahihi kwa mujibu wa kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inatambua kuwa Utumishi wa Umma ni nguzo muhimu ya ukuaji wa Taifa lolote lile duniani. Watumishi wa umma, hutoa mchango mkubwa katika kulinda na kujenga heshima ya nchi, kudumisha usalama na kuiwezesha Serikali kufanya shughuli zake kwa njia nzuri na kukuza kipato cha Taifa na hatimaye kwa mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inatambua umuhimu wa Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama sehemu muhimu sana katika kuimarisha utawala bora kwa uendeshaji wa shughuli za Serikali, kuweka mfumo wa uendeshaji wa Serikali unaoleta tija na ufanisi, kujenga uwezo wa watumishi wa umma na kuboresha maslahi ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa hilo, ni muhimu sana idara hii iangaliwe kwa umakini kwa sababu watumishi wa umma ni moja ya kiini cha maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inayaona mengi ambayo kimsingi yamekuwa yakidhoofisha suala zima la utendaji na uwajibikaji wa watumishi wa umma. Mambo haya yanatokana na kutokuwepo kwa umakini na ufuatiliaji thabiti ambao umepelekea kuporomoka kwa maadili na uwajibikaji wa watumishi wa umma, maisha duni yanayotokana na vipato duni, ubinafsi, ufisadi na urasimu na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, taratibu za ajira ya wataalam wa kigeni kwenye utumishi wa umma limeendelea kuwa tatizo kwani hakuna mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa pale ambapo wataalam hao wanaajiriwa panakuwa na mpango madhubuti wa kuwaendeleza wataalamu Wazalendo kama njia ya kupunguza utegemezi wa wataalamu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kama pangukuwa na mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa wataalam wetu wanaendelezwa na baada ya kuendelezwa pawepo na mpango mkakati wa kuhakikisha kuwa Serikali inajenga mazingira bora ili wataalam hao waweze kuja na kuendelea kufanya kazi hapa nchini badala ya kwenda kufanya kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la mishahara kwa watumishi wa umma. Maboresho ya maslahi ya watumishi wa umma ni jukumu muhimu sana la Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kwa kutambua hilo, Serikali ya Awamu ya Nne, haikubaki nyuma na ndio maana ikaahidi maisha bora kwa kila Mtanzania. Tumaini la kila mtumishi lilikuwa ni nyongeza ya mishahara kulingana na kiwango cha kupanda kwa hali ya maisha kiujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa tathmini ya Kambi ya Upinzani, kima cha chini cha mishahara kimepanda na kuwa Sh.100,000/= tu kwa watumishi wa Serikali. Kutokana na kupanda kwa hali ya maisha, mkate sasa ni karibu Sh. 1,000/=, kilo ya mchele ni zaidi ya Sh. 1,200/=, kilo ya nyama ni zaidi ya Sh. 2,500/= katika maeneo mengi na kilo ya sukari ni zaidi ya Sh. 1,200/= vilevile. Hali hii ya maisha haijajumlisha nauli zilizopanda, gharama za matibabu katika hospitali na zahanati nyingi zikiwemo za Serikali. Kwa hali hii, kima cha chini cha Sh.100,000/=, kwa hakika ni dhahira kwa watumishi na wafanyakazi wetu wa sekta ya umma. Isitoshe Serikali haijasema chochote kuhusu kima cha chini katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, kupitia kwa Hotuba ya Msemaji wake Mkuu kwa Wizara ya Fedha ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ilipendekeza kwa mara ya pili mfululizo kuwa Kima cha chini kiwe Sh. 250,000/=. Kiwango hiki kinawezekana kabisa kama ilivyoonyeshwa katika bajeti mbadala ya fedha mwaka 2007/2008 kama ilivyowasilishwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wakati alipowasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa mapato ya ndani na ukuaji wa makusanyo ya ndani, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa kiwango cha chini cha mishahara wa wafanyakazi wa umma kiwe Sh. 250,000/= kwa mwezi, kwa ngazi nyingine mishahara ungepanda kwa asilimia ambayo italetwa uwiano baina ya kipato cha chini na cha juu. Kiwango hiki hakitanzwa kodi ili kuweza kumfanya mtumishi wa ngazi ya chini aweze kumudu gharama za maisha ambazo zinapanda kila siku. Ni dhahira kabisa kuwa Serikali kwa kulipa wafanyakazi wake kima hiki, itawaweka katika hali ya kukwepa rushwa na ubadhirifu, kitawawezesha watumishi hao kujiweka akiba wakati wa kustaafu.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inalenga kumwezesha mtumishi wa umma kuweza kuhimili hali ya ugumu wa maisha na hasa kutokana na kasi ya kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali. Wastani wa kasi ya upandaji bei ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2006. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi April 2008, kasi ya upandaji bei ilikuwa asilimia 9.7, upandaji huu umemwathiri sana mtumishi wa umma kama ilivyo kwa wananchi wengine kwa ujumla wake na ndio maana tunaitaka Serikali ipandishe kima cha chini cha mshahara hadi kufikia Sh. 250,000/= kwa mwezi ili kuweza kuwanusuru watumishi wetu na hali ngumu za maisha wanayokumbana nayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, Kambi ya Upinzani iliitaka Serikali kuiweka hadharani Ripoti ya Tume ya Kurekebisha Mishahara ya Watumishi wa Umma ambayo ilikuwa chini ya Uenyekiti wa Ndg. Deogratias Ntukamazima, ili Wabunge na wawakilishi wa wafanyakazi, waweze kuona kama yaliyopendekezwa yanalingana na mapendekezo ya maoni ya Vyama vyao vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa ripoti hiyo haijaweka hadharani na hata Wabunge hatujapatiwa taarifa ya aina yeyote ile ama kupewa nakala ya taarifa hiyo. Hivi Bunge linategemewa vipi litimize majukumu yake ya kusimamia Serikali kama kila mwaka tutakuwa tunaendelea kupata taarifa kwa kuichokonoa Serikali? Fedha za Watanzania zilitumika katika mchakato mzima wa utendaji wa Tume hiyo na hivyo ni lazima Wabunge na Watanzania wajulishwe matokeo ya kazi iliyofanywa na fedha zao. Taarifa hiyo siyo ya Serikali, ni ya Taifa na hivyo haina sababu ya kuwa Taarifa ya Siri kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza kuwa huu ndio uwazi na uwajibikaji ambao Ofisi hii inauonyesha na kuwa ndio mfano wa kuigwa na Wizara nyingine?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa zinachukuliwa hatua madhubuti ili kukabiliana na janga la maambukizo ya UKIMWI kwa watumishi wa umma kwa kuhakikisha kuwa watumishi hawa wanapata mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kuweza kujikinga na maambukizi hayo. Hili tunalisema hapa kwani ukisoma kwenye kitabu cha mpango wa maendeleo wa Serikali mwaka 2008/2009, Serikali haikuweka mpango maalum wa kukabiliana na janga hili hasa kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Serikali kuweka mkakati bayana wa kukabiliana na janga hili kwani likiachwa bila kutiliwa mkazo hata kama kiwango cha maambukizi kinaonekana kupungua bado litaweza kufanya jitihada mbalimbali zilizopo kutokuweza kuzaa matunda yanayotegemewa.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya utumishi wa umma ni pamoja na kusimamia na kuweka miongozo ambayo itasaidia kuinua kiwango cha utendaji katika taasisi za

Utumishi wa Umma na kuifanya kuwa kila huduma itakayotolewa kufananishwa na bidhaa bora katika soko.

Mheshimiwa Spika, kwa dhana hii basi, kila shughuli itakayofanywa na taasisi ya kutoa huduma kwa umma ambayo haitamlenga moja kwa moja mteja ambaye ni mwananchi basi ihesabike kama upotevu wa raslimali ya nchi (*waste of resources*). Aidha, hii ihesabike kuwa ni moja ya uifisadi unaofanyika kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaamini kabisa kuwa pale ambapo sekta ya utumishi wa umma itaanza kuelewa dhana ya biashara isemayo kuwa ‘mteja ni mfalme’ na katika kadhia nzima ya utumishi wa umma mteja si mwingine bali ni mwananchi anayetakiwa kupata huduma, basi hapo tutakuwa tumefanikiwa kubadili *mindset* kwa watumishi hao na yale matatizo yote na malalamiko ya huduma mbovu, kuchelewesha majibu, kuwapiga danadana ya njoo kesho yatakuwa yamepatiwa suluhisho.

Mheshimiwa Spika, utumishi wa umma uliosahihi na unamchukulia mteja ambaye ni mwananchi kama ni mfalme, ni ule ambao utatoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa umma. Kutoa majibu kwa wakati kulingana na masuala yanayoulizwa na muulizaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha uongozi, Serikali imeshindwa na inaendelea kushindwa kuwapatia majibu wananchi (wateja) ambao wanaandika barua zao kwa misingi ya kupata ufafanuzi kulingana na masuala mbalimbali. Jambo hili kwa ujumla wake linadhalilisha nchi inayojiita kuwa inafuata sheria na utawala bora. Mfano mzuri ni Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Utawala Bora, alipoandika barua kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, kuhusu malalamiko ya wavuvi katika Wilaya ya Mafia, lakini hadi leo hii, hajapata majibu ya barua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza, Kama Waziri Kivuli wa Utawala Bora anashindwa kujibiwa barua zake, je, hali ikoje kwa wananchi wa kawaida?

Mheshimiwa Spika, moja ya kazi za Tume ya Utumishi wa Umma, ni kumshauri Rais kupitia Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuhusu utekelezaji wa Mamlaka ya Rais Kikatiba mintarafu Ibara ya 36 ya Katiba na kuhusu ujazaji wa nafasi zilizowazi katika utumishi wa umma, kadri Rais atakavyoona inafaa. Pia kuwezesha uteuzi wa nafasi mbalimbali kutoka mamlaka mbalimbali za ajira.

Mheshimiwa Spika, nafasi za uteuzi zinazoongelewa hapa ni zile za kada ya juu katika utumishi wa umma. Nafasi hizi ndizo zile zinazotakiwa kutoa maamuzi ya mwelekeo wa nchi yetu katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, udhaifu mkubwa katika utumishi wa umma wa kutokutaka kubadilika na kuwa na mtazamo wa kuongeza tija na kuweka mbele maslahi ya nchi, chanzo chake ni uteuzi usioangalia *records* na sifa (*vetting*) za utendaji wakati wa ujazaji wa nafasi mbalimbali za utumishi. Mwisho wa siku, ndio hayo yanayosabisha watendaji kushindwa kutoa maamuzi yaliyo katika wigo wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini sasa kuwa uteuzi mwingi anaoufanya Rais unatokana na ushauri mbaya na upendeleo ambao hautilii maanani maslahi ya nchi anaopewa Rais na Tume hii katika kujaza nafasi zilizowazi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, ukisoma maelezo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2008/2009, katika taarifa ya Kamati ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala, ukurasa wa saba wa taarifa hiyo, kwenye makadirio yaliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kiasi cha Sh.4,183,205,000/= ziliidhinishwa, ila mpaka kufikia mwezi April 2008 kwenye fungu la mishahara fedha zilizotolewa zilikuwa kiasi cha Sh.2,019,527,454/=, hiki ni kiasi cha 48.3% tu.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni kuwa, Wizara iliomba pesa nyingi kupita kiasi na sababu kubwa ni kuwa Idara hii haijui idadi ya watumishi wake, kama hali ni hii kwa Wizara hii, je, hali itakuwaje kwa Wizara nyingine? Nini kilitokea kiasi kwamba mishahara iliyotumika ilikuwa ni kiasi cha 48.3% tu.

Mheshimiwa Spika, isitoshe kumekuwa na taarifa za watumishi hewa katika Wizara mbalimbali hasa Wizara ya Elimu, kinyume na Naibu Waziri wa Fedha alivyojibu ndani ya Bunge hili kuwa watumishi wote wamesajiliwa kupitia waajiri wao na hivyo hakuna haja ya *TIN number* kwa watumishi walipa kodi, je, si kweli kuwa Serikali bado haijakuwa na majibu sahihi juu ya wafanyakazi hewa? Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri atupe majibu ya kina juu ya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bajeti ya Serikali 2008/2009, Serikali inaomba kupewa fedha kwenye fungu la matumizi maalum, imeomba kiasi cha fedha kwa ajili ya kulipia mishahara ya nyuma (*arrears*), hizi ni fedha za kulipia nini kama kipindi cha mwaka 2007/2008, Wizara haikutumia kiasi kilichoidhinishwa? Tunamtaka Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kina juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia, inataka kufahamu Kima cha chini kwa mishahara ya Serikali hasa ni kiasi gani au ndiyo hiyo Sh.100,000 tuliyoisema? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nguzo ya tatu ya MKUKUTA, ni kuhakisha kuwa nchi yetu ina utawala bora unaofuata sheria. Vita dhidi ya rushwa, ni msingi muhimu wa kujenga utawala bora. Pia ni msingi muhimu kwa Wahisani kuendelea kutupatia misaada yao. Tuhuma nzito za rushwa ikiwemo ile ya *Richmond* na malipo ya akaunti ya *EPA*, Benki Kuu (*BOT*), hazijachukuliwa hatua za kuwafikisha wahusika Mahakamani, si kipimo kizuri kwamba nchi yetu ina utawala bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi, Watanzania wanataka kuona sheria zinafuatwa bila ubaguzi, ambapo walalahoi, mara

wanapotuhumiwa hukamatwa, hupelekwa Rumande na kupelekwa Mahakani lakini kwa vigogo wenye kutuhumiwa kwa mabilioni, mambo ni tofauti kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye wizi wa fedha za umma uliofanyika kupitia *account* ya EPA, umeifanya nchi yetu kujikuta inajenga matabaka mawili kwenye kuwafikisha wahalifu Mahakamani na au kuwachukulia sheria vigogo waliohusika, kwani Serikali imejikuta ikikaa na wahalifu na kuwabembeleza kurudisha fedha walizoibia Taifa huku wezi wa kuku wakipelekwa Mahakamani na sheria kutumika juu yao, huu sio mfano wa utawala bora hata kidogo kwani nchi inagawanywa kati ya walionacho na wasiokuwa nacho na hii ni hatari kwa ustawi wa Taifa na dhana nzima ya utawala bora kwa ujumla wake. Hata kama hoja ni kurudisha fedha kabla ya kuwafunga, lakini watuhumiwa hao wote wana mali zinazoweza kuchukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivyo hakuna maelezo yoyote ya kwa nini taratibu za kawaida za sheria za nchi zisifuatwe hasa baada ya hatua hizo kupendekezwa na Wakaguzi wa *Ernst and Young*, kama ilivyoelezwa kwa vielelezo katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI Mheshimiwa Dr. Slaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Waziri Mkuu juzi, lazima tukubali kuwa kifo cha Gavana wa zamani wa Benki Kuu, kimegubikwa na usiri hasa baada ya Msemaji wa Ikulu kueleza kuwa Serikali haimtafuti Gavana wa zamani Daud Balali lakini ikimtaka itampata kwani Serikali ina mkono mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haikupita muda baada ya kauli hii ya Msemaji wa Ikulu, kwani muda mfupi vyombo vya habari viliripoti kuwa Gavana Balali amefariki. Taarifa rasmi ya Serikali kuhusu kufariki kwake, imechelewa kutolewa kiasi ambacho wananchi wengi hawaamini kama kweli Gavana Balali amefariki. Kwa Serikali kutokuwa wazi kuhusu kuumwa, kutibiwa na kufariki kwa Gavana Balali, kumejenga hisia kuwa kuna mambo yanayohusiana na ufisadi ndani ya Benki Kuu, yanafichwa ili kuwalinda viongozi wa Awamu ya Tatu na ya Nne waliyohusika kuidhinisha na kufaidi matunda ya ufisadi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kupata maelezo ya kina juu ya ni wapi na hospitali gani alikokuwa anaugulia marehemu Gavana Balali na je, ni Serikali ama ni nani alikuwa anagharamia gharama za hospitali wakati wote wa uhai wake hasa ikitiliwa maanani kuwa alikwenda kwenye matibabu bado akiwa mtumishi wa umma? Ni vema tukajua pia gharama za matibabu hayo.

Mheshimiwa Spika, Ndugu Balali alikuwa kiongozi wa juu sana na Watanzania wanahitaji kujua yaliyojiri na kwa kiwango gani alihusika na tuhuma zote zinazohusiana na EPA na kasma mbalimbali zinazohojiwa ndani ya BOT. Kambi ya Upinzani, kwa niaba ya wote wenye nia ya kutaka kufahamu ukweli, itaendelea kuhoji hadi tutakapopata majibu ya kuridhisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri akiwasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2007/2008, alisema naomba kunukuu:-

“Kuratibu utkelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa Taifa wa kudhibiti na kupambana na Rushwa, mwaka huu serikali inakuja na hoja kuwa sasa ni mwaka wa kuwahusisha wadau”.

Mheshimiwa Spika, hivi kama kuratibu tu ilichukua mwaka mzima je, hili la kuhusisha wadau litatumia miaka mingapi na je, tutaweza kufikia lengo la kupambana na Rushwa na Ufisadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendesha nchi kwa kufuata misingi ya sheria na demokrasia, ndio nguzo kuu ya utawala bora. Utawala unaofuata sheria maana yake ni kupinga aina zote za ufisadi zinazoihujumu nchi na kuwanyima haki wananchi katika umiliki wa raslimali zao. Aidha, uwepo wa demokrasia maana yake ni uwepo wa haki za msingi za binadamu pamoja na zile za kisiasa zinazoweza kulindwa na kusimamiwa kwa ukamilifu wake. Swali la kujiuliza ni kuwa kweli Tanzania inaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya utawala bora?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, katika kujibu swali hilo, inaona kuwa Tanzania haina utawala bora, kwa vigezo vichache vilivyoainishwa hapo juu ni kweli utawala bora bado. Ufisadi ndio umeota mizizi, sheria haziheshimiwi, mfano tumetunga sheria kwamba mwekezaji aende *Tanzania Investment Centre (TIC)*, mambo yake yote yatamalizwa, bado wawekezaji wanatangatanga, *TIC* haina ubavu mradi hakuna tofauti yoyote, huku tunatumia fedha nyingi kuwaita wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, siasa zimefuata mtindo wa kifisadi (fedha ndio inaongoza siasa). Matumizi mabaya ya vyombo vya ulinzi wa raia hasa nyakati za uchaguzi, badala ya vyombo hivyo kulinda maslahi ya nchi na wananchi ili mwananchi achague kiongozi amtakae na kura yake iheshimiwe, baadhi ya watumishi wa vyombo wanalinda maslahi ya watu binafsi, baadhi ya watendaji wa vyombo hivyo vinashirikiana na mafisadi kuficha ukweli wa upotevu na wizi wa raslimali za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inauliza ni nani anatakiwa awe mstari wa mbele alinde *(national interest)* maslahi ya Taifa? Mfano mzuri kuhusu kuvunjwa kwa kanuni na misingi ya utawala bora, ni pale viongozi wa Serikali walipo waalika viongozi wa Vyama vya Upinzani kwa barua, lakini wakafukuzwa katika kikao wakati wa ziara za Mheshimiwa Rais Geita, Mkoani Mwanza. Je, hapa ndio tunajenga umoja wa Kitaifa kama alivyosema Rais katika hotuba yake ya ufunguzi wa Bunge hili? *(Makofi)*

Aidha, sambamba na hilo ni pale aliyekuwa Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es salaam, kutumia ofisi za umma, kutangaza hadharani kabla hajaachia rasmi

ofisi yake kuwa akistaafu rasmi atajiunga na Chama Cha Mapinduzi. Je, watu wenye madaraka Serikalini au katika utumishi wa umma walio kama Kamanda huyo mstaafu ni wangapi? Pia inaonyesha kuwa Jeshi la Polisi lililokuwa chini yake lilikuwa linaongozwa kwa kufuata itikadi za Chama Tawala. Hii ni dhahiri kuwa demokrasia ya kweli katika siasa za nchi hii bado. Serikali inatakiwa kuwabadili watumishi wake kimtazamo ili waendane na mabadiliko ya dunia na mfumo uliopo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Idara ya Usalama wa Taifa, majukumu yake yameainishwa katika Fungu 30. Kambi ya Upinzani, inaomba kuwe na *value for money* inayopatikana kutokana na kuwekeza katika Idara hii kwa kuhakikisha kuwa inasimamia kweli maslahi ya Taifa na ya watu wanyonge hasa kule vijijini na hasa kwa kusimamia sheria na taratibu mbalimbali za kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU, ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Katika taarifa yake ya utekelezaji, inaonyesha kuwa pamoja na mambo mengine, wamefanya tafiti 28 ili kubaini mianya ya rushwa na hatimaye kutoa mapendekezo ya namna ya kuziba mianya hiyo. Kambi ya Upinzani, inaona kuwa taasisi hii, bado ipo nyuma ya dunia ya sasa kwani haonekani ikilishughulikia suala la rushwa kwa stahiki yake na hasa rushwa kubwa zinazofanywa na vigogo mbalimbali kwani wao wamejikita kufuatilia dagaa wa rushwa huku mapapa yakiachwa na kujitengenezea himaya zao bila hofu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaamini kabisa kuwa dawa ya kuzuia rushwa ni uwazi katika utendaji wa kazi huku kila mmoja akiongozwa na Uzalendo juu ya nchi yao. Kila mtu akielewa nini kinafanyika na kwa maslahi ya nani ndio njia pekee. Mfano, Tume ya Jaji Warioba ilikwishafanya kazi hii na wao wanarudia tena na huo kama si ufisadi ni nini? Hili ni tatizo la msingi katika nchi yetu, kufanya kazi moja mara mbili au tatu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni Serikali kuunda Tume za Madini sita tofauti kwa muda wa miaka mitano na zote zinatimia fedha za walipa kodi na baada ya hapo Serikali inaunda Tume ya kuangalia jinsi ya kutekeleza maagizo ya Tume ambazo zimewasilisha mapendekezo ya Tume. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atupe tathmini ya fedha na utekelezaji wa Tume angalau ya Majaji Nyalali, Kisanga na Warioba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tunaomba TAKUKURU watusaidie, hali hii tunaiweka katika fungu gani la upotevu wa raslimali ya nchi? Kambi ya Upinzani, inaamini kabisa kama kutakuwa na mabadiliko ya kimtazamo kwa watendaji wa sekta ya umma (*mindset*)

change), katika utoaji huduma kwa wananchi na wananchi kuelewa haki zao katika upatikanaji wa huduma husika ni dhahiri rushwa itakwisha.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU, haikuchukua hatua yeyote bali inasubiri uchunguzi wa *SFO* ya Uingereza ambayo kimsingi inapeleleza kampuni ya *BAE* ya kwao kuhusiana na tuhuma za rushwa inayoikabili Kampuni hiyo. Watanzania waliohojiwa na *SFO*, ni mashahidi tu wa Uingereza katika upelelezi huo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ieleze Bunge hili ni kwa nini Serikali au TAKUKURU inapata kigugumizi kuwapeleka Mahakamani wahusika hao kwa tuhuma ya rushwa ya katika ununuzi wa Rada baada ya mtuhumiwa aliyepokea dola milioni 12 kuruhusiwa kukiri kuweka fedha hizi katika akaunti yake Uswisi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, isitoshe Serikali ilimwachia huyo baada ya kutoa kiapo mbele ya Mahakama ya Kisutu na hata Hati zake za kusafiri hazikuchukuliwa! Wananchi wengi wamepoteza imani na TAKUKURU kama chombo cha kupambana na rushwa, kwani kinaonekana kuwa chombo cha kuwalinda mafisadi. Kuna baadhi ya viongozi wenye fedha nyingi katika akaunti za nje na ndani ya nchi ambazo hazielezeki kwa vipato vyao halali, hata hivyo hawajachukuliwa hatua yeyote angalau ya kiuchunguzi wa kijinai, ama sivyo Bunge lielezwe tofauti.

Mheshimiwa Spika, kunyamaza huku kwa Taasisi hii katika kuwachukulia hatua wale wote wanaotuhumiwa kuwa wameliingizia Taifa hasara kubwa kwa maslahi yao binafsi kunasababisha wananchi wakose imani na Taasisi hii muhimu. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ianzishe mchakato wa kuichunguza TAKUKURU yenyewe kwa lengo la kujisafisha, kuona kama yenyewe ni safi, jambo ambalo kimsingi linaashiria kuwa haiko safi ndiyo maana linashindwa kuchukua hatua kwa watuhumiwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri wakati akiwasilisha Hotuba yake ya Bajeti kwa mwaka 2007/2008 alisema kuwa, ninanukuu: “Kuendelea na uchunguzi wa tuhuma 2,037 zilizopo na nyingine zitakazowasilishwa, kipaumbele kitawekwa katika tuhuma zinazohusu mikataba mikubwa, manunuzi Serikalini, matumizi ya fedha za Serikali katika miradi mikubwa.” Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina juu ya hatua ambazo zimefikiwa kwenye uchunguzi huu na hasa wa mikataba mikubwa na manunuzi Serikalini. Ni hatua gani zimechukuliwa hadi sasa?

Kama kwa kipindi cha mwaka mzima TAKUKURU imefanya uchunguzi wa tuhuma kubwa za Rushwa zipatazo kumi na ni tuhuma tano tu kati ya hizo ndio ziko katika hatua za mwisho za uchunguzi, kwa mwendo huu je? Tutaweza kweli kukabiliana na rushwa kubwa?

Kama kwa mwaka mzima hatuwezi kupeleka kesi hata moja ya rushwa kubwa Mahakamani TAKUKURU wana haja kweli ya kuwepo? Kuna haja ya wao kuendelea kutumia rasilimali za nchi kama hawawezi kulisaidia Taifa? Tena siku hizi kazi yao kubwa imekuwa Semina yenye sura ya posho tu, isiyo na fanaka, kwani kwenye Wilaya nyingi maafisa wa TAKUKURU ndio wanaosemekana kuhusiana na wahalifu kuhujumu nchi kwa njia ya rushwa. Tunamtaka Mheshimiwa Waziri atupe majibu ya kina. Kwa mwendo huu tunahitaji muda wa miaka mingapi ili kuweza kukabiliana na rushwa hizi kubwa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: Katika utekelezaji utawala bora katika nchi, ni kuwa na Serikali inayowajibika kwa wananchi. Viongozi wanatakiwa wawe walio na maadili mema na kuwa mfano wa kuigwa kwa Watanzania wote kama alivyokuwa Hayati Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, misingi ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mujibu wa Ibara 132(5) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano ni pamoja na kuwataka viongozi wa umma kutoa mara kwa mara maelezo rasmi kuhusu mapato, rasilimali na madeni na kupiga marufuku mienendo na tabia inayofanya viongozi kuonekana hawana uaminifu au uadilifu au kuonekana kuwa kichocheo cha rushwa katika shughuli za umma na kuhatarisha maslahi au ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, Waziri wakati anawasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2007/2008, alisema na ninanukuu: “Kuendelea na zoezi la kuhakiki mali za viongozi wapatao 400 walizotaja katika tamko la Rasilimali na Madeni kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa mali zilizotajwa katika tamko ndizo walizonazo.

Aidha, ulinganisho utafanywa kati ya mali zilizotajwa kwenye Tamko na maelezo ya kipato cha viongozi husika.” Mwisho wa kunukuu. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri kutoa maelezo ya kina juu ya hatua ambayo imefikiwa hadi sasa kwani ni mwaka mzima sasa tangu Waziri atoe ahadi hiyo ndani ya Bunge. Pili, tunamtaka Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina juu ya hatua ambazo zimechukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 28 April, 2008 ni Viongozi wa Umma 4,261 sawa na asilimia 57.22% tu ndio wamerejesha fomu za tamko la mali na madeni kati ya viongozi 7,447 waliokuwa wametumiwa fomu hizo. Kati ya hao viongozi wa siasa waliowasilisha fomu zao ni 2,130 kati ya 3,983, sawa na 53.5% tu, huku viongozi wa utumishi wa umma ni 2,734 kati ya 3,464, sawa na 80%. Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina ni viongozi gani hao wa kisiasa ambao hawajawasilisha fomu zao kwa madaraja yao kama ni Mawaziri, Wabunge na Madiwani ni wangapi kwa kila kundi na kwa kuwa mengine ni ya kikatiba, ni hatua gani imechukuliwa dhidi ya viongozi hao wanaodiriki kuvunja Katiba na kutotekeleza Sheria za Nchi?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutokana na Ibara 132(6) ya Katiba, imeweka masharti ya kiongozi wa umma kufukuzwa

au kuondolewa kazini kutokana na kuvunja maadili ya viongozi, bila kujali kama kazi hiyo ni ya kuchaguliwa au kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina juu ya viongozi na watumishi wa umma ambao wamechukuliwa hatua hii kwani kila mwaka tunaletewa taarifa hapa Bungeni kila wakati kuwa kuna viongozi ambao hawatekelezi sheria hii. Kwa nini hatua hazichukuliwi? Ama hao viongozi na watumishi wako juu ya sheria za nchi? Tunataka maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutumia takribani milioni 150 kwa ajili ya kulipia gharama za kuendesha vikao vya Tume kujadili rufaa na malalamiko yatakayowasilishwa kwa Tume.

Aidha, Tume itatumia kiasi cha shilingi milioni 360.134 kwa ajili ya kujadili mashauri ya nidhamu na masuala ya ajira. Kambi ya Upinzani inaona kwa kweli hii ni kutokutenda haki kwa Watanzania walipa kodi wa nchi hii, kwa sababu mtumishi anapopata ajira anapewa masharti ya ajira mojawapo ikiwemo nidhamu yake mahali pa kazi. Kinyume na hapo kanuni ziko wazi, hivyo kuna sababu gani za kutenga fedha nyingi namna hiyo kwa ajili ya kujadili nidhamu ya watumishi? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Grace Kiwelu, ahsante sana kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Sasa Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia wameanza kuongezeka kidogo, lakini ngoja niwataje wote ambao wameomba kuchangia na bado ninasema kuna nafasi kwa wale ambao wanataka kuchangia.

Kwanza, ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Willison Mutagaywa Masilingi, Mheshimiwa Dr. Zanaib Gama, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Stephen Galinoma na Mheshimiwa Said Amour Arfi. Nimepata wengine wawili sasa hivi ambao ni Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama na Mheshimiwa Kanal Feteh Saad Mgeni.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea na hatua nyingine, sasa nina udhuru kidogo ofisini kwa maandalizi ya wageni wetu. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid - Mwenyekiti aweze kuja hapa kuendesha shughuli zilizosalia.

Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid) Alikalia kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nitaanza kuwapa nafasi wachangiaji kama tulivyosomewa na Mheshimiwa Spika na naanza kumwita mchangiaji wa mwanzo Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais ambayo

inajumuisha masuala ya Utumishi, Utawala, TAKUKURU, Usalama wa Taifa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajitahidi muda uwe wa kutosha nichangie maeneo matano. Kwanza, nitaanza na Idara ya Usalama wa Taifa, Tume ya Mipango, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, suala zima la wastaafu na suala la TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970 Sheria Na.3 na Sheria Na.15 iliyoanzisha *Tanzania Interagency and Security Service -TISS*, Sheria Na.15 imeunda chombo muhimu sana kwa ajili ya usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninasikitika kwamba chombo hiki Sheria imekiziba mikono na hasa Sheria ya mwaka 1996 imekifanya chombo hiki kishindwe kabisa kufanya kazi ambazo kinapaswa kufanya kwa ajili ya ulinzi wa Taifa letu. Imekuwa ni nadra sana kuzungumzia suala la Usalama wa Taifa katika Bunge hili, ni kwa sababu ya unyeti wa Usalama wa Taifa. Lakini tukikaa bila kulizungumza tutaendelea kupata matatizo makubwa sana. Toka mwaka jana Taifa limekuwa likipiga kelele, viongozi mbalimbali wamekuwa wakipiga kelele kuhusiana na masuala ya ufisadi na masuala haya siyo kwamba ni mazuri sana kuyazungumza. Kwa sababu sio kwamba yanatusaidia sana, maana yake ukiangalia *flow* ya *FDI Foreign Direct Investment* inaangalia sana masuala kama haya ya ufisadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni lazima tuyazungumze kwa sababu ni sawasawa na mtu ambaye anataka kusafisha mtaro. Unapotaka kusafisha mtaro wa maji machafu ni lazima kwanza uchafuke uingie kwenye mtaro, uusafishe, utoke uende ukaoge baada ya kuwa mtaro umekuwa msafi. Sasa lakini Serikali imekuwa ikipiga dana sana katika suala hili zima kwa sababu hatujaitumia vizuri Idara ya Usalama wa Taifa. Kwa sababu Sheria za Idara ya Usalama wa Taifa zimeibana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa masuala matatu tu. Kwa mfano, suala la nishati ni suala la Usalama wa Taifa, *national security concerned*, ilikuwaje nchi yetu ikaingia mikataba ya nishati bila *clearance* ya Usalama wa Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mikataba kama hii inapaswa kupata *clearance* ya Usalama wa Taifa ili tuweze kuona kwamba nchi inafaidika au haifaidiki, tufanye *espionage* kuweza kujua kampuni hii ni halali ama siyo kampuni halali. Lakini matokeo yake tumeingia kwenye matatizo kama nchi na Idara tunayo, watu tunao, tunawa-*finance* kila mwaka tunapitisha bajeti hapa na wala huwa haijadiliwi kwa kina bajeti ya Usalama wa Taifa, lakini kwa sababu Sheria imesema kazi yao hao ni kutoa ushauri tu, baada ya ushauri hakuna kinachofanyika.

La pili, ni suala ambalo Serikali imetoa kauli hapa juzi katika suala la *Meremeta*. Nataka kuwahakikishia kwamba suala la *Meremeta* halina uhusiano wowote na Usalama wa Taifa. Leo hii Bunge linaambiwa kwamba *Meremeta* haiwezi kuzungumzwa kwa sababu ni la Usalama wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niwambie kwamba, Kamati ya Rais ya Madini ilijadili suala la *Maremeta*. Ndani ya Kamati ya Rais ya Madini kulikuwa na watu wengine ambao sio Waheshimiwa Wabunge. Kulikuwa na watu ambao ni wafanyabiashara tu wala hawajawa *vetted* wala watu hao hawajala kiapo chochote, lakini tulijadili nao suala la *Meremeta* na tukatoa mapendekezo mahsusi kuhusiana na suala la *Meremeta*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Meremeta* ni wizi wa waziwazi na ni wizi ambao ni lazima Serikali iji- *clear* na iseme na kama haiwezi kusema *in public*, ndiyo maana Bunge lina Kamati za Bunge. Tuna Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kamati hii inaweza ikafanya mikutano yake *in camera*, mikutano ile isionyeshwe na Serikali ikaeleza ukweli kuhusu suala hili ili hayo mambo tuyamalize tuanze kujadili masuala ambayo yanahusu maendeleo ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini anaposimama Kiongozi wa Serikali tena Kiongozi mkubwa kabisa akasema hili hata mnisulubu nalo silisemi, hapana. Nitahitaji Bunge lipate maelezo mapya kuhusiana na suala hili na kama hayawezi kutolewa humu *in floor*, maelezo hayo yatolewe kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa sababu suala la *Meremeta* ni wizi na halina uhusiano wowote ule na Usalama wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kitu kimoja, mwone wenzetu jinsi ambavyo wanatumia Idara zao za Usalama wa Taifa sawa sawa. Mwaka 2005 Bunge hili liliamua kupiga marufuku uuzaji wa *Tazanite* ghafi na madhara ya marufuku hiyo ilikuwa ni kupoteza ajira 500,000. Kule India kuna Mji mmoja unaitwa *Jai Pool*. Idara ya Usalama wa Taifa ya India ina kitengo *cha Economic Espionage* wakajua madhara ya uamuzi wa Serikali ya Tanzania. Walichokifanya wakaongeza *scholarship* kwa Tanzania, wakaalika viongozi wetu kule mpaka leo hii *Tanzanite* bado inasafirishwa ikiwa ghafi. Kwa sababu walifanya *espionage* wakatuzuia hatukutekeleza maamuzi ambayo sisi tuliyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo tunapozungumza hapa na Waziri wa Zambia alikuwepo hapa. Nchi ya Zambia inajenga reli mbili. Moja, kuelekea Bandari ya Msumbiji na nyingine kuelekea Bandari ya Angola. Reli zile ndizo zitakazosafirisha *copper* yao na ndizo zitakazosafirisha madini yao mengine yoyote ama kwenda Rwanda au kwenda Manyika Msumbiji. Madhara yake ni nini? Ni kwamba *TAZARA* itakufa, *TAZARA* haitapata mizigo ya kusafirisha kutoka Zambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya kati hii haitapata mizigo ya *copper* kutokea Mashariki ya Kongo kwa sababu watajenga reli kutokea Rungumbasi kwenda Lusaka kuunganisha mpaka kwenda kule Rwanda. Hii ndiyo kazi ya Usalama wa Taifa ilipasa kufanya. Ilipaswa tufanye *economic espionage* kuweza kuona madhara ya maamuzi ya nchi zingine ambazo zinatuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwamba ifike mahali Bunge liamue na nimetoa mchango mrefu sana kuhusiana na suala la Usalama wa Taifa, nitauwasilisha kama mchango wa maandishi kwa sababu siwezi kupata muda mrefu zaidi wa kuweza kulizungumzia. Bunge liamue kwamba ni lazima tupitie upya Sera yetu ya Usalama wa Taifa. Ni lazima tufanye marekebisho ya Sheria ya Usalama wa Taifa na kifungu kimoja cha Sheria ya *TISS* ya mwaka 1996 kifungu 5(2)(a) ambacho kinawapa *TISS* kazi yao wakishaona kama kuna tatizo wanamwambia Waziri tu mhusika, hawana uwezo wa *reinforce security* ndilo tatizo lililotokea katika *EPA*. Kwa sababu fedha za *EPA* zinaibiwa zimeibiwa kwa *cash*, Idara ya Usalama wa Taifa ilikuwa inafahamu, lakini hata kama walitoa ushauri usingeweza kutekelezwa. Nilikuwa naomba suala hilo liweze kuangaliwa kwa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ninataka ni Tume ya Mipango. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuunda Tume ya Mipango. Ni muhimu sana na ni kitu ambacho kwa kweli kitatusaidia sana huko tunakokwenda. Lakini sikubaliani hata kidogo na wala haina mantiki Tume ya Mipango kuwasilisha Bungeni hapa na Waziri anayehusika na Utumishi. Nitawaambia madhara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mmeshuhudia mchango wa bajeti wa mwaka huu. Waheshimiwa Wabunge, takriban wote wamejikita katika masuala bajeti ya Wizara ya Fedha. Masuala yote yanayohusiana na mipango ya kiuchumi hayakupewa kipaumbele. Ukiangalia bajeti ambayo Mheshimiwa Hawa Ghasia ameiwasilisha leo ni *paragraph* mbili tu ndizo zimezungumza kuhusu Tume ya Mipango. Tume ya Mipango inapeleka taarifa yake kwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala hawawezi kuyajadili hayo mambo. Haya mambo ni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa rai. Najua kuna wasiwasi wa kwamba wananchi wataona kwamba Mawaziri ni wengi sana, hatuwezi ku-*risk* kutokuwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayehusika na Tume ya Mipango peke yake na nitawambia leo hii kila baada ya miaka miwili kuna kitabu kama hiki kinazalishwa na Serikali, *Poverty and Human Development Report*.

Hiki kitabu ndicho kinacho-*guide* Mipango ya Maendeleo ya nchi na juhudi za uzalishaji na juhudi za kupunguza umaskini. Kitabu hiki kinatolewa na aliyekuwa *commissioned* na Serikali na miongoni mwa vitu ambavyo vinapaswa kufanywa ukiangalia *chapter four* ya kitabu hiki inazungumzia mikakati ya ukuaji wa uchumi wa nchi. Lakini ukiangalia katika mpango mzima wa kazi wa Tume ya Mipango, ile *chart* ambayo Mheshimiwa Waziri ametuonyesha hakuna *reference* yoyote inayoonyesha shughuli kama hizi zitakuwa zinafanywa namna gani? Utakuwa vipi na Tume ya Mipango ambayo haiangalii. Maana yake Tume ya Mipango ni *vision 2025*, Tume ya Mipango ni MKUKUTA na hii taarifa ndiyo utekelezaji wa masuala kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwomba Waziri - Mheshimiwa Hawa Ghasia azungumze na Mheshimiwa Rais, ni bora tuingie gharama ya kumlipia Mtanzania mmoja kwa ajili ya kuwa mwakilishi wa Tume ya Mipango katika Bunge akiwa kama

Waziri wa Nchi wa Mipango. Hatuwezi kuwa hivi tunavyokwenda, tutapata taabu sana huko tunakokwenda. Kwa hiyo, naomba suala hili liweze kuangaliwa kwa jinsi ambavyo linavyostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo nataka kulizungumzia ni suala la maadili ya Viongozi. Tuna tatizo kubwa sana katika maadili ya Viongozi. Sheria ya Maadili ya Viongozi Sheria Na.13 ya mwaka 1995 ina mapungufu makubwa sana na kumekuwa na juhudi za kutaka kuifanyia marekebisho. Mimi binafsi nimewasilisha Ofisi ya Spika Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Viongozi ili tuweze kuifanya iwe na nguvu zaidi. Lakini tumefahamishwa na Mheshimiwa Waziri kwamba taratibu za ndani ya Serikali za mabadiliko ya Sheria hii zimeanza kuandaliwa. Lakini tuna tatizo kubwa sana kwamba taarifa ambazo viongozi tunazitoa kwa ajili ya mali na madeni yetu zinachezewa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa rai kwamba ufanyike uchunguzi maalum tuweze kulinganisha fomu ambazo Waheshimiwa Wabunge wote tulizisaini wakati tumeingia Bungeni na zile za kila mwaka na fomu ambazo zipo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, kuna baadhi ya fomu tutakuta zimerekebishwa baada ya matatizo fulani fulani kuwa yametokea. (Makofi)

Kwa hiyo, nilikuwa nataka tuchukue fomu zote za Waheshimiwa Wabunge ambazo zipo Ofisi ya Spika, kwa sababu *copy* moja inabakia katika Ofisi ya Spika, *copy* nyingine inakwenda Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi tuweze kuangalia, kuna matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, suala hili la maadili ya viongozi liweze kuangaliwa.

Mapendekezo ambayo yametolewa na Mheshimiwa Spika, alitoa uamuzi kwamba Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iiangalie Sheria hii ya Maadili na nilitarajia kwenye Taarifa yao wangeweza kugusia kitu kama hicho. Hawakukigusia, wamekwenda tu juu juu.

Lakini pili, tunahitajika kuwawezesha wale Watanzania wanaofanya kazi katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi waweze kuwapatia mafunzo mahsusi kwa sababu ni moja ya Idara ambayo inapewa bajeti finyu sana lakini ina-*handle* mambo nyeti sana kwa sababu siri zetu zote, mali zetu zote, madeni yetu yote yanafahamika kwa watu wale. Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba tunawawezesha jinsi inavyostahili ili waweze kufanya kazi yao sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimesikitika sana kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri haijagusia kabisa suala la wastaafu na hao ni Watanzania ambao wamefanya kazi ya kujenga nchi yetu kwa miaka yao yote na kuna matatizo makubwa sana ya wastaafu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu wanapata shilingi 21,000/= kwa mwezi na sisi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, tunavyosumbuliwa na wastaafu hao huko kwenye Majimbo kwetu, lakini Mheshimiwa Waziri hajaelezea chochote. Sasa sijui siyo suala ambalo haliko kwenye *mandate* yake kama Waziri au ni vipi? Lakini nilikuwa

nadhani kuna haja ya kuangalia upya suala hilo la wastaafu ili tuweze kuhakikisha kwamba ni Watanzania ambao wamefanya kazi tena wengine hata hawakuiba, wamefanya kazi kwa uadilifu, waweze kuishi maisha mazuri huko vijijini ambako wanakwenda au hata hao wengine ambao wapo Mijini ili tuweze kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ni suala la TAKUKURU, Msemaji wa Upinzani kuhusiana na Wizara hii amezungumza suala la TAKUKURU amesainisha mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa naomba Serikali iangalie kuna matatizo makubwa sana ndani ya TAKUKURU. Watumishi na viongozi hawaelemani, kuna kushutumiana, kunawavunja moyo wale wafanyakazi wa ngazi ya chini Wilayani wa TAKUKURU wanaofanya kazi ya kuchambua matatizo mbalimbali ya kufanya ukaguzi wa masuala yote yanayohusiana na rushwa yakifika Makao Makuu hayashughulikiwi. Kuna tatizo kubwa sana ndani ya TAKUKURU, inawezekana Serikali inalijua hilo au hailijui.

Lakini pia kumezuka mtindo ndani ya TAKUKURU zinapotokea taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ufisadi na mambo ya rushwa, wafanyakazi wadogo hivi sasa tunavyozungumza kuna Kamati imeundwa ya *witch-hunting* ya kwamba ni nani ambaye anazungumza mambo ya TAKUKURU nje?

Nadhani kuna haja kubwa sana Serikali ili iangalie suala hili. Waziri anayehusika nadhani ni Mheshimiwa Sophia Simba, noamba aliangalie, akae na viongozi wote wa TAKUKURU kuanzia Mkurugenzi, Naibu Mkurugenzi na Wakurugenzi wengine wote, kuna matatizo makubwa sana na ndiyo maana kesi zinazohusiana na ufisadi mkubwa, mikataba mikubwa mbalimbali ambayo Serikali inaingia ambayo ina ufisadi haifuatiliwi, kwa sababu ya migawanyiko iliyopo ndani ya kada ya juu kabisa ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale ambayo nilitaka kuyazungumza nimeyamaliza. Masuala ya Usalama wa Taifa nitampelekea Mheshimiwa Waziri kwa maandishi kwa sababu ni mengi sana. Nimeweza kuainisha matatizo ambayo tumekuwa nayo kama nchi, hali ambayo tunaipitia hivi sasa na Serikali kuwa iko *slowly* katika ku-*respond* katika masuala kama haya ambayo yatatuathiri sana kiuchumi huko tunakokwenda. Ni muhimu sana kuboresha Idara hii na kuwawezesha wafanyakazi wa Idara hii ili waweze kupata mafunzo mazuri na ya kisasa tuirekebishe Idara kutokana na mwelekeo wa mwaka 1970 wakati wa vita baridi iwe na mwelekeo wa sasa ili tuweze ku-*possession* nchi katika hali ambayo tutaweze kupambana katika *globalization*, lakini pia katika eneo zima la Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika Ofisi ya Rais. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii na nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri mwenzake mwenye dhamana ya Utawala Bora katika Ofisi ya Rais, watumishi wote ndani ya Ofisi ya Rais. Niseme kwamba yaliyoelezwa katika kifungu cha tatu ukurasa wa pili kuhusu uchapakazi wa Rais ambaye ni mtumishi namba moja ni sahihi, anachapa kazi kweli! Hapumziki! Kwa kweli Serikali yake inafanya kazi vizuri sana pamoja na kwamba kuna matatizo ambayo ndiyo dhamana yetu kusimamia kuhakikisha yanapungua au yanaondoka kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na hili la watumishi kupewa mshahara wa Sh.100,000/= kima cha chini kwa kweli hakitoshi. Hakitoshi kabisa na cha kusikitisha kabisa, zaidi hata na mimi nilidhani angetuambia kuongeza kima chini cha pensheni ya wazee wetu wastaafu, sasa sijui ni yeye anayepaswa kusema au kuna mwingine atasema kwa sababu tulisubiri aseme kwamba labda kima cha chini cha mshahara ndiyo kima cha chini cha pensheni pia. Kwa sababu Wabunge tumelisemea hili kwamba watumishi wetu wanapostaafu wasipopata pensheni ya kutosha maisha yao baada ya kustaafu ni magumu sana. Sasa anapokuwa ndani ya utumishi anapewa mshahara kidogo ndiyo chanzo cha kukosa amani ndani ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kulisisitiza hili, nilisema wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwamba ndani ya utumishi wa umma hakuna amani kwa sababu hawatosheki hao watu, huo ndio ukweli. Hawaoni faida ya kuwa na dhamana ya kulinda hata siri za Serikali wanauza. Sasa yeye mhudumu unampa Sh. 100,000/= ana njaa, ataacha kuacha bahasha ya siri kwa mtu anayeitafuta? Ndiyo maana tunaanza kusikia watu wana barua za siri.

Sasa pamekuwepo mvutano, hili ni kosa la Jinai nao wanasema kama ni wizi tukutane kotini. Sasa aliyemaliza kuchangia sasa hivi ni Mheshimiwa Zitto Kabwe, yeye anajua hata migogoro ndani ya TAKUKURU walivyogongana. Hilo linapaswa litolewa maelezo lisipuuzwe kwa sababu Kabwe Zitto hawezi kusimama hapa kuzungumza mambo ya TAKUKURU bila kuwa na ushahidi. Mimi naanza kumpa *benefit of doubt* kwamba anasema anachokijua. Kwa hiyo, ndani ya TAKUKURU kuna watu wamemweleza hafanyi kazi kule yeye. Mtoe maelezo kwa nini wanagongana na kwa nini habari zinatoka nje kwenye chombo ambacho kinapaswa kuwa cha siri ndani ya Ikulu? (*Makofi*)

La pili, napenda kuzungumzia habari ya kuheshimu kanuni na taratibu na sheria. Mimi nilivutiwa na mchango wa Mheshimiwa Dr. Harrsion Mwakyembe, tulikumbushana hata na sisi humu maana yake sisi ndiyo watunga sheria na tunapaswa kuwa mfano kuheshimu hata kanuni zetu kutorudiarudia ambayo tumeshayaamulia bila kuzingatia kanuni kwa kutengua kanuni ili ianze kujadiliwa.

Hili namuunga mkono sana *classmate* wangu Dr. Harrison Mwakyembe. Lakini niseme tu kwamba hata na sisi Wabunge tujipongeze kwa kweli na sisi tuna tabia nzuri, si ni watumishi na sisi wa umma ambao ni wanasiasa tunafanyakazi nzuri ili tupate moyo. Maana yake tutakuwa hii *tension* kila mtu anaangalia mwenzie. Tunachapa kazi vizuri mimi nawapongeza Wabunge wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa ndani ya uchaguzi, mpaka tunapitisha Sheria ya Rushwa marekebisho yake ya mwaka 2007 tuliahidiwa na Serikali kwamba kipengele cha rushwa wakati uchaguzi au kwenye vyama vya siasa kitashughulikiwa baadaye katika mchakato ulioahidiwa na Mheshimiwa Rais, kwamba wananchi watajadili tufanyeje na wadau tushiriki liko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi ni mwaka kesho, tunaanza Serikali za Mitaa, mwaka keshokutwa, ahadi ni ya Mheshimiwa Rais, ndani ya Ukumbi wa Bunge hili halikuzungumziwa, tupate maelezo. Nimeangalia ukurasa wa 39 nilitarajia TAKUKURU ndiyo wataratibu elimu hii, mdahalo huu au majadiliano haya. Lakini katika shughuli zake halimo. Sasa nasema hivi, TAKUKURU wanasema mambo ya vipaumbele ukurasa wa 39 mpaka 40, rushwa kubwa kubwa, endelea nazo kubwa kubwa lakini msisahau ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ndogo ndogo ni rushwa. Mimi mpaka kesho sitaamini kwamba kuna tofauti kati ya rushwa kubwa na rushwa ndogo. Mimi binafsi huwa sijui tofauti yake. Ie ndogo iliyopo kwenye Serikali za Mitaa ina madhara makubwa hata kwa upotevu wa fedha za umma. Zaidi ya trilioni moja inapeleka Halmashauri za Wilaya. Hesabu ndani ya vijiji, mikutano ya vijiji haiitishwi na Wakurugenzi hawafuatilii na wana magari na wananchi wanalalamika fedha zao hazitolewi taarifa ya mapato na matumizi.

Kama mikutano ya kisheria haiitishwi, kwanini tuiseme kuna rushwa pale? Wananchi wanampigia kelele Mbunge, Mbunge unaeleza, mkurugenzi hafuatilii. Sisemi Wakurugenzi wote, ni baadhi yao. Sasa hawa ndio wa kufuatiliwa na TAKUKURU. Kwanini Mikutano Mikuu ya vijiji haikutani kutoa taarifa ya mapato na matumizi? Tunapeleka zaidi ya trilioni moja, tunazopeleka kwenye Halmashauri tujue zinawafikia walengwa? Kuliko kuja kusikia ndani ya Bunge hili tunapewa taarifa, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Halmashauri kiasi kukubwa kimeliwa na wabadhirifu, haikuwafikia walengwa na *machinery* tunayo! Kwa sababu pesa ni nyingi, tuwaongezee mishahara na posho TUKUKURU wafanye kazi katika ngazi ya vijiji na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya yangu wamenituma salamu za pongezi kwa TAKUKURU. Sasa itawashangaza sana, kumbe kuna maeneo mengine wamechemsha! Muleba, TAKUKURU wanafanya kazi! Watu wameanza kulala macho, wale mnaita sijui mafisadi! Maana yake kuna mafisadi na vifisadi. Sasa sijui tuwaite mafisadi au vifisadi. Kule vyenyewe havisinzii sasa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa TAKUKURU na Mkurugenzi Mkuu, pongezi sana, ongeza kasi, ikiwezekana tangaza vita nchi nzima. Inawezekana nyinyi kutokusema mnachokifanya wanadhani hampo na mpaka watu wanasema hamstahili kuwepo. TAKUKURU ikiondoka twafa! Mimi najua TAKUKURU.

Kuna wengine hawaipendi hii TAKUKURU na hii ni kwa sababu inawasaka na upelelezi unachukua muda mrefu. Wapeni pesa wapeleleze kesi ziishe haraka sana, watu wachemke Mahakamani. TAKUKURU fanyeni kazi, wale wabovu ondoeni, maana hata ukizaa watoto hawezi kukosekana mwizi humo na mvuta bangi. Sasa safisha safisha hivyo vichafu ndani ya TAKUKURU na kama kweli mnagongana, hiyo ni aibu. Mnashindana nini? Chapeni kazi, kamata wala rushwa, lakini vilevile muwe macho. Msije mkachemsha mkakamata wasio na makosa ili kutufurahisha, hapana. Kama watu hawajala rushwa pumua tu. Anayepiga kelele kwamba kuna rushwa akuonyeshe nani amekula. Msiogope, kamata kikweli kweli baada ya kuchunguza chukua muda mrefu kuliko kuonea. Kheri majambazi 99 yapotee kuliko kumfunga mmoja asiye na hatia, ndiyo imani yetu sisi katika Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawapongeza sana TAKUKURU. Muleba mwongoze kasi, mimi kule nitapumua. Sasa na kwenye mikataba mikubwa kama mmekamilisha, kamata hawa watu peleka Mahakamani. Kwa kweli naomba kwenye Wilaya ongeza magari ya TAKUKURU, wafanyakazi wale wape moyo, wape motisha, vijana wajiamini, wapambane na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF*. *TASAF* hawa lazima niwapongeze. Nilikwenda kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa *TASAF* kumwuliza fedha ambazo amepeleka kwenye Wilaya yangu na nikamwambia nitarudi kesho unipe taarifa. Kwa sababu nitarudi Jimboni kesho kutwa akasema usitoke, nakupa sasa hivi. Akasema vyote ninavyo kwenye mtandao, akabonyeza baada ya dakika tatu alinipatia taarifa yote ya Muleba, miradi yote kwa majina, fedha zilizokwenda na zilizokwishatumika. Unajua kuna mambo mengi yanafanyika ndani ya Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tusiseme mafisadi tu, kuna wanaochapa kazi mle *TASAF*. Sasa nAshauri hivi, hivi kwa nini Halmashauri za Wilaya hawapelekwi shule ya *TASAF*? Kompyuta zimo kwenye Halmashauri za Wilaya, ukimwuliza Mkurugenzi taarifa miezi minne na ikija inakuja robo. Kwanini hawaweki kwenye kompyuta na hawako wazi na kwanini tuendelee kuwalea? Kama watu hawajui kompyuta peleka shule, hawajui ajiri wanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu wa *TASAF* tumemtoa nchi za nje, Bwana Likwilile. Si ni Mtanzania na wasaidizi wake wapo mpaka Wilayani! Kama hawa hawawezi kuelewa, Bwana Likwilile achukue Halmashauri zote na zile pesa zinazokwenda kwenye Halmashauri ziwe wazi, tuweze kusimamia. Ni mabilioni kwa maelfu ili tukikosa kuona hela ile tumweleze TAKUKURU awashughulikie. Tukikaa tunajibizana hapa, tutaanza kuzungumza ufisadi, ufisadi ambao mimi nasema mwendelee kusema. Mimi sichukii mtu akisema fisadi fisadi, isipokuwa ninachoomba jamani,

tukisema mafisadi, tuwaseme kweli na wawepo kweli. Kwa sababu siku nyingine tutakuja kuumizana bila sababu.

Mimi nilipokuwa *primary school*, darasa la nne, sitasahau hiyo historia. Unajua mtoto akiwa darasa la nne ana uwezo wa kukimbia sana. Ilitoka sauti ya mwizi! Mwizi! Mwizi! Wanao mkimbiza ni wazee ambao hawawezi kukimbia na yupo mbele yao. Sisi tukamwona tukaanza kumkimbiza na yeye akawa anasema mwizi! Mwizi! Tulikimbia tukampita kwa sababu sisi tunakimbia kuliko hata mwizi. Sasa kule mbele tukaenda hatuoni mtu. Sasa tunaanza kurudi baada ya kutoka kwenye migomba tunakutana na wazee wanasema mbona nyie mlikuwa mnakimbia mbele ya mwizi. Tukashangaa tukasema kumbe ndiyo huyo? *It is too late* na mwizi hatukumkamata. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hadithi ya kweli. Wale niliosoma nao *Rwantege Primary School* kabla sijakwenda *middle school*, ni kweli, wengine hawajafa wanakumbuka. Mwizi, mwizi! Tukampita. Kumbe lilitumia ujanja. Tusije tukakuta mafisadi wanasema, fisadi, fisadi tukawapita mafisadi kumbe fisadi ndiyo huyo unayekimbia naye.

Hii naisema kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ameleta taarifa ya kusikitisha ndani ya Bunge hili. Makatibu Wakuu wanaogopa kuamua na akatoa kauli. Hii ndiyo nataka kusisitiza. Anasema amueni kwa makosa ama kwa usahihi ndiyo nchi itakwenda. Kama wewe sio mwizi na si fisadi, unaogopaje kusaini kitu au kuandika barua? Kuomba tu hela India inakuchukua mwezi, pesa si zako! Wewe unataka kuiba, tukuhonge kwanza ndiyo uandike! Sasa jiaminini, mimi nawaondoa hofu watumishi, nyinyi sio wala rushwa, *presumption* ya *innocence* ipo kwenye Katiba yetu. Nyinyi sio wezi mpaka wathibitische Mahakamani chini ya Polisi na Mahakama. Nyie chapeni kazi atakayekamatwa aende jela.

Lakini mkikaa mmeloa, shughuli haziendi, Bungeni humu kila mtu mwoga hata kujenga mtaogopa kujenga na maghorofa. Eti nikijenga na kuwa na gari zuri wataniita fisadi. Jengeni, atakayekuita fisadi upambane naye na nunueni magari ya kifahari kama fedha ni halali na atakayekuita fisadi pambana naye, sheria zipo za kukulinda. Lakini tukikaa tumeloa, mwisho tutaanza kuokota vizibo, watumishi wataanza kustaafu bila magari, mtu anasomba kifusi wanamfuata. Sombeni vifusi pateni viwanja.

Mimi nawaondoeni uwoga, mimi nimejenga, nitafuteni niwaeleze nilivyojenga. Mbona sijaulizwa? Eti nasikia fomu zinabadilishwa na hili lifuatiliwe! huyu amejuaje maadili? Fomu ya Spika na maadili ya Mbunge ni tofuati, si ni jinai hiyo na Mheshimiwa Zitto Kabwe! Huwa hawezi kusema uongo, ni Mwenyekiti wa Kamati na yupo kwenye *Steering Committee* kama mimi na yenyewe ichunguzwe tukikuta sio kweli atutake radhi. Sisemi wamhoji sasa hivi, hapana. Chunguzeni huko, hivi ni kweli huyu ni Mbunge? Lazima tumheshimu. Mimi Wapinzani huwa naheshimu kauli zao. Kwa hiyo, muwe *responsible*, ukisema ukanistua nakufuatilia polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema TAKUKURU chapeni kazi, mapungufu yalipo rekebisheni na mimi Muleba mambo yaninyookee. Mimi ukininyooshea Muleba

nawapongeza, ya mikataba mikubwa siijui na sijui ni ipi kwa sababu sipo Serikalini. Mimi najua Halmashauri ya Wilaya ya Muleba Vijijini. Msipokwenda huko nitalalamika, lakini sasa hivi nawapongeza. Nimetumwa na wananchi na wananisikia. Siji kumfurahisha TAKUKURU, Hosea chapa kazi na Mungu awalinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. (Makofi)

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa, nasema naunga mkono hoja mia kwa mia ili nisije nikasahau baadaye. Mimi nataka nisaidiwe kitengo cha TAKUKURU. Je, wana utaratibu gani ili Miswada au sheria kuzitizama kama kuna mianya ya rushwa? Maana tunapozungumzia *prevention* na *treatment*, basi ile Miswada inayoletwa Bungeni kabla haijaletwa, TAKUKURU na Utarawala Bora wangukuwa na utaratibu wa kutizama Miswada ile kama ina mianya ya rushwa.

Kwa mfano, Muswada wa *Public Leaders Code of Ethic*. Sheria Na.13 ya mwaka 1995, viongozi tunatakiwa tu-*declare* mali zetu na madeni. Lakini Sheria hii ina mwanya wa rushwa ndani yake. Kwanini nasema hivyo? Dr. Gama nimepewa fomu nikajaza, Dr. Gama mnamfahamu, mapato yake. Nikasema nime-*declare* kihalali bila kuficha nina trilioni moja. Je, Sheria inasema nini baada ya hapo. Dr. Gama ninastahili kuwa na trilioni moja? Sheria inasema nini baada ya mtu akisha-*declare* ukiacha kungojea mpaka mtu alalamike? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu. Sheria izidi kuendelea na kusema kwamba ndio amesha-*declare*, lakini unamtizama na huyo mtu aliye-*declare* Dr. Gama ana trilioni moja. Sheria iseme wamchunguze. Mimi najua kuna watu wamesha-*declare* wana mabilioni ya hela. Lakini Sheria haisemi kitu, wamekaa tu, mwisho tunaanza kusikia Waandishi wa Habari wanazungumza mambo mengine. Kwa hiyo, mimi naomba hii Sheria iwe na utaratibu wa kutazama, mtu ame-*declare* kwa usahihi, lakini ukimtizama mapato yake hastaili kuwa na hela hiyo ili kuwe na utaratibu wa kumchunguza na kumchukulia hatua. Sio Sheria hiyo tu, kuna Sheria nyingine kwa mfano Sheria za Mikataba. Muitizame vizuri Sheria ya Mikataba, ina mwanya wa rushwa. Natoa mfano kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Halmashauri sio Mjumbe wa Bodi, Madiwani sio Wajumbe, lakini ile Kamati ikishakaa na kukubaliana, tunampa *tender* huyu, wanamwambia Mwenyekiti wa Halmashauri saina. Anasaini kitu ambacho hakijui. Huo ni upungufu. Hapo kuna mianya ya rushwa. Haina hata utaratibu wa kusema Madiwani kama tuna wasiwasi tuweze ku-*question*, hakuna! Kwa hiyo, mimi nia yangu ni kuiomba TAKUKURU, kila Sheria inayoletwa Bungeni au Sheria zilizopita wazitazame kama kuna mianya ya rushwa. Tuiseme tu wenzetu wameleta Serikalini, wamekuwa wazuri. Lakini kuna wengine sio wazuri, ni wabaya, wanaficha mambo. Kwa hiyo, hilo nilikuwa nataka tusaidiane. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ninaomba TAKUKURU au Wizara ya Utawala Bora iniambie. Najua katika kila Idara ya Serikali, Mahakama na Bunge kuna kitengo kinashughulikia masuala mazima ya utawala bora. Je, hii TAKUKURU au Wizara ina-coordinate namna gani? Ukishawaachia basi waendeleo? Tuwe tunafanya kama UKIMWI. UKIMWI kuna kitengo cha kutizama masuala mazima ya UKIMWI katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, mimi naomba Wizara au TAKUKURU tuwe tunatazama utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka nisaidiwe. Hatujapata maelezo kuhusu *NASCAP One* ule Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa, umefanikiwa kiasi gani au haujafanikiwa kiasi gani? Ni vizuri tungepata maelezo hapa tukajadili, kama sio kwenye semina mtaweza kutafuta utaratibu mwingine. Tungejadili na bahati mbaya *NASCAP Two* bado hatujaipata. Niliuliza: Bunge wameshapata *NASCAP Two*? Haijapatikana! Tumefikia wapi? Huu ni mwaka wa ngapi? Nikajibiwa wa tatu. Sasa tunaendeleaje? Kuelewa nataka nisaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la kuiomba TAKUKURU. Sehemu nyingi inapotokea uvumi wa rushwa, naomba wafuatilie. Mimi naomba niseme ukweli wangu na nimepata nafasi hii nitasema. Nimesikitishwa sana kabisa, kuna mahali pana uvumi wa rushwa, Mbunge anasimama hapa Bungeni anasema kuna uvumi wa rushwa, halafu Waziri anainuka anasema inaonekana hukubaliani na wenzio. Inaonekana mimi nina matatizo. Nimesikitika sana na niliheshimu tu kwa sababu Waziri Mkuu ni mtu mzuri sana, lakini ningeshika shilingi. Mimi naomba TAKUKURU ifuatilie kwangu. Kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jimboni kwangu nimeshasema mahali fulani kuna rushwa, tena sisemi mimi, wenzangu tunakubaliana mahali fulani pana rushwa. Lakini sioni lolote linalotekelezwa. Mfano mzuri ninarudia tena na nitarudia tena hata kama watu wataona mimi nina kero. Tunazungumzia suala la mtu binafsi anagawa viwanja zaidi ya 50 sio kwa faida ya Halmashauri, Halmashauri inashangaa, inakwenda inaweka 'x' na TAKUKURU inafahamu kule Wilayani hakuna hatua inayochukuliwa. Mwisho tunaambiwa kiwanja kile ni cha Ndugu yake Mkuu wa Mkoa, anasingiziwa. (*Makofi*)

Sasa mimi nasema mahali penye uvumi wa aina yoyote, TAKUKURU tunaiomba mfuatilie. Mfuatilie uvumi Mahakamani, nyie wote mnajua hakuna Mtanzania yeyote asiyesema Mahakamani kuna rushwa, uongo, kweli? Sasa mimi nawaomba TAKUKURU hata kama uvumi upo ndani ya Bunge ufuatiliwe wala msituogope kutufuatilia sisi Wabunge. Tufuatilieni. Tatizo ni kwamba bahati mbaya masuala ya TAKUKURU yakishamalizika yakakwenda Serikalini, hayaji Bunge.

Mimi nafikiri ni wakati muafaka sasa tuwe na Kamati inayotizama masuala ya rushwa na TAKUKURU ituletee habari. Mimi hilo naliomba kabisa. Kuacha tu TAKUKURU inapeleka habari Serikalini na Serikali ikanyamaza, mwisho tunakutuhumu kaka yangu Hoseah na wakati mwingine wala huna kosa, unalazimika tu kufanya hivyo na sisi wengine tunajua. Mimi naomba TAKUKURU nayo iwajibike, ripoti yake iletwe Bungeni. Naomba tufanye taratibu kama tulivyofanya kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Lakini lingine ningeomba TAKUKURU kama inawezekana ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu hasa kitengo kile cha *value for money* mngeshirikiana nao. Hapa ndiyo kwenye rushwa. Halmashauri zinatisha, zinapelekewa mabilioni ya hela, lakini zinatisha na wanaokula sana ni watendaji kuliko wale waliochaguliwa. Maana ukichukua elimu ya mtu aliyeteuliwa, kwa mfano Diwani, ukichukua elimu ya mtendaji ambaye ni *graduate* katika masuala hayo, mimi nimemaliza darasa la nne nitapambana naye! Sasa ni wakati muafaka TAKUKURU mkae na CAG na hasa kitengo cha *value for money*. Mimi napenda hilo nisaidiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sikuwa na masuala mengi kabisa. Ila la mwisho, niliposimama wakati wa Sheria ya Rushwa nilisimama katika kifungu cha *part four* nikizungumzia suala zima alilolizungumzia kaka yangu Masilingi la kuingizwa suala la rushwa ya uchaguzi. Katika sheria hiyo, Waziri aliinuka na akasema vizuri, mimi namshukuru sana, kwamba tuwape muda ili tufuatilie hili na Rais ameamua kupata maoni ya watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwaka mzima, hatujasikia mkakati huo, hatujasikia Tume iliyoteuliwa. Maana utaratibu siku hizi ni kuteua Tume. Je, ni yale yalikuwa ni maneno tu ya kulilidhisha Bunge ili Miswada ipite? Mimi nafikiri sasa Waziri atuambie, kauli ile nilitaka tufanye mabadiliko, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri kama huna ninayo hapa haya mabadiliko. Mkaniomba niliondoe na nikaliondoa kwa ahadi yenu. Ninayo mabadiliko ya kipengele namba *four* suala linalozungumzia *corruption, transaction at election*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaahidiwa vizuri sana na mimi nikaamua kabisa kwamba nimekubaliana na Serikali yangu chini ya Chama cha Mapinduzi. Sasa naomba tusaidie ile ahadi itatimizwa lini na kama halitimizwi ni kwa sababu gani? Masilingi kasema hapa mwakani uchaguzi. Hilo ninaomba nisaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho. Katika masuala ya rushwa nilizungumzia suala zima la gari la zimamoto. Gari la zimamoto inaonekana kuna tatizo ikiwemo Wilaya yangu. Kwanza hela ilitaka kuliwa, shilingi milioni 300. Mimi nikasema jamani kuna hela inaliwa, imehamishwa kutoka kwenye akaunti hii imepelekwa akaunti ya Dar es Salaam bila idhini. Tumekaa tumepambana, gari limeletwa. Gari tangu limeletwa mpaka leo halijaja Halmashauri, tunaambiwa lipo *Fire Brigade*, sijaliona. Lakini bado nina taarifa kwamba hiyo ni taarifa ambazo nataka TAKUKURU mzithibitishie kwamba bodi ni jipya lakini vifaa ndani vya zamani. Mpaka leo lile gari halijapewa namba tayari sisi tumeshajenga nyumba ingawa haijamalizika. Tayari tumeshawaajili wafanyakazi tunawalipa kila siku hela ya chakula. Sasa hilo ninataka kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo mimi naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki haumtoshi msemaji anayefuata sasa hivi, Mheshimiwa Magidalena Sakaya, lakini pia napenda nitoe wito

kwamba bado tuna nafasi kwa wachangiaji ili waweze kuendelea kuomba. Lakini kwa jioni napenda nisome hii orodha ili wachangiaji wanaofuata waweze kujiandaa. Jioni ataanza Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Kanali Feteah Saad Mgeni, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Salim Yusuf Mohamed na wa mwisho ingawa nafasi bado ipo ni Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa.

Kwa hiyo, napenda niliahirishe Bunge mpaka saa kumi na moja jioni leo.
(Makofi)

(Saa 06.50 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Steven Galinoma ajiandae.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni ili tuweze kuijadili. Naanza na suala la mishahara ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imesema kima cha chini cha mishahara Serikalini ni shilingi laki moja. Mimi nashindwa kuelewa. Hali ya maisha ilivyokuwa ngumu sasa hivi, ni kweli Serikali imeona shilingi laki moja itamtosha Mtumishi aweze kuishi kwa mwezi mzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kuelewa kwamba Serikali imetumia kigezo gani kuweza kupima shilingi laki moja kama mishahara wa Mtumishi kwa muda wa mwezi mzima. Atagawanyaje hizi hela ili aweze kuishi? Sasa hivi chumba cha kawaida kabisa kwa mfano hapa Dodoma Mjini ni Sh. 25,000/= hadi Sh. 30,000/=, hapo hajalipia umeme, hajalipia maji na hajapeleka mtoto shule, hajala, hajapanda basi aende kazini, hajagua aende hospitali kujitibu. Je, hii shilingi laki moja atagawanya vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani kama Serikali haitaweza kuangalia ni jinsi gani Watumishi hawa tuwaangalie na tuwapatie mishahara ambayo inaweza kukidhi mahitaji yao, tutaendelea kupambana na tatizo sugu la Rushwa na hatutakaa tufanikiwe hata siku moja, kwa sababu kumpa Mtumishi mishahara kidogo inaibua masuala mengine kama ya rushwa, uzembe kazini na masuala mengine kama hayo kwa sababu anaona akikaa pale ofisini na mwisho wa mwezi anapata laki moja haimtoshi kuishi ina maana atakaa pale kwa muda mfupi, anaondoka kwenda maeneo mengine kutafuta riziki

nyingine, atauza *ice cream*, maji karanga na kadhalika, maadamu aweze kupata senti aangalie ni vipi itamsaidia kuishi na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine pia ni suala la rushwa ambalo ninalizungumzia. Hii inakuwa ni kichocheo kwa Watumishi kuweza kudai rushwa ili kuwaongezea kile ambacho anakipata kwa sababu hakimtoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ikae tena iangalie suala hili kwa makini, vinginevyo hali ya maisha ya Watanzania itaendelea kuwa ngumu. Ni kweli kwamba Serikali haifahamu kwamba sasa hivi mchele ni Sh. 1,300/= mpaka Sh.1,400/=? Je, ni kweli hawajui mafuta ya taa ni Sh. 1,500/= mapaka Sh.1,600/=? Ni kweli hawajui kila kitu kimepanda mpaka waweke mshahara shilingi laki moja? Mshahara wa shilingi laki moja hautoshi. Tunaomba Serikali iliangalie suala hili kwa umakini wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *Pension* kwa wastaafu wetu. Lengo kubwa la *pension* kwa wastaafu wetu ni kuwawezesha kuishi baada ya muda wao wa kazi kwisha. Lakini tunakuwa tunazungumza hapa Bungeni muda wote na siku zote, kwamba tunaomba *pension* ziongezeke. Wapo watu ambao wamestaafu, kwa cheo cha Afisa Wanyama Pori *grade II* anapata kwa miezi sita Sh. 180,000/= mpaka sasa hivi, hebu chukua miezi sita mtu amekaa anasubiri sh. 180,000/= itamsaidia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wametumikia Taifa hili kwa muda mrefu, tena kwa uaminifu, wana hali mbaya sana huko vijijini. Ukiwakuta wale wazee wanatia huruma! Mimi nasema wametumikia Taifa kwa uaminifu kwa sababu kama wangukuwa ni wale wa Chukua Chako Mapema, sidhani kama wangukuwa na hali waliyokuwa nayo, wangukuwa wamejenga majumba, wangukuwa wame-invest vya kutosha na wangukuwa na maisha mazuri. Lakini walikuwa waadilifu na waaminifu ndiyo maana sasa hivi wanaathirika kwa hali yao duni. Kwa hiyo naiomba sana Serikali iharakishe kubadilisha kiasi hiki cha fedha mapema ili waweze kupatiwa fedha ambayo itawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inapobadilisha kiasi hiki, izingatie hali ya maisha ya sasa, isije ikasema tu tunatoka Sh. 21,000/= na sasa tunakwenda Sh. 40,000/= ikae iwe na *base*, iangalie kwamba hela hii tunayompa sasa hivi itamsaidia angalau kwa kidogo kile kimfikishe mahali fulani. Kwa hiyo, naiomba Serikali wazingatie hali halisi na gharama ya maisha ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Watumishi wa sekta binafsi. Mwaka jana Serikali ilitoa tamko hapa kuhusu kima cha chini cha mshahara, lakini sekta binafsi wengine waliendelea kutoa chini ya kima ambacho kimetamkwa na Serikali. Waliendelea kutoa hela ambayo wanataka wenyewe na Watumishi walivyojitokeza kudai kwamba Serikali imetutangazia kima cha chini ni hiki, walinyanyasika na hata wengine ilibidi wafukuzwe kazi kwa sababu wamedai haki yao ya msingi. Kwa hiyo, ningependa sana baada ya Serikali kurekebisha hiki kima cha chini pia ifuatilie kwa makini kwenye sekta binafsi ihakikishe kwamba kima kinachotamkwa na Serikali ndiyo

kima ambacho kinalipwa na Serikali na kinalipwa pia na sekta binafsi ili watumishi hawa waweze kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la Watumishi wa Umma ambao wamepewa dhamana kubwa sana ya kuwahudumia wananchi kwa moyo wote na hasa ninakwenda moja kwa moja kwa watumishi wa huduma za afya ambao ni Madaktari na Manesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuwahudumia wagonjwa ni kazi ya wito. Ni kazi ambayo yule ambaye ameamua kusomea na kwenda kuhudumia wagonjwa anatakiwa ahudumie kwa upendo, kwa ukarimu na kwa moyo utakaomwezesha angalau hata yule mgonjwa aweze kuridhika na ile huduma anayoipata, lakini kauli zinazotumiwa na hasa Manesi wa hospitali mbalimbali na hasa hospitali za Serikali ni bora hata hospitali za *Private*, zinasikitisha sana na zinatia huruma na nyingine zinaongezea hata wagonjwa maumivu zaidi ya pale waliyokuwanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Watumishi wamekuwa wanatoa maneno mengine ya kejeli kwa akina mama wajawazito kama vile nilikutuma, usitusumbue na kadhalika. Kauli kama hizo hazitakiwi kutamkwa na watu ambao wamekula viapo ambao wamekubali kwa nia yao kabisa kuhudumia wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na huduma zinazotolewa kwenye hospitali za Serikali, wananchi wanaamua kwenda hospitali za *private* kwenda kupata huduma kwa sababu wanajua watafika pale na watapokelewa vizuri na watapata huduma nzuri na iliyo bora. Lakini sasa ni wangapi wenye uwezo wa kwenda *private hospital*, ni wachache na hizi hospitali za Serikali zipo kwa ajili yetu sisi Watanzania ni lazima zihudumie. Kwa hiyo, tunaomba sana hospitali za Serikali hasa manesi na Wahudumu wengine wawe na kauli na lugha ambazo zinakubalika kwa sababu hizi kazi ni za wito wasije wakawakemea na kuwakoromea wagonjwa kwa sababu wako pale kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama mwanamke Mtanzania niliguswa sana na tukio la hivi karibuni mwezi huu wa sita mwanzoni la mwanamke mjamzito aliyefia kwenye hospitali ya Mwananyamala kwa sababu ya uzembe wa Manesi. Hili ni suala la kusikitisha sana. Mwanamke ni muumbaji anashirikiana na Mungu katika kuumba, lakini kitendo cha mwanamke huyu kufa kisa amekosa vifaa ambavyo havifiki Sh. 5,000/= inasikitisha sana, ukizingatia kwamba Serikali imeshatoa tamko hapa Bungeni kwamba huduma kwa akina mama wajawazito, huduma kwa watoto chini ya miaka mitano ni bure. Ni kwa nini mama huyu aachwe afe kisa eti alikuwa hana vifaa hivyo vya Sh. 5,000?/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Manesi palepale hospitalini walikiri kwamba ulifanyika uzembe na hata Madokta walisema kwamba uzembe ulifanyika na waliomba Serikali ichukue hatua ya kuunda Tume itakayofuatilia suala hili kwa makini na walikubali kutoa ushirikiano wa kutosha ilimradi tu ajira zao zilindwe. Walisema kwamba kumekuwepo na Manesi pale Mwananyamala, hospitali ambayo imekuwa ikilalamikiwa sana. Mimi mwenyewe nimewahi kwenda kuhudumia mgonjwa wangu

pale sitaki kusema hapa, lakini kwa kweli hali ya Mwananyamala inasikitisha. Kumekuwepo na Manesi ambao wamekaa pale muda mrefu, nadhani wamejenga kitu kama ngome, hawahamishwi na wamejenga jeuri. Kwa hiyo, ndiyo wanaoendesha mambo wanayotaka wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua sasa kwamba Serikali imefikia wapi kufuatilia suala hili? Kilichonishangaza kwenye tukio hili ni kwamba haraka walikurupuka wakaanza kutoa mafuta kwa ajili ya kusafirisha ile maiti kupeleka Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu lini utaratibu wa kusafirisha maiti na utaratibu wa kutoa mafuta unatolewa na hospitali. Huu utaratibu umeanza lini? Ni wangapi ambao wameshatolewa mafuta zaidi ya huyu mama, kama sio kuficha tu ushahidi? Pamoja na kutoa mafuta, waliwaziba midomo, lakini yote yalifahamika na taarifa ziko wazi. Tunaomba Serikali iunde Tume ili hospitali hii isafishwe. Hawa ambao wameshaota mizizi hapa waondolewe na iwe ni fundisho kwa hospitali nyingine ambapo kuna wahudumu kama hawa wanaotoa kejeli na wanaowaua wagonjwa kwa sababu ya kutokuwajibika na kutokutimiza wajibu wao kama Watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naomba kuzungumzia ni suala la upandishwaji wa vyeo, Serikali inatambia hapa kwamba wamepandisha vyeo, lakini kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri hakusema kwamba vyeo hivyo vimepandishwa watu gani au ni wapi. Tungependa Mheshimiwa Waziri atuambie kwamba katika hao watu waliopandishwa vyeo ambao haku-*specify*, waalimu ni wangapi waliopandishwa vyeo? Kwa sababu mwaka jana alitambia kwamba anategemea kupandisha Waalimu 38,505 vyeo ndani ya mwaka huu wa fedha. Leo hajatamka kwenye hotuba yake kwamba ni walimu wangapi waliopandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo kubwa sana la waalimu kwenye nchi yetu, kwa ujumla kila kona, Waalimu wamekuwa wakipangwa kwenye mashule hawaendi kwa sababu Serikali imekuwa haiwajali kikamilifu. Wakipelekwa huko vijijini wanasahaulika, mishahara ni midogo, hali ya maisha ni ngumu, hawapandishwi vyeo, matokeo yake wengine wanaamua kuondoka wanakwenda kukaa mijini, wanaona ni bora wauze maji ya kunywa, askrimu ili mradi waishi waepukane na ile hali ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linasababisha watoto wetu kukosa elimu bora na tukubali kabisa kwamba msingi wa maendeleo ya Taifa lolote ni elimu. Kwa hiyo, kama tusipowekeza kwenye elimu vizuri kuanzia kwenye ngazi za chini kwenye *primary schools*, tunajenga Taifa lisilokuwa na mwelekeo mzuri. Kwa hiyo, suala la Waalimu liangaliwe vizuri. Kwenye nafasi hizo tungependa kujua ni Walimu wangapi wamepandishwa vyeo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Watumishi kukaa eneo moja la kazi kwa muda mrefu. Hili limekuwa ni tatizo sana na hili limesababisha watu kujenga kiburi na kujenga uzoefu, kwa hiyo, wamebaki kufanya kazi kwa mazoea na hawafanyi kazi kwa kuwajibika. Kwa hiyo, naomba Serikali iweke mwongozo kamili kwamba mtu

atakaa kwenye kituo kimoja cha kazi na baada ya muda fulani ahamishwe, kwa sababu akihamishwa pale, kwanza anahamisha uzoefu wake wa kazi pale na anahamisha sehemu nyingine na hapo anakuja mwingine na pia anahamisha yale mazoea ya kukaa pale yanayomjengea jeuri kwa sababu anajua kabisa kwamba pale ni kama nyumbani kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano halisi wa huko kwetu Urambo, kuna Kijiji kinaitwa Mwendakulima, Kata inaitwa Mwendakulima kuna Mtendaji wa Kata alizaliwa pale pale, akapata kazi pale pale na amekaa pale kituo kimoja kwa miaka 17 yuko kwenye kituo kimoja. Yule Mtendaji alijenga jeuri ya ajabu, ilifikia hatua akang'oa na akauza hata mabomba ya maji yaliyokuwa pale mpaka sasa hivi, kile Kijiji hakina maji kwa sababu ya huyu mtu aliyekaa pale kwa muda mrefu. Matokeo yake ameleta hasara, wananchi wamekosa maji kwenye lile eneo na yeyote atakayeongea naye anasema mimi ni mzizi wa hapa, sing'oki. Ni kweli kwa sababu mtu kazaliwa pale, kasoma pale, kaajiriwa pale na miaka 17 anafanya kazi pale, unategemea huyu mtu atafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa amehamishwa, lakini hii iwe ni fundisho kwa Serikali kwamba Watumishi kama hawa wasiendeleo kuachwa eneo moja kwa muda mrefu, wanakiuka taratibu za kazi na pia hapo hapo wanakwenda kinyume na utaratibu na utendaji wanaotakiwa waufanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni suala la Watumishi wanaokwenda kujiendeleza shuleni. Kumekuwepo na tabia ya Serikali ya kutokutambua Watumishi ambao wanakwenda kujiendeleza shuleni kwa baadhi ya Wizara.

Kwa mfano, Mtumishi amekaa kazini akaamua kwenda kujiendeleza kwa nguvu zake mwenyewe kwa nia kwamba aweze kutoa huduma bora kwa wananchi kwenye kituo chake cha kazi, iwe amekwenda kuchukua *degree* ya kwanza au ya pili, lakini anaporudi kwenye kituo chake cha kazi anakuwa amekaa pale, pale alipokuwa hapandishwi cheo, hawi *re-categorization* pale na wala haongezewi mshahara.

Kwa hiyo, suala kama hili kwanza linakatisha tamaa kwa wale waliokwenda kujiendeleza elimu hiyo, kwa sababu hawakutambulika na hawaoni sababu ya wao kwenda shule. Pia inakatisha tamaa kwa watumishi wengine wale ambao wangependa kujiendeleza kama tunavyojua elimu ni msingi wa maendeleo ndiyo itakayolitoa Taifa letu hapa tulipo kwenda kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwatambua watu kama hawa tunawakatisha tamaa ya utendaji wa kazi na pia tunawakatisha tamaa wengine kutokwenda kujiendeleza kwa sababu wanaona wenzao wamekaa pale na hawana sababu ya wao kwenda kujiendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili lipo kwenye Wizara ya Kilimo na Ushirika na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wamekaa pale kwa muda mrefu na wapo wamekaa miaka minne na zaidi tangu wametoka vyuoni hawajafanyiwa chochote. Kwa kweli hili suala linatia huruma na tunaomba lifanyiwe kazi ili watumishi hawa waweze kuwa na moyo wa kufanya kazi na waweze kuendelea kulitumikia Taifa hili kwa uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nashukuru sana kwa kunipa nafasi, nasema ahsante.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nitamke mapema kwamba pamoja na yote nitakayosema ambayo sio lazima nikubaliane na hotuba iliyotolewa, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaunga mkono taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala. Juzi wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu, nilisema mambo mengi kidogo. Nafikiri yalikuwa mengi kiasi kwamba nilishindwa kumaliza. Kwa hiyo, naanzia pale nilipoishia. Nitaanza na suala la umasikini. Pamoja na juhudi zote na fedha zilizotumika kwa muda mrefu sana kuondoa au kupunguza umaskini, maoni yangu ni kwamba umaskini bado umekithiri licha ya takwimu mbalimbali tunazopewa kwamba uchumi umekua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nisingependa kuutazama umaskini kwa njia ya takwimu. Sisi tunaishi vijijini tunaona bila ya takwimu umaskini umezidi sana. Ziko sababu nyingi, mojawapo na wataalamu watakubaliana nami, kwamba ni kuongezeka kwa idadi ya watu. Wakati tunapata uhuru mwaka 1961 mimi nilikuwa na miaka kumi katika utumishi, tulikuwa na watu milioni 8.5, leo tunakaribia milioni 40. Kwa hiyo, ni kweli kwamba inawezekana juhudi mbalimbali zinazama na hazionekani kwa sababu ya wingi wa watu, lakini mimi naamini kwamba ziko sababu nyingine na sababu moja kubwa ninayoona mimi na ninasema baada ya kutathimini kwa uzoefu nilio nao wa miaka 58 katika utawala wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alitoa mifano mingi kidogo inayoonyesha mapungufu mengi tena makubwa katika maamuzi yetu ambayo yamesababisha adha nyingi na makosa mengi kwa sababu maamuzi hatukuyafanya wakati unaostahili na vilevile wakati mwingine tumefanya maamuzi yasiyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikumbushe tu, kosa moja ni lile alilotamka la reli (*TRL*). Ni kwamba kwa sababu *system* yetu ilitoa takwimu zisizo sahihi na sasa hivi tumefika hatua hili shirika japo limeanza lakini linatoa huduma mbaya sana. Hata katika Idara hii ya Utumishi, tumepanga kima cha chini, lakini hatukulipa, tumesema kima cha chini kiwe Sh. 100,000/= lakini hatulipi leo hadi baada ya miezi sita ijayo. Kwa hiyo, tumeweka kiporo. Huu sio uamuzi mzuri na kwa kweli ni kudanganya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uzoefu huo, mimi nadhani jambo moja ambalo linachangia sana katika mapungufu au udhaifu wetu ni mambo ya mfumo au miundo yetu. Jukumu la kuhakikisha kwamba mfumo yetu inafanya kazi iko chini ya idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, vijiji vyetu bado havijaweza kupanga na kutekeleza miradi yao kama ilivyokusudia wakati tunaanza *Decentralisation* au siku

hizi mnaita *D by D* ambayo mimi mwaka 1972 pamoja na *Mckinzie Inc.* ndiyo tulioanzisha na kutekeleza. Mimi kwa uzoefu huo ninaweza kusema kwamba bado hatujatekeleza hilo.

Kwa hiyo, umasikini bado utaendelea kuonekana kwa sababu tumeshindwa kutekeleza jambo ambalo ndiyo hasa lilikuwa kiini cha *Decentralisation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kuna tatizo moja ambalo mimi naliona nalo ni kwamba sasa hivi tuna *two parallel systems* za Serikali yaani Serikali Kuu inaishia kwenye Tarafa, kuna Makatibu Tarafa na sisi Serikali za Mitaa tunaendelea mpaka chini vijijini.

Mimi nasema utaratibu huu wa Serikali za Mitaa kulazimika kupanda farasi wawili kwa wakati mmoja, yaani Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni wa hatari na kwa kweli Makatibu Tarafa walio wengi, kwa uzoefu wangu, ni watu ambao hawana majukumu yanayoeleweka, kwa hiyo, wanaelea tu na mara nyingi ni chanzo cha migogoro na mapambano mengi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba ile Tume yetu ya Maboresho itazame na ifikirie upya suala hili la mtiririko wa Serikali kwa sababu inaleta utatanishi unapozungumzia Serikali za Mitaa na Serikali Kuu wakati ule ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niongeze kwamba hoja ya kwamba Makatibu Tarafa wanahusika na ulinzi na usalama siyo kweli kwa sababu kisheria Katibu Kata ndiye mwenye jukumu la kuangalia suala la Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala hili hili la muundo ambalo nimezungumza mara nyingi, lakini *system* yetu haieleki kuwa inasikia haya. Mfumo wa sasa katika Mikoa ni mbaya na kwa kweli ni mzigo kwa maana kwamba hauna tija hasa kwa sababu hakuna *linkage* kati ya *Secretariate* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, washauri hawa zamani walikuwa *Regional Heads*. Sasa baada ya kuwafuta katika vyeo vyao wanaitwa Washauri katika sekta zao. Ukweli ni kwamba, kisheria tumekiuka kwa sababu Wakuu hawa wanafanya kazi kulingana na sheria zinazotawala sekta zao.

Tuchukue mfano mmoja tu au miwili, *Regional Education Officer* anatawaliwa na sheria namba 25 ya mwaka 1978 pamoja na *amendments* zake na ndiyo kazi yake, lakini sasa kama mshauri hana nguvu ile ya kisheria ya kufanya kazi zake za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukua kwa mfano *Regional Livestock Officer*. Huyu vilevile ana uwezo fulani chini ya sheria inayotawala kazi yake. Anaweza akaweka karantini kama kuna magonjwa ya milipuko na kadhalika, lakini akiwa mshauri hana nguvu hiyo ya kisheria. Wako pia *Regional Cooperative Officers* wanaotawaliwa na sheria ya ushirika, lakini kwa sababu sasa siyo *Region Cooperative Officers* ni *Region Consultants* au kitu kama hicho, hawana uwezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri, kwa mawazo yangu, ukishafuta vyeo vyao, maana yake umeondoa madaraka yale kisheria inayotawala kazi zao. Nafikiri iko haja ya kutazama suala hili upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufutwa kwa vyeo hivi na kwa maelezo ambayo hayaeleweki sana ni ya jumla jumla juu ya kazi za *Regional Commissioner* na kazi za *District Commissioner* inaleta hali ambayo tunakosa *linkage* kama nilivyosema mwanzoni kati ya Mkoa na Serikali za Mitaa na mimi kwa uzoefu wangu wa miaka saba nikiwa Vijijini na miaka mingi nikiwa Serikalini ninaona kwamba hakuna kiungo kinaojulikana cha maana kutoka Mkoani unavyosaidia *District Councils*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Tume ya Maboresho ya Utumishi itakiwe kutazama upya na kusahihisha mfumo huu ambao mimi kama nilivyosema, siyo tu hauna *linkage* lakini pia una gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni mfumo wa Kanda. Pamoja na ubovu wa mfumo wa Mikoani, lipo tatizo la Kanda ambazo zipo katika baadhi ya Mikoa na Mikoa mingine iliyobaki ikitaka huduma ni lazima ifuate huduma hizo kwa Mikoa ile ambayo haina *Zonal Headquarters*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mifano kama vile elimu, madini, umwagiliaji na kadhalika, Mikoa kama Mkoa wangu mimi ambao hauna *Zonal Headquarters* ni lazima tufuate huduma hizi Mbeya na tukifuata huko mara nyingi tunaambiwa Bajeti imekwisha. Mkitaka tuje tufanye kazi hii, inaweza kuwa *inspection*, wanasema tupeni fedha kwa ajili ya nauli, malazi, posho na mambo kama hayo. Hii nafikiri sio sahihi.

Mimi nashauri utaratibu ufanywe ili kila Mkoa uwe na idadi inayostahili ya wataalamu ili tusiwe na matatizo haya ambayo tumelazimishwa kuyakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mara nyingi katika vikao mbalimbali hata mwaka jana nimeongelea suala hili, lakini naona majibu hayatoshelezi na kwa hiyo, nitaendelea kupiga kelele. Niseme wazi kwamba kama tutakwenda na mwendo huu, tija ya watumishi wetu itazidi kupungua na itakapopungua ni sisi wenyewe wa kujilaumu na hasa idara hii kama haiwezi kuchukua hatua ni lazima ihakikishe kwamba mifumo inayowekwa ni ile ambayo itaongeza tija na itakayokuwa rahisi kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo machache, najua muda umepungua, naomba niishie hapa, Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Galinoma. Sasa namwita Mheshimiwa Said Amour Arfi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir na Mheshimiwa Col. Feteah Saad Mgeni ajiandae.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda nijikite sana mchango wangu katika eneo la utawala bora. Pengine pia nitagusia masuala ya Utumishi, lakini tunapoitazama dhana ya utawala bora ni pana sana ndiyo maana wakuu wa nchi za Kiafrika, waliamua na wakatoa azimio la nchi ziweze kujitathmini na kutathiminiwa katika maeneo yanayohusu utawala bora katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuangalia suala la utawala katika huduma. Pamoja na kwamba sasa hivi Wizara imetoa mikataba ya huduma kwa wateja, lakini bado hawajafanya tathmini kama mikataba hiyo kweli inatekelezwa ipasavyo. Lakini ili mikataba hiyo iweze kutekelezeka, huduma sahihi itolewe kwa wateja, kuna vitu vya msingi ambavyo ni lazima viangaliwe na Serikali.

Kwanza, ni kwa wale watoa huduma. Mishahara wanayopata watumishi wa Serikali na hususan watumishi katika kada za chini haitoshelezi. Mishahara ni midogo, inawavunja moyo watumishi na hata pale wanapowekeana mikataba ya kutoa huduma kwa wateja wanashindwa kutekeleza kwa sababu hakuna kichocheo cha kuwafanya wafanye kazi kwa ufanisi zaidi. Mishahara ni midogo, na tofauti kati ya mishahara inatisha. Kundi la viongozi linachukua sehemu kubwa ya mapato ya Taifa letu kuliko wafanyakazi wakati soko tunalokwenda ni lile lile. Lakini bado hatuwafikiria kuwaongezea kima cha chini cha mishahara wafanyakazi wa ngazi ya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakaa bila kuangalia suala la kuweka motisha kwa wafanyakazi hata hiyo mikataba kufaulu kwake itakuwa kidogo sana. Huo ulikuwa ni wasiwasi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika kidogo angalau sasa hivi wanafikiria hata kuongeza posho hizo za Madiwani kama alivyotangaza hapa katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini nilikuwa najaribu kuangalia kabla ya tangazo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wizara Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ilikuwa imetangaza kima cha chini cha mishahara kwa mfanyakazi wa *Bar* au wa nyumbani ni Sh. 80,000/= wakati Diwani wake anayesimama mabilioni ya fedha za Serikali alikuwa anapata chini ya Sh. 80,000/=. Sasa nikawa ninashangaa sana Serikali ambayo inamfikiria kumwongezea mishahara mtumishi wa nyumbani kima cha mishahara ambacho hata Diwani hapati.

Lakini bado suala la kuangalia maslahi ya wafanyakazi kwa ujumla wao na kupunguza hii tofauti kati ya wafanyakazi wa ngazi ya juu na wa ngazi ya chini ni lazima Serikali sasa ikae na hata ikiwezekana kwa hatua za makusudi kabisa na kuwasimamisha hao ambao wapo juu wasimame walipo na kuwasogeza hao waliopo chini ili angalau wasogee mahali waweze kukabili hali ya ugumu wa maisha yalivyo katika nchi yetu. Hilo lilikuwa ni eneo moja la kuangalia suala la mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni lazima pia tujipime, ni lazima tufanye tathmini juu ya hao hao wafanyakazi. Wafanyakazi wa Watanzania wanalipwa mishahara kwa kwenda kazini na siyo kwa kufanya kazi. Kwa maana hiyo, ni kwamba tutabakia tumesimama hapo hapo tulipo na wanazo sababu, hao wafanyakazi, wala mimi

siwalaumu kwa kulipwa kwenda kazini. Ni lazima watafute muda wa ziada ndani ya muda wa kazi ili watafute njia yoyote ya kujiongezea kipato ili waweze kukidhi ugumu wa maisha. Sasa hivi ni lazima tuangalie kwamba mishahara inayotolewa inalingana na kazi wanazozifanya watumishi na wafanyakazi watafanya kazi kwa bidii tu kama hali ya mishahara itaboreshwa kama nilivyotangulia kusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ili uweze kusema tuna utawala bora ni pamoja na kuziangalia huduma zinazotolewa kwa jamii. Unapowakuta watoto wamekaa vituo vya *Bus* wanahangaika, wanasukumwa wanachelewa kufika shuleni katika muda unaotakiwa na ukasema una utawala bora mimi ninatilia mashaka. Huduma za Jamii ambazo ni za msingi zinapaswa zitolewe na Serikali. Serikali inajiondoa, taratibu na kutaka huduma hizo zibebwe na wananchi. Leo tunawalaumu watu wa daladala kwamba wanawanyanya wanafunzi.

Vijana wetu wanahangaika katika vituo vya mabasi, lakini Serikali imefanya jitihada gani ya kuondoa tatizo la kero ya usafiri kwa wanafunzi? Bado huyo mwenye daladala unataka umlazimishe atoze mwanafunzi nauli ya Sh. 50/=, tunamwonea huyo *operator* wa daladala.

Hilo ni jukumu la Serikali na pia ni jukumu la mzazi kuhakikisha mtoto wake amekwenda shule na siyo jukumu la daladala *operator* ambaye tunataka kumkandamiza. Unampangia bei, lakini unashindwa kusaidia kumsimamia kwenye bei ya mafuta. Mafuta yanaongezeka bei, lakini wewe unataka kumlazimisha amchukue mwanafunzi kwa nauli ya Sh. 50/=. Serikali haina mpango wowote wa kusaidia kuondoa kero ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi inanisikitisha sana ninapowakuta watoto wamekaa wakihangaika wakisukumwa mpaka usiku. Ninatilia mashaka sana kusema kwamba nchi yetu ina utawala bora. Kama hatuwezi kuwafikiria hao wasiokuwa na sauti, hao watoto wanaonyanyaswa kwenye vituo vya mabasi, ni lazima lipo tatizo. Serikali ijaribu kubeba majukumu yake, isiyapeleke majukumu yake ya msingi kwa wananchi.

Kwa mfano, tumeweka mamlaka, Serikali inajitoa inapunguza majukumu yake, inatengeneza mamlaka kama zilivyoainishwa ndani ya kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, zipo zaidi ya mamlaka 29 sasa hivi Serikali inajitoa inaziachia mamlaka zisimamie. Lakini: Je, Serikali inafanya tathmini kuona mamlaka hizo zinatekeleza majukumu yake ipasavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, zipo mamlaka zinazosimamia wakandarasi wa ujenzi wa majengo au barabara au kitu chochote, ipo mamlaka inayowasimamia wahandisi, majumba yanaanguka, ripoti iliyoletwa hapa inatia huzuni. Takwimu zinasikitisha, Serikali muda wote huu imefanya nini katika kutathmini Wakala wake wanafanya kazi gani? Kuna mapungufu gani ndani ya hizo sheria zilizounda mamlaka hizo zikashindwa kusimamia kazi zao ipasavyo? Hayo ni mapungufu ambayo Serikali inatakiwa iyatazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia suala la nauli za wanafunzi. Utakuta kuna Mamlaka ya *SUMATRA*, kuna mamlaka ya *EWURA*, lakini mipaka ya *EWURA* inahusu maji na umeme na wale wengine wanahusika na usafiri wa nchi kavu na usafiri wa majini. Hakuna mamlaka inayodhibiti bei, lakini bado mamlaka hizo zinataka kuwapangia bei hususan wasafirishaji. Wanawaonea! Hao wanakandamizwa kwa sababu hakuna chombo kilichotengenezwa na Serikali kitachoweza kudhibiti bei katika nchi yetu. Wameliachia soko holela liendeleo kuwa holela. Vinginevyo hawa mtawatoa. Hilo lilikuwa ni eneo moja.

Eneo lingine ambalo nilikuwa napenda nilizungumzia ni eneo la pensheni. Mheshimiwa Waziri hakugusia chochote kuhusu pensheni. Wazee wetu hao wamefanya kazi kwa muda mrefu, lakini leo wazee hao ndiyo wenye kutaabika, wanasukumwa, wanadharauliwa, hakuna mtu anawaangalia, inafikia mahali wazee hao wanajikusanya wanakwenda Ikulu. Nilisikitika sana pale nilipowasikia wazee wanasema hakuna mahali pa kimbilio la mwisho isipokuwa Ikulu na leo katika viwanja vya Ikulu tunafukuzwa. Nani wa kuwasikiliza hao wazee? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni wanayopata ni ndogo, hakuna mahali popote ambapo kunaonekana kwa makusudi kabisa Serikali inafikiria namna ya kuondoa kero na matatizo ya wazee hao. Juzi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi hapa alisema mtu aende mmoja mmoja hataki makundi kwa sababu hakuna kumbukumbu. Ni Serikali gani ambayo inashindwa kutunza kumbukumbu zake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifuatilia mafao au mirathi ya wafanyakazi katika nafasi zetu kama Waheshimiwa Wabunge, tunapata matatizo makubwa. Kama Mbunge unaingia katika Ofisi ya Serikali jalada la mfanyakazi linatafutwa kwa muda wa siku tatu halijaonekana, sembuse huyo mtu mwingine! Bado anaambiwa aende akamwone Waziri, nauli ya kutoka Mpanda mpaka kwenda Dar es Salaam ni zaidi ya Sh. 70,000/= huyo mzee kipato anachokwenda kuchukua Dar es Salaam ni Sh. 21,000/= hujamsaidia mzee huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali sasa iangalie na itengeneze utaratibu ambao hao wastaafu pamoja na sisi viongozi kesho tutakuwa wastaafu, tutaingia katika kundi hilo hilo, tutasukumwa pale Hazina. Ukienda Hazina utaona ni namna gani Utawala Bora unavyopuuzwa. Ni lazima utengenezwe utaratibu utakaondoa adha na kero na hususan kwa hao wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utengenezwe utaratibu pia wa mafao yao yalipwe kwa wakati wasisumbuliwe. Kwani Serikali hivi haijui kwamba mfanyakazi wake fulani atastaafu wakati fulani ikamtayarishia mafao yake? Mtu huyo anasumbuliwa, anahangaishwa, anakimbilia kwa Mbunge, anakwenda kukopa kuwa ana watoto wanasoma, anashindwa kulipa karo kwa sababu ya urasimu uliopo ndani ya Serikali. Ni lazima sasa jitihada za makusudi zifanywe kuhakikisha kwamba urasimu huo unapunguzwa. Ukipunguzwa kero na manung'uniko ya wananchi kwa Serikali yatapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani wakati ule ndugu zetu walipokuja na kauli ile ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya nikahisi kwamba mambo yatakwenenda kwa kasi kama walivyohidi. Lakini kila siku tunasikia subiri, tushubiri, vuta subira, vuta subira. Imebadilika kutoka kwenye Kasi Mpya imekwenda kwenye vuta subira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Said Arfi, ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, atafuatiwa na Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni na Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama ajiandae.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuungana na wale wote waliotoa shukrani kwa hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala mawili ambayo nitajikita zaidi. Suala moja ni suala la mshahara wa kima cha chini, lakini la pili ni suala la wastaafu. Inawezekana lingine likatoka nikiwa njiani.

Mheshimiwa Mama Hawa Ghasia kuna njaa Tanzania. Kuna njaa ya kipato, kuna njaa kwa wafanyakazi hasa wa kima cha chini. Leo baada ya hotuba hii kutolewa, naelewa sio kwamba sielewi lakini nilikwenda Marikiti pale nyie mnaita Soko sisi tunaita Marikiti nikipitapita nikaangalia vitu vinavyokwenda vipi kabla sijajiandaa kuja kuchangia, Mheshimiwa Waziri pale mchele kilo Sh. 1,300/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mboga wanasema sisi kwetu tunaita kitoweo, kule kilo Sh. 3,000/=. Ukija katika mkaa kikopo kimoja Sh. 500/=. Mimi katika hesabu zangu za haraka haraka nikaichukulia familia ina watu watatu, baba na mama katika familia hiyo yumo. Hesabu zangu za haraka haraka nikakuta kwamba familia hii atahitajika kutumia Sh. 6,000/= kwa siku wala huna ujanja isipokuwa atumie Sh. 6,000/= kwa siku.

Waheshimiwa Wabunge sisi tuliomo katika Bunge hili hapa tulipo tunajijua, tunapiga kelele lakini tunajua vile vile wafanyakazi wa Serikali wanapiga kelele pamoja na hao wanaolipwa kima cha chini cha Sh. 100,000/= wanachotaka kulipa. Hii Sh.100,000/= utaitumia vipi kwa mwezi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sh.100,000/= panga, pangua utaitumia vipi kwa mwezi ikiwa nasema leo nimekwenda wala sio jana wala juzi nakuta matumizi kwa siku moja inawezekana kwa mlo mmoja Sh. 6,000/= utatumia. Sisi tumekuja hapa tumechaguliwa na tuko hapa kuwawakilisha wananchi asilimia 90 ya sisi tuliopo hapa ni waumini wa dini ama ya kikiristo ama ya Kiislam, tuseme kweli kweli tunafanya kazi tuliyokuwa tumetumwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, hii bajeti yake Wizara hii aipunguze, akate fungu la 20 na fungu la 30 kwa maana kwamba hizo fedha ziletwe katika bajeti ya kuwasaidia hawa wa kima cha mshahara wa kima cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kama inawezekana na Serikali inatusikia, kupitia kwako, Naibu waziri wa fedha yupo, hapa ningeshauri zile *entertainments allowances* zote zikatwe na zikusanywe ziletwe ili kusaidia kima cha chini cha mshahara. Njaa kama iko katika nchi hakuna (*stability*) utulivu kabisa. Jeshi litageuza, Polisi watageuka kama wanavyogeuka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyokuambia nimepigiwa simu kutoka Jimboni kwangu kuna njia inatengenezwa barabara miaka mingi inapigiwa kelele Mishelishelini – Mchangani, kuna jamaa wamekatwa wanaiba dizeli ambayo ya kuendeshea *bulldozer* kwa ajili ya kutengenezwa barabara ndani ya wale waliokamatwa mmoja ni askari anawalinda wezi waendeleo na kuiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali itakapofika hapo unakuta ndiyo suala tulizungumza la maadili yanapotea siri za Serikali/nyaraka zinaibiwa watu hawafanyi kazi kama walivyosema walionitangulia hapa wanakwenda kuonekana kwamba wako kazini, lakini hakuna kazi inayofanyika. Hiyo ni kishawishi tosha cha kwamba mimi napata mshahara wa Sh.100,000/= ni *office attendant* anakuja mtu anataka nyaraka ananipa shilingi milioni tano ambazo mimi sijaziona katika maisha yangu, hivi mimi nina moyo kiasi gani wa uzalendo nisimpe nyaraka hizo? Sasa anayehatarisha hilo ni nani? Ni yule mwizi ama ni sisi?

MBUNGE FULANI: Serikali!

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Serikali. Tunaelewa kuna nchi ya *Georgia* askari walisimama wakawa hawalindi, jeshi halifanyi kitu Serikali hawafanya kazi, watu wakaingia njiani kwa sababu ya kwamba Serikali imeshindwa kutekeleza yale yote tunayoyazungumza kila siku.

Hapa kila siku sisi tunapiga kelele kuna hili, kuna hili hakuna kinachotekelezwa. Mheshimiwa Hawa nakuomba bajeti ifumue kima hiki cha Sh. 100,000/= kiondoke hatuendi, tutavuruga kabisa nchi hii na tusiwalaumu watendaji, tusiwalaumu watu wote hata iwe uko vipi. Kwanza huwezi kuiba kama uko peke yako, wanaiba wote asili ya ushahidi kupatikana na watu kuelezwa ni kwa sababu kuna watu ambao wanawaona. Sasa hawa watu wanaowaona hawa ndiyo wanaotoa taarifa. Hawa watu wanaona wanaiba ndiyo hawa nao wanaotaka kuiba vile vile. Wanasema: “*Idha kana labul-baita ya dufu munnan fashum alal haulat*”, anasema ikiwa baba wa nyumba anapiga ngoma watoto wanafanya nini, wanacheza. Kwa hiyo, ikiwa sisi watendaji katika Serikali tunapiga ngoma, waliobakia watacheza tusiwalaumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepiga suala hili tulisikie na tunasaidie watu wananuka njaa, unakwenda Jimboni wewe unamwangalia mtu, macho anayokuangalia, basi unaogopa! Sasa kama tutaendelea hivi nadhani tufike wakati sasa hivi tunapotembea mitaani tusivae makoti haya kwa sababu ukivaa koti ukijulikana Mbunge, huyu Waziri, watu watasema ehee, sasa hapa hapa napata.

Kwa hiyo, kama kuna uwezekano kuanzia sasa hivi tuingie na mashati humu Bungeni badala ya kuvaa makoti, sio hivi katika hali hii tunavyokwenda, kuna hatari kubwa inayotukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja tena katika suala la pensheni. Nguruwe alimwambia mamaye domo hilo, nguruwe mzazi akasema ndiyo unakokuja huku na hili domo na wewe litakufika hili hili! Maana linakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kijana mdogo mdomo wako mdogo, lakini sasa domo unashangaa la kwangu mimi, litakua! Sisi tupo hapa pamoja na wenzetu walioko Serikalini kama suala hili la pensheni hatutalisimamia ipasavyo leo, sisi tumeajiriwa, lakini kesho tutakuwa wastaafu waliokuwa wastaafu leo jana walikuwa waajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tungejipanga mapema tusije tukafika mahali hasa watendaji kazi Serikalini waliokuwa na dhamana hizi za kupanga na kupangua kuweka *sealing*, kuweka hii, fanya hii, hii usifanye mnakuja na ninyi.

Kwa hiyo, yatakapokufikieni msije mkalaumu, ni vizuri kwamba, hili litengenezwe sasa hivi kabla ya domo halijawafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimeeleweka na kama nimeeleweka, mimi nimesema nitachangia hoja mbili, moja ya pensheni na ya pili ya njaa, mshahara wa kima cha chini ala ala, chonde chonde, sisi kwetu tunasema ala, ala, nadhani wengi wengine hatufahamu. Lakini chonde chonde, mambo haya yakiharibika juu ya mgongo wa Waziri tutamfuata tumwambie je, umeyaona haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kisha nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi kuchangia mawili, matatu.

Sina budi vile vile kumpongeza Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchagua timu safi sana timu ambayo nina hakika inafanyakazi vizuri. Mimi nina uhakika kabisa akiwa yeye ndiyo nahodha atalisafirisha jahazi hili na litavuka mwaka 2010 kwa salama na ushindi wa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wote walio katika Ofisi ya Rais, pamoja na menejimenti ya utumishi kwa hoja nzuri waliyotuletea ambayo nina hakika pamoja na michango tutakayokuwa tunachangia, basi itakuwa nzuri na nina hakika kwamba italetu manufaa na maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakuja katika suala la hali ya maisha. Tunazungumza haya na kila anayesimama atazungumza hilo kwa sababu ndiyo jambo la mwanzo linalomfanya mtu awe na imani kama tulivyosikia kwa baba wa Taifa imani huzaa imani pale ambapo tutakapoifanya.

Naipongeza Serikali kwa kuongeza mshahara na kuwa Sh.100,000/= kwa wafanyakazi wa kima cha chini. Lakini mimi naamini kwamba Serikali hiyo ilipofikiria hayo inaelewa wazi kwamba kima hicho hakitoshi, lakini kutokana na hali ya uchumi inavyokuwa basi tuanzie hapa.

Sasa basi kama ndiyo hivyo na mimi naungana nayo na hivyo bado itakaa kwa huruma zile zile ilivyokaa ikaongeza kima cha chini Sh. 100,000/= itakaa tena iongeze zaidi. Naamini Serikali siyo mtu, Serikali ni chombo lakini chombo hicho kinaongozwa na watu, ni chombo kinachoweza kutumia mabavu pale panapobidi kutumia mabavu, lakini vile vile ni chombo kinachotumia hekima busara pale panahitajika kutumika busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa zitatumika busara kuwaona hawa wanyonge hawa wafanyakazi wa chini wanyanyuliwe kipato chao nao wajisikie kama wako katika Taifa lao huru linaloongezeka uchumi mwaka hadi mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naizungumzia Taasisi yetu ya Rushwa, mimi naipongeza. Naanzia kuipongeza kwa sababu inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmojawapo katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ninaiona juhudi zake kwa sababu sisi wenzenu mmetuteua tuvishughulikie vyombo hivyo, tuwe navyo vyombo hivi vinatuletea taarifa nzuri tu, tunaijua inavyofanyakazi na inafanya kazi kweli. Lakini inahitaji kuimarishwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyotupa jicho letu katika kuimarisha *intelligence* yetu na sasa tutupe macho katika kuimarisha TAKUKURU yetu, TAKUKURU ina jukumu kubwa kwa sababu haishughulikii tu rushwa lakini inawajibika kushughulikia matatizo kadhaa yanayosababisha uchumi wa Taifa kuudondosha chini. Mfano, hivi sasa kumeingia hawa waharibifu wa uchumi wa Taifa.

Tunasikia kwenye vyombo na sisi wenyewe tunazungumza hapa, *transforma* zinaibiwa mpaka mafuta na zikiibiwa mafuta maana *transforma* zile zitalipuka, nyaya za umeme zinaibiwa, vyuma vya reli vinaibiwa.

Sasa haya ni mojawapo katika majukumu ya TAKUKURU ione ishughulikie ifike wakati ipate taarifa kwa sababu hii ni sehemu ya kinga si sehemu ya tiba. TAKUKURU

maana yake ielimishe ifanye kazi ya kuelimisha kabisa kujua kwamba tunapoharibikiwa Taifa ndivyo linavyoharibikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa rai kazi hii ya kupambana na rushwa sio kazi ya Taasisi ya Rushwa peke yake, ni kazi ya kila mwananchi na hasa kila mzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ndiyo nafikiri sasa umefika wakati lianzia tangu watoto wetu wa shule kuelimishwa namna rushwa ubaya wake, hasara zake na ubovu wake na vipi linavyofika mahali kuliangusha taifa katika suala la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kuwaelimisha watoto wetu kuchukia rushwa na wizi mdogo mdogo wa kunyang'anya, watakuwa na imani, upendo wa Taifa lao, watakuwa watoto wazuri na Taifa litakuwa safi kabisa hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za Ulaya Mashariki, hasa kwa nyakati zile za nyuma, ilikuwa kama Uchina, Ujerumani ya zamani, *GDR*, Urusi na nchi nyinginezo, nasema Ulaya ya Mashariki wakati huo; kama utaiba sindano tu au utafanya ufisadi unaofikia gharama ya sindano, sasa haya wamefuzu vipi? Wamefuzu kwa sababu wameanza kutoka chini mpaka kufika juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana kwamba, elimu ya rushwa pamoja na kazi inayofanywa iongezwe bidii na ninaamini tutapata Taifa safi kabisa huko mbele.

Sasa nazungumzia hili suala la kuibiwa nyaraka. Kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba ni kule kutoweza kujitosheleza wale wafanyakazi wetu, tukiwatosheleza vizuri na kuwapa mafao mazuri, ninaamini kabisa suala hili halitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia katika kumalizia, mimi nilikusudia kuzungumzia maneno matatu haya; nazungumzia zaidi suala hili la kumaliza rushwa. Nitarudi tena kwa sababu nilisikia wachangiaji wa mwanzo; Mheshimiwa Masilingi hapa na Mheshimiwa Zitto walizungumzia kwamba, pamoja na hayo kuna matatizo madogo katika chombo chetu hiki. Sasa kama yapo basi hili litakuwa doa. Sifa hizi zote zitaharibika kama chombo hiki hakitasafishwa. Hii ni kazi kupitia kwako Mheshimiwa Waziri na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, ahakikishe kwamba anasafisha. (*Makofi*)

Huwezi kumkemea mtoto wako kwamba mchafu, hukogi, unanuka ikiwa wewe mwenyewe umeoza. Sharti ujisafishe wewe, uwe safi na ndipo utakaposikilizwa. Mashehe wetu husema kwamba, ninawausieni ninyi pamoja na kujiusia mimi mwenyewe katika kufanya mema. Maana yake na yeye mwenyewe katika kundi lile ajisafishe awe mzuri, awe safi na ndipo atakapoweza kumlaumu na kuweza kumkosoa yule ambaye amefanya kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumzia mwanzo, chombo hiki safi, kizuri, tusikubali kuona madoa madogo madogo. Haya yote yanawezekana na kutekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia juu ya mia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kanali Feteah Saad Mgeni. Sasa namwita Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Yussuf Mohamed na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa ajiandae.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba hii ya Waziri wa Utumishi wa Umma. Nianze kwa kuwapongeza Mawaziri; Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, Wafanyakazi wote wa Wizara hizo, Ikulu na Taasisi zake, kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mimi binafsi naridhika kwamba, Mheshimiwa Hawa Ghasia ni kati ya Mawaziri wanaofanya kazi vizuri, kwa ubora wa hali ya juu na viwango vya hali ya juu kabisa. Vilevile ni mjasiri na mbunifu na mimi naamini kwamba, Wizara ile ipo mahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu *concept* ya Utawala Bora. Kwa wananchi wetu walio wengi, wanaona kuwepo kwa Utawala Bora ni kupata huduma nzuri kutoka Ofisi za Serikali na Taasisi za Umma, kupata mahitaji yao ya msingi, kuona huduma zipo karibu na kuona huduma za dola zipo karibu nao. Sasa hapa nataka mimi nitoe maoni yafuatayo:-

Mwananchi wa kijijini ambaye hapendi kuchukua sheria mkononi, anategemea kwamba, kitakuwepo Kituo cha Polisi ambapo anaweza kwenda kupeleka taarifa za uhalifu. Pia itakuwepo Mahakama ya Mwanzo ambapo anaweza kwenda kupata huduma ya kimahakama. Kule kwetu Lushoto na maeneo mengi, huduma hizi zipo mbali sana na wananchi. Mahakama za Mwanzo pale ambapo zipo hazina Mahakimu. Wenzetu wa Sheria hutukumbusha kwamba, ukichelewesha haki ni sawa na haipo; na Utawala Bora ni pamoja na haki kupatikana kwa haraka na kwa viwango.

Wananchi kwa kutaka Utawala wa Sheria, wamejenga Vituo vya Polisi, lakini maboma yale waliyoyajenga kama kule Mkuzi, kule Mlola yako tupu, maana hayana askari, kilomita 75 - 100 kutoka Kituo cha Polisi, Utawala Bora unakuwa mgumu katika hali ya aina hiyo. Kama mambo haya hayaangaliwi vizuri, Utawala Bora ambao mimi nauona ni sawa sawa na maisha bora, utachukua muda mrefu kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza kwa muhtasari kuhusu hilo, nizungumzie huduma na maslahi kwa wastaafu. Wabunge wengi wamezungumzia sana kuhusu suala hilo kwamba, mstaafu anapostaafu kwa mshahara wa kiwango fulani, akapewa pensheni, labda miaka 20 iliyopita, wakati ule pensheni ile kwa maana ya *value for money* ilikuwa inakidhi haja. Kwa mfano, nilipokuwa nikifanya Serikalini mwaka wa 60, Ofisi ya PC wa Kikoloni nikilipwa shilingi 215 kwa mwezi zilikuwa pesa nyingi sana, nazitumia sizimalizi. Sasa wakati ule ningelipwa pensheni, leo sijui ningelipwa shilingi ngapi? (*Makofi*)

Mimi nilidhani Serikali ingefanya marekebisho kwamba, pensheni wanazolipwa wastaafu wa vyeo mbalimbali wa ngazi mbalimbali, ziwe na uwiano na mshahara wa leo au pensheni ya anayelipwa leo. Serikali imefanya hivyo kwa Viongozi wa Kisiasa, Rais na wengine na baadhi ya Viongozi wa Taasisi. Kwa kuwalipa pensheni asilimia 80 ya mshahara wa kiongozi wa ngazi ile ile aliyepo madarakani. Sisemi hivyo kujipendelea, maana mimi nilikuwa Katibu Mkuu kwa miaka mingi. Hoja hapa ni kwamba, pensheni ninayolipwa iwe na uwiano fulani na mwenzangu ambaye amestaafu jana. Maana siamini kwamba yule aliyestaafu jana ana mahitaji makubwa ya maisha kuliko yangu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huo ni ushauri kwa Serikali. Serikali itazame uwezekano wa viwango vya pensheni zinazolipwa wastaafu wote viwe na uwiano. Pensheni za leo kiwango cha chini cha mshahara, kimezungumziwa Wabunge wengi kwamba, hivi kweli huyu mtumishi ambaye hawezi kukidhi mahitaji ya familia yake; atakuwa na ufanisi? Kuna mifano hapa tukiitoa itakuwa inashangaza. Katika baadhi ya maeneo, wapo wafanyakazi wa ngazi ya chini wa vyombo vya dola ni wafanyabiashara wakubwa. Sasa unashangaa huyu ana-*balance* vipi kati ya kazi hii ya dola na biashara zake. Maana utakuta ana viduka, ana *viosk* 20, lakini inawezekana anafanya hivyo hana jinsi. Angekuwa na *option* ya kuiba au ya kuchukua rushwa akaona bora ajishughulisha. Lakini je, anapojishughulisha na biashara huduma kwa jamii zinaboreka au zinanakuwa na upungufu? Je, huo ni Utawala Bora? Mimi naishauri sana Serikali kama haitaweza kwenye bajeti hii itafute namna za kuweza kuboresha kima cha chini cha mshahara na mishahara kwa ujumla miaka inayofuata.

Ndugu Mwenyekiti, nizungumzie suala la Utawala Bora ngazi ya Kijiji, ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa. Unapokuwa kule Kijijini unaweza kushangaa, kweli maeneo mengi Utawala Bora haupo, maana elimu ya Utawala Bora haipo. Uelewa wa Utawala Bora haupo. Hawa Watendaji wa Vijiji ndiyo hao hao, Wenyeviti wetu hata posho hawana. Hawana mafunzo ya majukumu yao, mradi ameshapigiwa kura basi.

Mimi nilidhani Serikali yetu ifikirie kuimarisha mafunzo katika ngazi ya Kata, Tarafa, Wilaya na hata Mkoa. Vilevile baadhi ya watumishi katika maeneo haya, wanakaa muda mrefu sana kiasi kwamba, sasa wamejenga mazoea. Mimi nilidhani kwamba, iwepo *rotation* ya mtumishi na iwe ya uhakika; mtumishi asikae katika kituo kimoja kwa zaidi ya miaka mitano ili kuondoa mazoea.

Lingine, kule ngazi ya Vijiji na hata Kata, vikao haviratibiwi. Michango ya wananchi haisimamiwi, mapato na matumizi yanaenda kombo. Mimi nashauri kwamba, Serikali iweke utaratibu madhubuti wa kuratibu vikao vya ngazi zile za Serikali, kuimarisha Utawala Bora. Uwepo utaratibu wa kuhakikisha kwamba michango ya wananchi, mapato na fedha za Serikali, matumizi yake yanasimamiwa vizuri. Hapa naishauri Serikali kwa dhati kabisa kwamba, baada ya kukubali kuboresha malipo kwa Madiwani, basi Serikali ifikirie ikiwezekana mwaka huu, angalau kuwapa Wenyeviti wa Vijiji posho ili wasishawishike kudai kwa wananchi malipo ya vificho wanapotoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo tu suala la ufisadi; ufisadi Serikalini na ufisadi katika Taasisi za Umma. Mimi nadhani tatizo la kutokuwa na uzoefu, tatizo la kutokuwa na taaluma katika maeneo ya kazi, tatizo la kutokujiamini na tatizo la kutojilimisha na sheria na kanuni za maeneo hayo ya kazi na tatizo kubwa sugu la nidhamu ya woga. Vinachangia kufanikisha ufisadi katika taasisi za umma. Kuna Wabunge wenzangu hapa walikuwa Makatibu Wakuu, walikuwa Mawaziri. Sisi wakati wetu na siyo kwamba tunajisifu, tulikuwa tunawaheshimu sana Viongozi wetu wa Kisiasa, Mawaziri wetu na tuliwaheshimu sana sana na tuliwasaidia sana kuwapa ushauri sahihi. Akileta maagizo Katibu Mkuu tenda hili, tunasema sawa Mheshimiwa Waziri. Tunalifanyia kazi. Tunaangalia Sheria inayosimamia eneo lile; kuhakikisha imezingatiwa na madhumuni ni sahihi. Bajeti ipo na kila kitu kiko sawa, tunatekeleza.

Ikidhihirika maelekezo hayo hayakidhi matakwa ya Sheria, Kiongozi mhusika hushauriwa ipasavyo. Mimi nakumbuka katika Wizara ambayo nimefanya kazi, hata Mheshimiwa Rais aliwahi kuagiza, tukajua kwamba ameagiza kwa nia njema, lakini tukabaini kwamba, maagizo yale hayakidhi matakwa ya Sheria. Tukaenda na Waziri wangu kwa Rais, Mheshimiwa Rais umeagiza hili lakini ona Sheria hapa itavunjwa, ona hapa madhara ni haya. Mheshimiwa Rais akatuambia na Waziri wangu, nawashukuru mmenisaidia sana.

Sasa naomba Watendaji Wakuu wa Serikali na Taasisi zao, wasaidieni Mawaziri, msaidieni Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba, yale yanayoagizwa hayavunji Sheria za nchi, hayavunji Katiba na hayavunji Kanuni ambazo tumejiwekea wenyewe. Kwa hiyo, nawashauri hilo kwamba, msiwe na nidhamu ya woga; muwe na nidhamu ya hali ya juu, lakini si nidhamu ya kutomshauri kiongozi wako pale ambapo unaona maagizo yataleta kasoro na kuharibu sifa ya nchi yetu.

Mwenyekiti, lingine haraka haraka ni mashauriano kati ya Wabunge na Wakuu wa Mikoa. Mimi nadhani kwa muda mfupi ambao nimekaa katika Taasisi ya Bunge, nimeona kwamba, Mbunge ni mdau muhimu sana; ndiye mwakilishi wa wananchi na anajua matatizo ya wananchi na matarajio yao. Sasa inapokuwa hakuna utaratibu rasmi wa Wakuu wa Mikoa kukaa na Wabunge wao kushauriana matarajio, matatizo ya Mikoa, Utawala Bora unaweza usipatikane. Nashauri kabisa kwamba, kuwepo utaratibu rasmi wa Wakuu wa Mikoa kuwa na vikao na Wabunge, kushauriana masuala yanayohusu Mikoa yao.

Haraka haraka nizungumzie watumishi hewa. Mimi nimeshangaa sana; hivi inawezekanaje kukawa na watumishi hewa; kuna kiongozi pale; kuna Mkaguzi wa Ndani na kuna *Auditor General*? Naomba sana, Waziri huyu namwamini sana, atafute njia za uhakika ili suala hili la aibu lisiwe linajirudia rudia.

Nizungumzie haraka haraka kuhusu kauli za Serikali hapa Bungeni. Kauli za Serikali hapa Bungeni ni vizuri ziwe za usahihi na za uhakika, maana inapokuwa zinagongana au zinakuwa hazina usahihi uliokamilika, hii si sifa nzuri kwa nchi yetu, maana Bunge ni Taasisi ya wazi. Wanatusikia wananchi wa ndani na nje ya nchi. Kwa

hiyo, nawashauri kwamba, pale ambapo Kauli za Serikali zinahitajika kufanyiwa kazi, basi bora kuchukua muda kuliko kutoa Kauli za haraka haraka ambazo siku nyingine zitaonekana haziko sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wahusika waniwie radhi kama siyo mahali pake, niwasemee Wakuu wa Mikoa ambao pia ni Wabunge. Hawa ndugu zetu Wakuu wa Mikoa ambao ni Wabunge, lakini wamepangiwa Mikoa ya mbali, nawahurumia sana; kama wenyewe hawasemi, tuwasemee. Maana kazi ya Mkuu wa Mkoa ni kubwa katika Mkoa wake na kazi ya Mbunge ni kazi kubwa. Wanapokuwa wapo Mikoa ya mbali, naamini kwamba inawawia vigumu. Vilevile kuna kundi lingine la Wakuu wa Mikoa ambao walishindwa katika Ubunge. Hawa mimi ninavyoona wakiwa Mikoa ya jirani mara nyingine wanashawishika kuendelea na shughuli za Ubunge katika Mikoa au Wilaya zile walikotoka. *(Makofi)*

Mimi nashauri kama inawezekana, wapangiwe maeneo ya mbali ili wasishawishike kufanya vitendo vya kuleta makundi katika majimbo yale ambayo walikuwa ni Wabunge. Baada ya hayo, nimpongeze tena Mheshimiwa Ghasia, Mawaziri wenzake na Taasisi zake kwa mfano, TAKUKURU kule Lushoto wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Mshangama. Sasa namwita Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa na Mheshimiwa Paul Kimiti ajiandae.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu mfupi katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati, kwa hiyo, sitakuwa na mengi sana. Maoni yetu kwenye Kamati yamekwishatolewa, nitakuwa na mchango mdogo tu. Nawapongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Sophia Simba, pamoja na Watendaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la mishahara ya wafanyakazi, limeshaongelewa sana lakini na mimi naomba nichukue nafasi hii kidogo nilizungumzie. Mheshimiwa Rais, alipokuja kulizindua Bunge hili alizungumza mambo mengi tu na miongozi mwa mambo aliyoyazungumza, alisema anayajua malalamiko ya watumishi wa umma na yeye atafanya kazi kadiri atakavyoweza na kutokana na hali itakavyoruhusu, kuhakikisha kwamba, anayatazama maslahi ya watumishi wa umma. Alisema suala hilo alilianzisha Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, lakini bahati mbaya halikuendelea yeye ataliendeleza na ataunda Tume.

Alisema ataunda Tume, lakini alitahadharisha watu wasiwe na matumaini makubwa. Kwa hiyo, hali itakavyokwenda itategemea namna gani Serikali itakavyopata uchumi wake na watumishi ndivyo watakatavyofanikiwa. Sasa naomba uniruhusu ninukuu

sehemu ndogo tu ya hotuba hiyo iliyoko kwenye *Hansard*: “Lakini tutafanya kinachowezezana kadiri ya uwezo wa Serikali unavyojengeka ili mwaka hadi mwaka, watu waanze kuona tofauti ya walivyokuwa kabla.”

Sasa hivi tumeambiwa mishahara imepanda kutoka shilingi 85,760 mpaka shilingi laki moja. Sasa kabla haikuwa hivyo, ilikuwa ni shilingi 60,000. Kwa hiyo, tumetoka 60,000 na kuja 80,000 sasa hivi ni laki moja. Kweli hapo wananchi au wale watu hawapo tena kule walikotoka. Imani yangu ni kwamba nia ya Mheshimiwa Rais haikuwa hiyo tu, lakini pamoja na nia hiyo ni kuhakikisha kwamba, mishahara itaendana na hali halisi ilivyo. Ikiwa kabla ilikuwa 60,000 sasa hivi 80,000, halafu laki imalize hiyo hali haina tena wasi wasi, lakini kama nia vilevile ni kwamba hali ya mishahara iendane na hali halisi ilivyo sasa, hapo ni kazi kubwa. Sasa tujiulize; shilingi laki moja inaendana na hali halisi ilivyo hivi sasa?

Jawabu ni kwamba, hailingani. Sasa nawaomba Mawaziri, Ofisi ya Rais Ikulu, kama ni Washauri Wakuu wa Mheshimiwa Rais; wamshauri vizuri wamwambie bado hiyo hali haijaonyesha tofauti yoyote. Hapo hapo Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ametuambia mishahara imepanda kwa asilimia kuanzia 17 mpaka 30. Sasa kwa hesabu ya haraka haraka tu ni kwamba, yule wa kima cha chini ndiyo utegemeo kupata ongezeko la asilimia 30. Baada ya kufanya mahesabu na baadaye tena nikaomba msaada, nikaona hili ongezeko ni asilimia 23.8. Kwa maana hiyo, kima cha chini hakikuongezeka kwa asilimia 30, kimeongezeka kwa asilimia 23.8. Sasa ikiwa wapo wengine waliopata hilo ongezeko la asilimia 30 ni akina nani kama kima cha chini ndiyo hiki? Ongezeko ni asilimia hii, kwa hiyo, kidogo naomba hapo Mheshimiwa Waziri atufafanulie zaidi akina nani hawa waliokuwa wamepata kuanzia asilimia 25 na kuendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetuambia kwamba, sasa hivi nyongeza hizi zitaanza kulipwa malimbikizo kuanzia mwezi Januari. Sasa ni kwamba, wafanyakazi au watumishi wanaidai Serikali kuanzia mwezi wa Januari. Tatizo linalojitokeza, mara nyingi Serikali inashindwa kutimiza wajibu wake. Matokeo ni kwamba, huwa kuna migongano kati ya watumishi wetu na wengine hugoma na hufanya maandamano. Kwa kweli mimi naomba niitahadharishe Serikali ni hatari kuwafikisha wafanyakazi wetu pahala wakaona kwamba, maslahi yao hayawezi kupatikana isipokuwa kwa mgomo. Itakuwa ni hatari kubwa. Serikali tayari imeshawaambia watumishi kwamba, kuanzia Januari itawalipa malimbikizo na tukijaliwa na Mwenyezi Mungu; bajeti tayari imeshapita, naomba haraka sana wawafikirie watumishi wetu na kuwalipa malimbikizo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo niendeleo kuhusu suala zima la matumizi mazuri ya fedha za umma. Mara nyingi huwa tunaambiwa hapa sungura ni mdogo. Hii kauli ya sungura siku zote ni mdogo, hatakuwa mkubwa hata siku moja. Ni tofauti kusema ng’ombe; ukisema ndama anajulikana, ukisema mtamba au kidume anajulikana na koo vilevile anajulikana, lakini sungura ni sungura tu hata awe vipi ni mdogo na ataendelea kuwa ni mdogo. (*Makofi*)

Sasa kauli hii si nzuri hata kidogo, kuitumia kama kinga kwa wananchi na kwa watumishi wetu kwa ujumla. Fedha zilizopo ni nyingi, lakini matumizi yake huwa ni mabaya mno. Hili nitalizungumza nitakapozungumzia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza na hiki kitabu ambacho tulikipata kwenye Kamati. Kwa ruhusa yako, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 9.8 matumizi ya kawaida kwa mwaka 2007/2008, lakini mpaka Aprili, 2008 walitumia bilioni 12.4. Matumizi ya Kawaida tu. Hapo pana ongezeko la shilingi bilioni mbili, milioni 605 na nukta kidogo. Sasa mmoja wetu alihoji je, ilikuwakuwaje haya? Jibu alilolipata siyo baya ni zuri na mimi sina wasiwasi na jibu hilo kwamba, Rais Mstaafu alikwenda kusuluhisha Kenya sasa ni suala zuri, lakini hizi pesa ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa hali ni hiyo, imani yetu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri atatuletea matumizi ya ziada lakini hali inatisha mno. Inawezekana kama kweli zote zilitumika katika hali hiyo, lakini inawezekana kulikuwa na mwanya na wengine walipata wakapita hapo. Pamoja na yote tunasema sungura ni mdogo, sungura hawezi kuwa mkubwa. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, atupe ufafanuzi mzuri wa maswali hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo tukizungumzia Zanzibar wengi wanaumia sana. Bilioni 2.6 kwenda kusuluhisha Kenya, lakini Zanzibar kana kwamba hatuna habari. Hili ni suala ni baya mno. *(Makofi)*

Tunajifanya wazuri au wema kwa majirani, lakini sisi huku kwetu tunaumizana katika hali hiyo. Suala hili linavunja moyo sana. Huku kwetu tunaficha moto wakati moshi tayari unaonekana, suala hili ni zito sana. Suala hili linavunja moyo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema sina mchango mkubwa sana, namalizia kuhusu suala zima la Utawala Bora. Hili suala ni kubwa na lina uwanja mpana, lakini nitazungumzia kuhusu masuala ya fedha tu. Kwenye kitabu...

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti - Mwongozo wa Spika

MWENYEKITI: Mwongozo wa Spika.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji wa sasa hivi anasema kwamba, Usuluhishi wa Kenya zilitumika shilingi bilioni mbili; ana uhakika na anaweza kuthibitisha hayo? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salim Yussuf, labda nikupe nafasi uweze kuthibitisha uliyoyasema.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo hiyo Kanuni aliyoisoma Mheshimiwa Waziri, ilitakiwa kwanza yeye atuambie anafahamu vipi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Hapana, nadhani amekutaka uthibitisha. Samahani Mheshimiwa Waziri, umetumia Kanuni ipi?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni Namba 68(1).

MWENYEKITI: Isome.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, 68(1) inasema kwamba: “Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu ambapo Mbunge yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika, atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa.” (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salim Yussuf, nafikiri kulikuwa na ufafanuzi ulitakiwa hapo.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kwenye Kamati, mimi binafsi niliuliza swala hili na Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ndugu George Yambesi, aliniambia kwamba, kulikuwa na swala la Mheshimiwa Mkapa, alipoenda kusuluhisha Kenya. Mheshimiwa Rajab, akaniambia Mheshimiwa Salim, tazama *delegation* ya Rais Mkapa ilivyo. Kwa hiyo, hizo siyo nyingi.

MWENYEKITI: Naam, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichohoji mimi si ukweli kwamba Mheshimiwa Mkapa, alikwenda kusuluhisha Kenya. Nilichohoji ni fedha ambazo ametamka, ana uhakika nazo hizo bilioni mbili?

MWENYEKITI: Samahani, hebu toa ufafanuzi mzuri ili aweze kukuelewa. Bilioni mbili yeye ametamka kwamba zimetumika kwa ajili ya usuluhishi au vipi, hebu fafana kidogo.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyomwelewa, alikuwa anasema kwamba, Serikali ya Tanzania ilitoa shilingi bilioni mbili kwa Mheshimiwa Mkapa, kwenda kusuluhisha Kenya, wakati Serikali hii hii haitoi pesa kwenda kusuluhisha Zanzibar. Ndio nikasema,

hizo bilioni mbili ambazo Serikali ya Tanzania imetoa kwa Mheshimiwa Mkapa, ana uhakika nazo? Anaweza kuthibitisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salim Yussuf, unaweza kuthibitisha au huwezi?

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri hajanielewa; tulipokuwa kwenye Kamati, mimi binafsi niliuliza na *note* tayari niliandika hapa, mbona kuna ongezeko hili, ambapo tayari makisio yenu ni bilioni 9; mbona mmefika bilioni 12? Ndio Katibu Mkuu, akaniambia hivyo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti – kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kanuni?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hiyo hiyo ya 68. Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kifungu cha 4 cha kanuni hiyo, lakini tunaposoma Kanuni hatusomi kifungu kimoja tu, tunasoma Kanuni nzima kwa ujumla wake. Kifungu cha 6 cha kanuni hiyo, kinamtaka Mbunge au Waziri, anayemtaka Mbunge mwingine athibitisha, yeye kwanza athibitisha kama hayo yaliyosemwa na huyo Mbunge ni uwongo ndipo aweze kuthibitishiwa.

Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, aweze kuthibitisha kama Serikali haikutumia bilioni 2.6 kwenda kusuluhisha Kenya. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nafikiri kabla hatujafikia tamati ili tuweze kuendelea, labda kwanza na mimi nimtake Mheshimiwa Waziri, ukweli ukoje kuhusiana na suala hili ili baadaye tena turudi kwa Mheshimiwa Salim Yussuf, kuweza kuliweka sawa suala hili. Samahani, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa takwimu sahihi, lakini kwa kawaida Rais anapokwenda katika mikutano kama ile huwa halipiwi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Anapopata mialiko kwa shughuli kama zile, kule ambako anaenda kama ni Jumuiya labda ya *AU* ndio inalipia, kama ni *UN* ndio inalipia, lakini kusema kwamba tumelipa sisi Utumishi sio kweli. (*Makofi*)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Kuhusu utaratibu

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dr. Slaa kaa kwanza.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Kuhusu utaratibu

MWENYEKITI: Ahsante, kaa kwanza kwa sababu Mwenyekiti amesimama hapa kwa hiyo mtu mwingine yeyote haruhusiwi. Mimi nikisimama, wewe unatakiwa ukae kitako.

Nadhani ufafanuzi uliotoka kwa Mheshimiwa Waziri ni mzuri tu.

WABUNGE FULANI: Hapana!

MWENYEKITI: Samahani, suala lililotakiwa kufanyika hapa; Mheshimiwa Waziri alimtaka Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anazungumza athibitisha, hicho kiwango kilichozungumzwa ni cha kweli? Waziri nadhani ameshatoa ufafanuzi hapa, amesema kwamba kimetumika kiasi hicho.

WANUNGE FULANI: Hapana!

MWENYEKITI: Basi nampa nafasi ili azidi kufafanua, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba zimetumika shilingi bilioni 2.6, kwa ajili ya kusuluhisha mgogoro wa Kenya. Ongezeko la pesa katika fungu lile limetokana na suala la kupanda kwa gharama za mafuta kwa hawa wastaafu wetu, lakini pia kwenda katika matibabu na kuongezeka kwa kiongozi mwingine, ambaye tunamshughulikia katika Viongozi wetu Wastaafu, lakini haijatumika shilingi bilioni 2.6.

Mr. Yambesi, anayemtaja amethibitisha. Naomba kama ana ushahidi atoe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salim Yussuf, hebu tunaomba ufafanuzi kwa sababu inaonekana mmojawapo atakuwa amepotoshwa na Katibu Mkuu hana uwezo wa kuingia hapa. Hebu tunaomba ufafanuzi.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nasema tena mimi binafsi ndiye niliyeuliza swali hilo. Katibu Mkuu akaniambia unajua Mheshimiwa Mkapa, alikwenda kusuluhisha Kenya. Nilipokaa kitako, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, akaniambia Mheshimiwa hizo sio pesa nyingi, tazama *delegation* ya Mheshimiwa Mkapa, ilivyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Naomba ukae Mheshimiwa Salim Yussuf. Uamuzi nitakaoufanya ni kwamba, huu mjadala nitaumaliza hapa ili tuweze kuendelea tuokoe muda. Suala hili kesho baada ya maswali na majibu, nafikiri tutapata ufafanuzi mzuri zaidi. Kwa hiyo, tuendeleo Mheshimiwa Salim Yussuf, malizia muda wako.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, naomba watumishi wanapotujibu maswali wasitujibu kwa kulega lega tu, kwa sababu tunafuatilia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Naomba uendeleo na mjadala usiliendeleze hili.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye suala zima la Utawala Bora; Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ametoa taarifa katika vitabu vitatu. Kitabu cha kwanza ni kwa ajili ya Serikali Kuu, huku kuna Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Sasa hivi vyote naviacha, naenda huku tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ameir amezungumza kwamba, ikiwa mzee anapiga ngoma, mtoto atafanya vipi? Ukurasa wa 17 wa kitabu hiki, Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma; malipo yasiyo na nyaraka ni milioni 47.0, masurufu yasiyorejeshwa milioni 120.2. Sasa nazungumza kidogo tu kwamba, ikiwa hali ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni hii na ni sehemu tu; hali iko hivi; na hiki ni kitabu cha Serikali Kuu; je, Serikali za Mitaa hali itakuwaje? Sasa hivi tujitahidi sana, suala la Utawala Bora hasa kuhusu udhibiti wa fedha uwe mzuri. Hapo hapo nafikiri nimalizie kwa mapendekezo aliyoyatoa huyu Mdhibiti, ukurasa wa 92. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba ninukuu kidogo tu: “Kuimarisha nidhamu ya matumizi; ni muda muafaka sasa Serikali iangalie mfumo wa matumizi na iweke nidhamu katika matumizi miongoni mwa watumishi wa umma ili kupunguza kabisa matumizi yasiyo ya lazima. Serikali ifanye jitihada ili kuhakikisha kwamba, Watanzania wote wanafaidika kutokana na ongezeko la maduhuli na kukua kwa uchumi. Hii inawezekana tukizingatia yafuatayo: Serikali iwe na viwango vya aina za samani na magari ili kuweka udhibiti wa matumizi ya mafuta.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoingia humu Bungeni, Mheshimiwa Spika alituambia, meza ile pale imetengenezwa na wenzetu wa JKT. Sasa hebu tutazame meza nzuri kama ile iliyopo Bungeni, kuna haja gani ya kuagiza samani kutoka nchi za nje? Mara nyingi wenzetu huwa wanazungumza; magari kama mashangingi, yaliyokuwa hayana ulazima ni vyema yapunguzwe. Sasa huo ni ushauri ambao kautoa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; naomba sana wahusika wautilie maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi angalau na mimi niweze kuchangia, nafasi ambayo ilikuwa adimu sana katika Wizara mbili zilizopita. Kwa mujibu wa Kanuni ya 151 na Kanuni ndogo ya pili, sitaendelea kupongeza na nitaendelea katika kuchangia moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza ni hotuba hii ya maoni ya Kambi ya Upinzani, iliyotolewa na Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu. Kwa kweli hii ndio hotuba ambayo ninaiunga mkono na ni mchango makini unaofaa kusikilizwa na Serikali. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu mara nyingi sana, nyani haoni sehemu yake ya nyuma, lakini sisi huku ndio tunaona. Makosa, marekebisho au ushauri uliotolewa katika hotuba hii, ume-cover hotuba nzima ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa hiyo, ningepomba Serikali iizingatie sana katika kusuma hilo gurudumu mbele vinginevyo, itakuwa ile ya mdharau mwiba. Mwiba tunaouzungumza hapa, wananchi ndio mwiba kwa sababu wanaona haya yaliyozungumzwa. Sasa mdharau mwiba huota tende. (*Makofi/Kicheko*)

Mhsheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka kuzungumzia kwamba, inaonekana Wabunge takriban wote waliosimama kuchangia, kuna suala halikuepukika kuzungumziwa ambalo ni hili la kima cha chini cha mshahara. Si vibaya kulizungumza kwa sababu wadau wetu wote ni hao hao wananchi na wanaoumia ni wananchi. Ongezeko hili la kutoka Sh. 80,760 mpaka Sh. 100,000, ambayo ni ongezeko la Sh. 19,240 kidogo linachekesha. Labda Mhsheshimiwa Waziri, akija hapa atuambie *factors* zote zilizotumika kupata ongezeko hilo, kwa kutilia maanani *inflation* yote hivi sasa; ongezeko la mafuta, ongezeko la vyakula, ilikuwaje ikawa kutoka Sh. 80,760 zikaongezwa Sh. 19,000 kufikia hiyo Sh. 100,000? Hizo *factors* tunataka tuzijue kutokana na hali halisi kwamba haiwezekani.

Mhsheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitabu kimoja kinachozungumzia *Low Salary to Africans and High Salary to White People*. Sasa tusigeuke sisi wenyewe, Serikali haiwezi kulipa mishahara midogo kwa wananchi wake, pamoja na hali ngumu kwa sababu kama inalipa mishahara mdogo kiasi hicho, tutakuwa na hoja gani ya kuwalaumu *private investors* wanaowanyasya watu wetu huko kwenye viwanda na kwenye migodi? Tutakuwa na *argument* gani ya kuwakamata wale, ikiwa sisi wenyewe ndio watendaji?

Nafikiri hili suala lizingatiwe na ukichukua hesabu ndogo tu ukasema labda chai ya asubuhi, mtu atumie Sh. 1,000, chakula cha mchana aende kwa mama ntilie, hicho chakula tunachoambiwa kina matatizo alipe Sh. 1,500 na jioni alipe Sh. 1,500, tayari ni Sh. 4,000 hizo. Ikiwa ni Sh. 4,000 tayari kwa mwezi ni Sh. 120,000, hajafanya kingine chochote. Sasa hii *consideration* imefanyika vipi? Mhsheshimiwa Waziri, atufafanulie hizo *factors*, lakini hii ni hali ambayo haivumiliki na ibadilishwe. Hilo ndio suala la kwanza. (*Makofi*)

Mhsheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ninalotaka kulizungumzia ni sawasawa na baniani mbaya kiatu chake dawa; suala la *pension*. Hii Wizara inahusika na mambo mengi yakiwemo ya Usalama wa Taifa, Tume ya Mipango, TAKUKURU, Maadili, Utawala Bora, na kadhalika. Nataka kuzungumzia suala la *pension* ambalo wenzangu wameshalizungumzia, lakini kwa *case* ya Zanzibar. Kwa nini nimesema baniani mbaya kiatu chake dawa?

Nimesema hivyo kwa sababu nataka kuzungumzia hoja za watu ambao hao hao wakati mwingine ndio huona sisi Kambi ya Upinzani ni maadui zao. Sisi tunawatumikia na kwa sababu ni wapiga kura wetu, hatuna budi. Hatuwezi kubagua tukasema huyu hakunipigia kura siwezi kumtetea au kumchagua, hata kama hakunipigia kura lakini nitawatetea. Usalama wa Taifa upande wa Zanzibar, hiki kitengo kiliunganishwa mnamo miaka ya 80 hivi. Sasa wapo ambao walikuwa wamesha-*serve* kwa upande wa Zanzibar tu kwa miaka kama 19, wengine miaka 15 au 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunganishwa kunako miaka ya 80, kuna wengine wamestaafu na wamestaafu wakiwa wameshatumikia kama miaka 35 ya kazi; 19 upande ule kule na baadaye 16 katika Jamhuri moja ya Muungano. Sasa mtu huyu baada ya kustaafu leo, anapata *pension* yake Sh. 19,000; mtu ambaye amefika cheo cha *RSO*, aibu. Kwa nini ichukuliwe kipande hiki tu, wakati pameshaunganishwa, usichukuliwe muda wake wa miaka yote 35? Hili suala lipo katika ofisi yako Mheshimiwa Waziri, lishughulikie hawa ndugu zetu ambao waliitumikia nchi hii kwa muda mrefu sana halafu baadaye wawe *watchmen* au waombe ombe ni aibu jamani. Tusiruhusu hali hii na walikuwa watu wazuri tu japo wengine ndio hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu linahusiana na Utawala Bora. Utawala Bora hauendi peke yake, unakwenda na mambo ya rushwa. Rushwa na Utawala Bora. Palipo na rushwa hakuna uwezo wa kuondoa umaskini, palipo na rushwa hakuna Utawala Bora, palipo na rushwa hakuna Demokrasia ya kweli, palipo na rushwa hakuna maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, mambo ya Utawala Bora na rushwa yanakwenda sambamba. Ili tuwe na Utawala Bora, pasiwe na rushwa. Kuna Waheshimiwa Wabunge, wameisifu TAKUKURU; aisifuye mvua imemnyea.

Kwa mujibu wa *research* waliyoifanya *REPOA*, rushwa imeongezeka sehemu nyingi sana ya Tanzania kwa kulinganisha miaka ya 2003 na 2006. Ni sehemu chache sana ambapo imeshuka *ki-graph*. Sheria mpya tumepitisha hapa na imeanza kufanya kazi; Sheria Namba 11 ya 2007, imeanza kufanya kazi Julai, 2007. Hiki ni kiasi cha mwaka mmoja sasa na kama ile Sheria ya zamani ilikuwa haina meno, hii ina meno ya kila aina; kwa nini hatujaona tofauti? (*Makofi*)

Mheshimiwa Menyekiti, leo nitoe mfano; rushwa, Utawala Bora na haki za binadamu; hivi karibuni mwenzangu mmoja, bahati mbaya nasikitika alijibiwa Zanzibar si nchi. Sasa, *okay*, tukiichukulia hivyo, inategemea wengine hujibu hivyo kwa wakati tofauti. Ikiwa ni hivyo; hii Tanzania iwe na *double standard*? Leo Dar es Salaam kuna kesi ya Zombe inaendelea, hata wasipozungumza, askari anayetuhumiwa mambo ya mauwaji. Zanzibar wameshaujiwa watu mara ngapi na maaskari hatujasikia; kwani kuna kesi iliyofunguliwa? Hii nchi yetu ya Tanzania inafanya nini? Utawala Bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za binadamu; hii *double standard* ya kitu gani? Ikiwa huku polisi huyo huyo anapelekwa Mahakamani kushtakiwa lakini polisi huyu upande mwingine asifanywe chochote kwa nini? Ndio mpaka inafika *stage* watu wanakwenda *United Nation*, mara wanakamatwa, wanafanywa vipi; lakini Wahadzabe walipokwenda *United Nation* kudai ardhi yao, hawajakamatwa, hawajanyanyaswa wala hawajafanywa jambo lolote. Hii *double standard* ya nini? Ili tuwe na Utawala Bora, ondoeni *double standard* Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhuluma zipo na TAKUKURU wanapaswa moja katika kazi yao, kuona wapi panaashiria mambo ya rushwa waingilie kati. Wamepewa

meno ya kupeleleza, kukamata na kufungua mashtaka. Kuna kesi Geita ya kudai eneo la ardhi, ilikuwa Mahakamani akashinda Hosea, akatoka. Mpaka leo anashindwa kumilikishwa hati ile.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti – kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kanuni?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 63; ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyaa alipokuwa anachangia anasema kwamba, Zanzibar maaskari wamekuwa wanakufa wanauawa na hatua zozote hazichukuliwi, ikiwa ni pamoja na kufunguliwa kesi.

Vilevile askari wanauwa hawafunguliwi kesi. Sasa taarifa kama hizi wakati Watanzania wanazisikiliza zinatisha, kama watu wanaweza wakauwa halafu wasichukuliwe hatua! Nilikuwa nakutaka utupe mwongozo wako; anaweza kulithibitishia Bunge kuwa watu waliouawa na askari hatua hazikuchuliwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyaa, unatakiwa uthibitishie au ufute usemi wako.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu mpya kifungu cha 63(4); ni yeye anayepaswa kuthibitisha kama nililosema mimi sio kweli. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Labda nisaidiwe kwa kusoma Kanuni. Kanuni ya 63(3)...

WABUNGE FULANI: Kifungu cha 4.

MWENYEKITI: Nitaanzia cha (3). Samahani, bora niisome yote nzima; 63(1): “Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni. Na kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni, ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na sio jambo la kubuni au la kubahatisha tu.”

Kifungu kidogo (2): “Mbunge yeyote, anapokuwa akisema Bungeni, hatachukuliwa kuwa anasema uwongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa au lililoandikwa katika vyombo vya habari.” (*Makofi*)

(3): “Mbunge mwingine yeyote, anaweza kusimama mahala pake na kutamka kuhusu utaratibu na baada ya kuruhusiwa na Spika, kudai kwamba Mbunge aliyekuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uwongo kuhusu jambo au suala alilokuwa amelisema Bungeni.”

Kifungu kidogo (4), kinasema: “Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya tatu ya Kanuni hii, atakuwa na wajibu wa kutoa au kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.” (*Makofi*)

Kifungu kidogo (5): “Bila kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Spika au Mbunge mwingine yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi wa maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake; na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.” (*Makofi*)

Sasa, ninamwomba Mheshimiwa Mnyaa...

MBUNGE FULANI: Ya sita?

MWENYEKITI: Kiti ninacho mimi. Ya (6) inasema: “Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyoyatoa Bungeni, atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, papo hapo au katika muda atakaopewa na Spika, kwa ajili ya kufanya hivyo.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mnyaa, nakutaka uthibitishie au ufute tu huo usemi wako.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti - kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabwe, nadhani ...

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti - kuhusu utaratibu

MWENYEKITI: Ndio, lakini bado nikmesimama. Nafikiri ruhusa niliyotoa sasahivi ya Mnyaa, kuthibitisha, baada ya hapo utasimama kuhusu huo utaratibu unaozungumza.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kufuta usemi huo. Mauwaji yametendeka si mara moja wala mara mbili, ushahidi upo na juu ya hivyo, Kanuni ya 63(2) inatosha kwa sababu vyombo vimeandika mara nyingi sana na ipo hapo. Kwa hiyo, tunaweza kwenda Kanuni ya 63(4) kabla hatujafika ya sita na hiyo ya (4) ni yeye athibitishie *otherwise*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Hapana, Mheshimiwa Mnyaa, wewe itabidi utupe muda; unahitaji muda gani kwa sababu wewe umesema umeona kwenye vyombo vya habari; unalo gazeti au ushahidi mwingine wowote ulithibitishie Bunge na tukupe muda gani ufanye hivyo? (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti - kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Nazungumza na Mheshimiwa Myaa.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti - kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haki ya Mbunge kuzungumza anapomba kuhusu utaratibu. Naomba uniruhusu.

MWENYEKITI: Nadhani nilizungumza, tukimaliza suala hili nitakuja kwako Mheshimiwa Kabwe, kwa sababu tuna suala lingine hapa. Wewe unaleta jambo lako jipya, sasa hivi tuna suala linalomhusu Mheshimiwa Mnyaa, ngojea alikamilishe hili halafu utakuja wewe.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi yako hiyo na kwa kiapo chetu, naomba utende haki na hatuwezi kurukia Kanuni ya (6) wakati kuna (1), (2), (3), (4). Kanuni ya (4), ikiwa hakuna mauwaji ya askari yaliyofanyika Zanzibar, wala si mara moja, athibitishe yeye Mheshimiwa Mbunge. Hii ndio Kanuni inavyotaka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyaa, wewe ndiye uliyezungumzia mauwaji humu ndani ya Bunge na ndio una wajibu wa kuthibitisha kwa kuleta vielelezo au kwa kuwataja hao wahusika na sio yule aliyetoa kuhusu utaratibu hapa. Yeye alichokitaka, ametaka apate ukweli kutoka kwako wewe. Wewe ndiye uliyelizungumza, ndio unalifahamu hili suala, kwa hiyo ulete ushahidi. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti ...

MWENYEKITI: Samahani sijamaliza

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani - kuhusu utaratibu. Kanuni inakiukwa na inapokiukwa hatuwezi kuachia. Kifungu cha (4) ...

(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (4).

(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele)

MWENYEKITI: Nakuomba ukae kwanza Mheshimiwa Slaa. Ili tuokoe wakati nadhani bora tufanye hivi, hili suala lipate ufafanuzi kesho vilevile ili tuweze kuendelea. (*Makofi*)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti - kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Sasa ninakuruhusu Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa hilo lako jipya.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kuzingatia Kanuni za Bunge na tunapozitafsiri ni lazima tuzitafsiri kwa ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 63 (5) inasema: “Bila kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, ninarudia na ninaomba Wabunge wa CCM wasikie; bila kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, kwa wanasheria wanajua, unapokuwa na kifungu ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zitto nilitegemea utakuwa na jambo jipya kwa sababu hili ...

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti - taarifa.

MWENYEKITI: Hapana, sijaruhusu taarifa. Nadhani hili suala nimesema kwamba, kesho ndio tutalimalizia, litapata ufafanuzi na nilimruhusu Mheshimiwa Mnyaa aendelee. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuokoa muda niweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninazungumzia rushwa na Utawala Bora.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Kifungu 63 (1), Mheshimiwa Mbunge katika mchango wake ametaja suala la *double standard* kwamba, wananchi wa sehemu fulani ya Tanzania wakienda Umoja wa Mataifa wanakamatwa lakini Wahadzabe wakienda Umoja wa Mataifa hawakukamatwa, nataka atuhakikishie kwamba; je, Wahadzabe nao walienda kudai kujitenga kutoka Jamhuri ya Muungano au ni masuala mawili tofauti, yanafanana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, naomba ukae. Mheshimiwa hakutamka kwamba Wahadzabe wanaenda kudai kujitenga, nafikiri neno kujitenga halikuwemo katika misamiati aliyoitaja, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mnyaa aendelee. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kukalia Kiti chako vizuri na kunilinda, niendelee na mjadala wetu ambao tunazungumzia rushwa na Utawala Bora.

Nilikuwa ninasema kwamba, kutokana na *rearch* iliyofanywa, rushwa haijaonekana dalili ya kupungua nchini Tanzania na inaonekana mwaka 2006 ilikuwa kubwa zaidi kuliko hata ilivyokuwa mwaka 2003 katika sehemu nyingi sana za Jamhuri ya Muungano. Yapo mambo mengi ambayo yanaainisha rushwa. Nilikuwa

nazungumzia kesi ya ndugu Hosea Katampa kule Geita, ambapo alishinda kesi Mahakamani na mpaka leo hajapata *rights* zake. Anacheleweshewa kupewa *rights* zake za kumilikishwa eneo tokea mwaka 2004. Huu ni mfano mmoja, nini kinatendeka kule wakati mpaka mahakama yetu imeshaamua kwa sababu ya mwekezaji mkubwa *GGM*? Hivi ni viashiria vibaya, aidha, ukisema vya Utawala Bora au rushwa na TAKUKURU wapo na ingefaa watupatie ufumbuzi; je, hawajaona kesi hiyo ya muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa hilo halitoshi, kuna Ndugu Geoffrey Emmanuel au Ndugu Emmanuel Petro Zombwe wa Kijiji cha Rufusi Tabora, anahangaishwa *just* kwa msimamo wake wa kisiasa anayimwa haki zake. Imefikia *stage* anauza bamba halipwi! Mtoto wake Geoffrey amejajiri mwenyewe anatengeneza madirisha, anauza kuna watu wanasema halipwi; sasa hii ni kitu gani? Watendaji wapo, Wakurugenzi wapo, *DC* yupo; nini kinaendelea? Je, TAKUKURU hawajaona kesi kama hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa upande wa Kanda ya Ziwa, kuna unyanyasaji mkubwa na demokrasia haiwezi kushamiri kwa namna hii. Hivi ni viashiria vibaya hatuwezi kuviachia na TAKUKURU wangepaswa washughulikie masuala haya. Kwa maana hiyo, panapo rushwa demokrasia ya kweli haipatikani. Halafu siyo hilo tu, ikiwa katika Sheria ya Rushwa tuliyoipitisha kuna mambo mengi yanayozungumzwa hata kwa mfano ushawishi, nafikiri kifungu cha 39; Waziri atatuambiaje, vile vyama vinavyowashawishi watu kwa misingi ya pesa kuviacha vyama vingine si rushwa ile?

Je, vile vyama ambavyo vinatoa bure kwa mfano, kofia, fulana na vitu vingine angalau wangetoa nusu ya pesa akalipa yule anayepewa suala lingine, lakini unapotoa bure; hivi si viashiria unatoa bure kwa sababu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU wana kazi kubwa na ipo haja ya kufuatilia kwa makini. Ahsante sana, mchango wangu ndio huo.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie machache kuhusiana na hotuba nzuri aliyoitoa Waziri.

Kabla ya yote, nataka nitumie nafasi hii, kumpongeza kwa dhati, Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kwenda kila mahali, kutafuta namna ya kufanikisha maendeleo ya nchi hii. Amefanya kazi kubwa ni sawa na sisi Wabunge tunapozunguka kutafuta chochote kuwarudia wapiga kura wetu. Ndio kazi na Rais tumpa hiyo kazi, lazima azunguke atutafutie chakula ili akirudi tuseme angalau tumeletewa chakula. Naomba aendelee na kazi hiiyo wala asiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Mawaziri wote waliozungumza; kuanzia Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu na Watumishi wote, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Bado kuna matatizo ambayo nitajaribu kuyazungumza kidogo, lakini nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, sisi ambao tumekaa kwa muda mrefu ndani ya Bunge, kama mtu yoyote anazungumza Bungeni na ana ushahidi nacho, kulikuwa na utaratibu ambao nataka mpaka sasa tuendelee nao; unakuja na ushahidi ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapunguza hii kusimama una hoja, una taarifa, itatupunguzia maneno hayo; unazungumza ushahidi wangu ni huu, hutakuwa na mtu yeyote atakayezungumza. Tukiendelea hivi tutapata matatizo makubwa sana na Bunge badala ya kuzungumzia maendeleo, tutakuwa tunabishana mambo ambayo baadaye yatatupoteza muda bure, badala ya kuangalia nini kimetuleta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka niwaombeni; kuna mtaalam mmoja ambaye amelalamikiwa kuhusiana na suala zima la tabia ya wafanyakazi Duniani. Sote tunakumbuka, walikuwepo akina Abraham Maslow, Mc Gregory na Licard. Wote hao ni wataalam na wanakubaliana na maneno yaliyoandikwa katika misahafu ya kwamba, binadamu haishi kwa mkate peke yake na wao wameendelea zaidi wanasema, binadamu huyo siku hizi haishi kwa mishahara peke yake; yapo mambo mengi yanayomzunguka huyu binadamu ambayo usipoyatekeleza utapata matatizo katika utendaji wa kazi. Nataka nianzie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 10, 15 iliyopita tulikuwa na kitu kinachoitwa ni Sera ya Tija, Mishahara na Bei. Makusudi mazima ilikuwa ni kuangalia mfumo mzima wa mishahara ili isije ikapishana sana; mwingine anapata mara 100. Walifanya makusudi mazima ili angalau kuoanisha tofauti za mishahara kati ya kima cha chini na kima cha juu na sera wakati huo ilikuwa inasema kisizidi asilimia 10. Sasa nini kimetokea? Tofauti za mishahara zimekuwa kubwa sana kati ya kima cha juu na kima cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hiyo unasema hivi tunaenda wapi! Wasiwasi wangu ni kima cha chini kwamba, ukiangalia ni kidogo sana; kinawafanya watumishi wetu wawe na tabia tofauti na ndio maana kinaleta mambo makubwa mawili; la kwanza, hivi katika utendaji wetu wa kazi kwa nini fulani anapata zaidi na mwingine sipati! Katika utendaji yapo mambo mawili yanayojitokeza; kwanza ni kudharau utendaji wa kazi mambo yanaenda taratibu. La pili, ili asionekane mbaya kunakuwa na nidhamu ya woga, ndilo Mheshimiwa Balozi Mshangama alilolizungumza, mimi nitalizungumza kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidhamu ya woga imetufikisha mahali fulani baadhi ya watumishi wetu kutotoa majibu sahihi. Nitawapeni mifano, hakuna kitu kiliniuma wakati Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete anapewa taarifa ya kwamba, baadhi ya barabara zitakuwa zimejengwa au zimekamilika kipindi fulani na akasema hadharani. Hakuna kitu kinaudhi Waziri anapewa taarifa tofauti na hali halisi mpaka inafikia Mbunge anasema sikubaliani na aliyosema Waziri! Mtumishi anakupa *wrong information*, Rais anatoa *wrong information*, Waziri anatoa *wrong information* na tunakaa kimya bure bila hata kumwadhibu! Hiyo dalili lazima tuiangalie, itatufikisha mahali pabaya. Ndio maana nasema, lazima sasa tuanze kusimamia kwa dhati kuhakikisha kwamba, taarifa tunazozipata ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako, mwaka 1984 nilikuwa *front bench* najibu maswali kwa niaba ya Waziri Mkuu, wakati huo Marehemu Sokoine. Mzee Malecela unakumbuka wakati huo? Nimejibu swali la nyongeza, Mbunge mmoja

akaniuliza Mheshimiwa Waziri utatusaidia kumaliza kipande cha barabara kilichobaki ambacho ni kilometa mbili mtutafutie fedha mahali popote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasimama nikasema, kwa niaba ya Waziri Mkuu, hilo suala tutaliangalia. Waziri Mkuu akasimama, akasema sikubaliani na Waziri wangu alivyosema. Alisema *openly* pale pale, sikubaliani kwa sababu hatuna fedha wala hazimo katika mpango hivyo, Waziri usiwe unawadanganya watu waambie ukweli. Alikuwa anajaribu kuonyesha nini? Alikuwa anaonyesha *credibility* ya Serikali ya kwamba, hakuna kutoa taarifa ambayo huwezi kuitekeleza. Hilo lilikuwa fundisho la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna mambo mawili ambayo yananisumbua sana; la kwanza, watu wanadhani ukitoa taarifa ya kumpendezesha labda Waziri ndio inakuongezea *credibility* hapana. Kama taarifa siyo sahihi, afadhali umwambie Waziri hapa si kweli. Naomba kabisa watumishi, waseme si kweli hapa haiwezekani ili kama ni marekebisha Waziri mwenyewe atajua namna ya kurekebisha kuliko kumpa taarifa ambayo si sahihi ikaja kutu-*embarrass* hapa; itakuwa ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Bunge ambalo linazungumzia maslahi wa wananchi; mojawapo ni pensheni za wastaafu. Baba wa Taifa aliwahi kusema, ukitaka kufanya jambo lolote lifanye vizuri, usifanye nusu nusu. Ukitaka kutoa mshahara, hakikisha unawapa mshahara mzuri usifanye ovyo ovyo. Hayo ambayo tunaita ya kwamba ni pesa za wenzetu, wazee wetu waliostaafu kuwapa kima cha chini cha Sh.30,000 na sasa sijui zitaifika ngapi hatuelewi; huo kwa kweli ni utani na pensheni siyo hisani ni haki yao. Ukisema kwamba tunawapa kama hisani, hapana ni haki yao, naomba Serikali mliangalie hilo, wazee wanataabika na wengine wanakufa hata kabla ya muda wao kwa ajili ya hali hiyo. Hilo nadhani lazima tulisimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kwa wafanyakazi ni motisha. Nimetambua miaka mitatu iliyopita, tuliomba Wizara hii iweke utaratibu wa motisha kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira magumu au wanaokaa katika mikoa ambayo ipo pembezoni. Tulishaomba na Rais alishaagiza, tazameni utaratibu mzuri utakaowahamasisha wafanyakazi angalau wapende kukaa katika maeneo hayo. Hakuna lililofanyika, Mkoa wa Rukwa tukaamua kufanya wenyewe; tumeanza na Wizara ya Elimu lakini kiasi cha fedha tunazotumia ni kingi sana, ambapo inabidi wanachi tuwaombe wachangie ili kuhakikisha walimu wanabaki katika mkoa huu. Kwa nini Serikali haiji kujifunza Rukwa ili waangalie katika maeneo mengine? Watumie mfano, badala ya Rukwa kwa waganga iwe kwa walimu na wale wengine ambao mnaona umuhimu, kwa nini hamfanyi hivyo? Nadhani ni vizuri tuwe *fair*, msiwaonee watu wa Rukwa wafanye wenyewe, agizo lilishatolewa tuanze na sisi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upandishwaji wa vyeo; bado tuna matatizo makubwa sana, kuna wengine wanakaa zaidi ya miaka kumi hawajarekebishiwa mishahara yao. Kwa mfano, waganga na wauguzi wengi ninaowafahamu, wamekaa miaka mingi wanasota; sijui tatizo lipo wapi; hivi wanangoja mpaka watu wagome?

Waganga walishakataa hawataki kugoma; wanataka wagome kama walimu ndio wawarekebishie? Nadhani ni vizuri mkalifuatilia, yote haya yanapunguza *morale* ya utendaji kazi kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uongozi bora; mtaalam mmoja anaitwa Peter Laurence alikuwa na kitabu chake kinaitwa *Peter's Principle* kinasema, mambo *very simple* kwa Kiingereza, ninanukuu anasema: : “*The ability to lead does not depend on the ability to follow*, uwezo wa kuongoza hauendani sambamba na uwezo wa kuongozwa.” Maana yake mtu ambaye ni mzuri sana kwa kuongozwa *is not automatically* ukimpa madaraka ya juu atafanya vizuri, kwa sababu huyu alikuwa anaongozwa ndio maana alikuwa anafanya vizuri lakini ukimpa madaraka ya juu anaweza kushindwa kuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana katika suala la uongozi, tunadhani ni vizuri viongozi wetu watusaidie na vyombo vya usalama vitusaidie katika kuchambua viongozi tulionao. Tunapata *embarrassment* siku mbili huyu ametolewa, siku mbili huyu amepelekwa, *no* watusaidie tufanyiwe kazi hiyo. Ninalisema hilo kwa dhati, kwa sababu ningependa Serikali iwe na *continuity*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Mawaziri wangu wakianza mwaka wa kwanza wafike mpaka wa tano, *I will be comfortable* kwa sababu ya kujenga uzoefu na namna ya kuendesha shughuli. Hata kama anafanya makosa madogo madogo tunamrekebisha hapo hapo anaendelea. Wengine miezi miwili wamehama huko, mwezi mmoja wamekwenda kule, sasa ni vizuri mtusaidie ili angalau tumsaidie Rais afanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pia masuala mengine ninaomba sana, hapa katikati kuna misafala ya viongozi wetu, makaribisho unapompokea kiongozi nakubali, watu wote mnatoka mnaenda kumpokea kiongozi wenu, mnamkaribisha lakini baada ya hapo, anapoanza ziara za kazi anaenda kutembelea migodi ya almasi, wewe bwana mifugo unaenda kufanya nini? Wewe bwana shamba unaeenda kufanya nini? Wewe bwana samaki unaenda kufanya nini? Hali ya uchumi jamani ni ngumu, tuwe na utaratibu wa kuhakikisha wanaohusika tu ndio wanaenda, lakini unakuta kila mmoja anaenda na gari lake, msululu wa magari 60; kama una shida kule msubiri kiongozi huko huko akukute, siyo kuingia kwenye misafala. Tunawa-*embarrass* viongozi wetu, hawataki kusema tu, misululu ile ndio na ajali zitakuwa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri tukaliangalia kwa sababu kwanza ni hali ya kiuchumi, lakini pia lazima tuhakikishe ya kwamba, wanaohusika ndio waende tu siyo wote. Ndio maana nikarudia kusema, nidhamu ya woga tusipoiangalia itatufikisha watu kwenda tu kwa ajili ya kuogopa kwamba, nisipoonekana nitafukuzwa kazi. Kwa nini tunafikia hapo?

Tumsaidie Rais wetu kufanya kazi vizuri na watu wa *protocol* wapange vizuri. Mtu wa kwanza kumfikiria mwenye watu ni Mbunge, katika maeneo hayo yeye ndio ana watu, unamuweka mwisho. Anatakiwa kuwa wa kwanza kabisa kuhakikisha na ndio

anaye-organize na ku-mobilize watu. Watu wanakaa pale tutafanya kazi vizuri, lakini wakati mwingine unaambiwa Mbunge haumo hata kwenye msafala. Nadhani tuangalie upya *protocol*. Huu ni utaratibu wa kujenga sasa Utawala Bora ili sote tufanye kazi kama timu moja.

Nina imani, tukishirikiana sote kwa pamoja hakuna lolote litakaloharibika. TAKUKURU tushirikiane nao, watu wa Usalama wa Taifa tushirikiane nao, kwa sababu wanahitaji msaada wetu na sisi tunahitaji msaada wao. Mimi kama kiongozi siwafichi, wengine wamefanya kazi nzuri sana; kama kuna tatizo la mmoja mmoja lisiwe ni nongwa. Vyombo hivi jamani tunapumua hapa, vinafanya kazi usiku na mchana, mimi ninajua siri yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niwaambieni msione watu wanalala usiku, kuna watu hawalali wanafanya kazi usiku na mchana, wanahakikisha tupo salama na hakuna lolote linaloharibika. Siku moja ilikuwa kama saa tisa usiku, wakati tunamrehemu Mzee Sokoine, akasema Paul njoo hapa, nini? Kumbe kuna tatizo, hakutakuwa na mafuta nchini kwa siku mbili zijazo, sasa lazima muanze kazi usiku huo kuanza kutafuta meli zipo wapi; zipo huko bandarini au barabarani huko njiani tuzichukue zituletee mafuta ama sivyo *this country ita-paralyze, you can just imagine*; viongozi wanavyo-sweat usiku na mchana. Usalama wa Taifa ndio wanaompa taarifa mzee hali si nzuri, sasa vyombo hivi lazima tuvipe kila aina ya msaada vifanye kazi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nichangie angalau kidogo, lakini zaidi ninakushukuru kwa kukaliA vizuri kiti chako. Najua Kanuni unazielewa na ninaamini kwamba, hautayumba katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nianze kwa lile ambalo Watanzania wengi wangetegemea leo kutokea, ambalo Mheshimiwa Hawa Ghasia angelitangaza ni kupandishwa kwa mishahara. Kwa kuwa Kanuni za Bunge hazituruhusu kurudia rudia, nataka niseme kwa kutoa mifano tu; kuna wanafunzi wawili waliohitimu katika *Soviet Union*, mmoja yupo kule na mwingine yuko Tanzania. Baada ya muda wakapigiana simu; wa Tanzania akamuuliza yule wa *Soviet* vipi hali ya maisha huko? Yule wa *Soviet* akajibu *they pretend to pay me and I pretend to work*, kwa maana ya kwamba, inaonyesha hali ya mishahara inapokuwa ndogo wale wafanyakazi huwa hawafanyi kazi vizuri.

Kama walivyotangulia wenzangu kusema, hii ndio hali halisi ya hapa Tanzania kwamba, mishahara yenu midogo basi wafanyakazi wetu hawafanyi kazi kama inavyotakiwa. Nilitegemea leo mtakuja na ile hoja yenu tuliyoizoea ya kupiku. Bajeti ya Upinzani ilisema itawalipa wafanyakazi wa kima cha chini Sh.250,000, basi

ningetegemea na ninyi mngesema tutalipa Sh.300,000, lakini mmekuja na Sh.100,000; maana yake kumbe hawampiku kwa kila kitu, mambo maalum ya kupiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Utawala Bora ni kubwa, ina safari ndefu na sisi Watanzania tumekuwa tukiwanyooshea wenzetu vidole, karibuni Kenya sasa hivi Zimbabwe, lakini tunajisahau kumbe tuna matatizo makubwa sana ya Utawala Bora katika nchi hii. Nataka nitoe mfano mmoja wa *live* kabisa, nimeushuhudia mwenyewe ambao unaigusa Serikali moja kwa moja; katika Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo kuna hakimu mmoja katika Mkoa wa Morogoro alikuwa anasafiri kwa miguu zaidi ya kilometa 20 siku ya hukumu. Unaweza kujiuliza hakimu yule ambaye anaenda kutoa hukumu ya kifungo au ya faini halafu anatembea kwa miguu; je, maisha yake yatakuwaje? Zaidi ni kuwa je, hadhi yake inakuwaje? Je, Serikali yake inamwaliaje?

Kwa hiyo, Utawala Bora ni pamoja na kutengeneza maslahi ya wale watu ambao tunawatumia, tunategemea wafanye haki. Bila shaka, hakimu kama huyu ni rahisi sana kuweza kununuliwa na asipofanya haki basi tusimlaumu kwa sababu hana njia nyingine ya kujikomboa kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mwingine hai, nasema sirudii yale yale kuwa, wanavijiji wetu, Halmashauri za Vijiji na Serikali za Vijiji hazijui Utawala Bora. Hazina taaluma ya Utawala Bora, kwa hiyo, yanafanyika mambo ambayo huwezi kuamini kama hawa ni viongozi sahihi. Nitatoa mfano; tuna Kijiji kimoja kinaitwa Kisingiri katika Kata ya Ilola, Jimbo la Solwa; Diwani wa Kata hiyo anaitwa Mheshimiwa Amos Malungu Mshandete, aliitisha mkutano wa hadhara ili kujadili maendeleo ya Kata.

Baada ya mazungumzo marefu, ikafika kipindi cha kuuliza maswali na wananchi wakataka kujua mambo yafuatayo; je, Mapato na Matumizi ya Serikali yetu ya Kijiji kwa muda wa miaka miwili iliyopita yalikuwaje? Je, Mapato na Matumizi ya Shule yetu ya Sekondari yako vipi? Je, Mapato na Matumizi ya Sungusungu yako vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ambayo yalitolewa na viongozi wa mkutano wa hadhara, yalikuwa hayaridhishi na wananchi wakaamua kuondoka polepole. Yalipotokea hayo, wale viongozi wakashutumu kwamba, wale waliokuwa wanaondoka ni Wapinzani wa Maendeleo. Kwa hiyo, waorodheshe majina yao na watiwe adabu na hilo lilifanyika na adhabu waliyopewa ni kuwekwa chini ya kalantini katika meno yao. Wanawekwa katika hali hiyo mpaka watakapolipa ama ng'ombe 20 au mbuzi 100.

Hali hiyo iliendelea mpaka wananchi kwa shida na tabu wakatekeleza mambo hayo ndio wakaachiliwa. Hayo yanayofanyika; kule kuna Mbunge na Mkuu wa Wilaya, hakuna hatua zinazochukuliwa; je, hii dhana ya Utawala Bora iko wapi? Tunawaachia wananchi wafanye wapendavyo wakati Serikali ipo; je, tunasemaje katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya matumizi mabaya ya vyombo vya habari vya umma. Tumekuwa na tabia kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi, kufanya hivi vyombo ni haki ya

chama kimoja cha siasa hapa nchini. Kipindi cha uchaguzi ndio inakuwa hali mbaya zaidi, unaweza kuona kwa mfano, *television* za kule Visiwani ni *greenery* tupu kama Ngorongoro hivi, kila siku nyimbo ndio hiyo hiyo tu.

Kabla ya uchaguzi, hata Dar es Salaam vyombo hivi vilikuwa na ukiritimba; wanaweza wasikujibu moja kwa moja lakini ukitaka shughuli yako itangazwe watakupandishia bei kubwa sana. Waswahili wanasema akukataaye hakwambii toka na haya yanafayika. Ninataka niseme kwamba, vyombo hivi sote tunalipia kodi au siyo jamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunalipa kodi, ikiwa mfanyakazi, mfanyabiashara, mkulima anapovitumia vyombo vile anavilipia kodi, kwa nini sasa iwe ni milki ya upande mmoja kwa njia ya hadaa, njia ya kificho na ya mlango wa nyuma? Kama hilo halitoshi, wakati wa kufanya maandamano au mikutano ya hadhara ni haki ya wanachama wa chama fulani, lakini mara nyingi unazungushwa unapangiwa katika maeneo ambayo hutaki kupite ili tu kukuvunja moyo. Hata mikutano ya hadhara mara nyingine unaambiwa hapa huwezi kufanya mkutano wa hadhara, kwa nini?

Unaambiwa babu hapa hakuna wanachama, sasa kama sina wanachama si ndio maana yake nifanye mkutano nitafute wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanatendeka, Serikali inajua na haichukui hatua yoyote. Kwa hiyo, ninasema haya mambo Watanzania tunayajua, lakini wakifanya wenzetu tunawanyooshea vidole. Kwa kweli litatufikisha mahali pabaya, lazima tulinde heshima ya nchi kwa sababu tumeamua kuwa na Vyama Vingi, basi kila chama tukipe haki yake ili nchi hii iendelee kuheshimika Duniani kote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kidogo kuhusu suala la wastaafu, sisi sote ama tumeshakuwa wastaafu au tutakuwa wastaafu na ni kusema sote tutakufa. Sasa unapoanza kuona yale maslahi ya wastaafu ni kuyachezea chezea, nafikiri itakuwa hufanyi jambo zuri. Leo nilikuwa natembelea asasi zile zisizo za Serikali (AZAKI), nikapita katika banda moja wakaniuliza Mheshimiwa wafanyakazi hawa wanaolipwa Sh.26,000 wataishije?

Nikawauliza sasa mtafanya nini? Wakasema tuwape elimu ili kabla hawajafikia kustaafu, wawe wamejiimarisha; wamejenga, wana maeneo yao ya kuishi mazuri. Nikasema huo mshahara wa kuyafanya hayo uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu lazima wapewe nafasi nzuri ili nao waweze kuishi kama binadamu wengine, kwa sababu hawa ni watu walioitumikia nchi hii wakiwa wazima na kwa moyo wote.

Cha kushangaza zaidi katika wastaafu ni kwamba, inapofika wakati wa kudai maslahi yao, wanakuwa wanayumbishwa sana.

Mfano mzuri tuliupata juzi hapa hapa Bungeni, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha akijibu suala la wastaafu wa Afrika Mashariki alisema kwamba, fedha zipo, *cheque* zimeshaandikwa lakini watu waje kuniona mimi binafsi!

Unashangaa; hivi Serikali hii ni ya mtu mmoja tu haina *organization chart* kuwa ukitoka hapa pita pale nenda pale; sasa kama Waziri hayupo maana yake watu hawana haki; huu ukiritimba unatoka wapi? Nafikiri suala hili la wastaafu jinsi linavyoendeshwa linavunja moyo na linakatisha tamaa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwa ufupi ni kuhusu walemavu. Walemavu ni sehemu muhimu sana na wana kila haki ya kuishi. Hapa Bungeni tuna wawakilishi wao, lakini kumchagua Mheshimiwa Mpanda kama mwakilishi wa walemavu, hujawasaidia walemavu bado.

Lazima kwanza hawa wenzetu wafanye kazi zao vizuri, hapa Bungeni lazima kuna mambo wawe nayo. Inafika mahali Mheshimiwa Mpanda ninamwonea huruma, anasema ovyo kwa sababu anatakiwa asome aweze kuweka kila kitu kichwani lakini hana.

Sasa walemavu wengine ambao hawapo Bungeni; je, wamepewa msaada gani? Je, majengo yetu ya ofisi tunayoyajenga hivi sasa yanawawezesha wale wastaafu kutembelea ofisi zetu vizuri au wanazitembelea kwa shida?

Hiyo ndio baadhi ya misaada ambayo tungependa hawa wenzetu walemavu wawe nayo. Bahati mbaya, wanahangaika hivyo hivyo wanafanywa kama ni sawa sawa na watu ambao si walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la maalbino vilevile, juzi Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir alitoa pendekezo lake, kwa kweli inasikitisha nchi kama hii ambayo tunasema inaendelea kwa ushirikina wao, watu wanauwa maalbino ambao hawana hatia. Tunaomba Serikali ichukue kila hatua kuhakikisha kwamba, maalbino wanaishi kama binadamu wengine bila ya kuwa na kero ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine dogo ambalo ningependa kulizungumzia kuhusu ajira. Suala la ajira pamoja na kwamba, Chama cha Mapinduzi kimesema kinatoa ajira 1,000,000 ifikapo 2010, bado tunaona ni tatizo kwa sababu kuna ajira ambazo wanapewa watu lakini siyo muhimu na haziwezi kuwasaidia.

Nitatoa mfano katika Wizara ya Kilimo walitaka kuajiri Mabwana Shamba 2,500
...

MWENYEKITI: Una dakika mbili, ulikuwa na dakika mbili.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa muda tuliobakiwa nao, haumtoshi Mheshimiwa Richard Ndassa ambaye angekuwa mchangiaji anayefuata kuweza kutoa mchango wake.

Napenda niwatangazie wachangiaji wetu wanne wa mwanzo kesho; kwanza kabisa atachangia Mheshimiwa Richard Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Magalle Shibuda na Mheshimiwa Kingunge Ngombare-Mwiru.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muda tulionao hatuwezi kuendelea kama nilivyosema hapo awali kwamba, mchangiaji wetu hawezi kuchangia.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu Kanuni ya 68(8), alipokuwa anazungumza mchangiaji wa mwisho, alimtaja Dr. Samson Mpanda kama Mbunge wa Walemavu na akasema kwamba, anaposema ovyo, nilikuwa nafikiri mchangiaji alikuwa anapaswa amwonee huruma mwenzetu kwamba, hakupenda kwanza ile hali imkute, lakini pia yeye ni Mbunge anayewakilisha Jimbo na wala siyo Mbunge wa Walemavu.

Kwa hiyo, nilitaka kumbukumbu ziwe sahihi.

MWENYEKITI: Ahsante, nadhani umetusaidia kwa kuliweka sawa suala hilo kwamba, Mheshimiwa Mpanda si Mbunge wa Walemavu ni Mbunge wa Jimbo kama tulivyo sisi wengine na hasemi ovyo, ile inakuwa michango yake ni kawaida yake anapozungumza.

Huyu ni Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, nafikiri yeye anatofautiana na wale ambao wanaingia kwa nafasi za Viti Maalum wale wanawake.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo napenda kuahirisha Bunge hili mpaka kesho saa tatu barabara asubuhi.

*(Saa 07.38 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 01 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*